ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID	-	SPIKA
1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais

9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13. Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais

19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Mihayo Juma N'hunga	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa pili wa Rais wa Zanzibar/ Jimbo la Mwera
22. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ / Jimbo la Micheweni
23. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
24. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
25. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
26. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
27. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Naibu Waziri wa Uwezeshaji,Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake

28. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
30. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
31. Mhe. Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
32. Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil	-	Uteuzi wa Rais
33. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe
34. Mhe. Ali Salum Haji	-	Jimbo la Kwahani
35. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)	-	Jimbo la Kijitoupele
36. Mhe. Ame Haji Ali	-	Jimbo la Nungwi
37. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	-	Nafasi za Wanawake
38. Mhe. Asha Abdalla Mussa	-	Jimbo la Kiwengwa
39. Mhe. Bahati Khamis Kombo	-	Jimbo la Chambani
40. Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-	Nafasi za Wanawake
41. Mhe. Hamad Abdalla Rashid	-	Jimbo la Wawi
42. Mhe. Hamida Abdalla Issa	-	Nafasi za Wanawake
43. Mhe. Hamza Hassan Juma	-	Jimbo la Shaurimoyo
44. Mhe. Hassan Khamis Hafidh	-	Jimbo la Welezo
45. Mhe. Hidaya Ali Makame	-	Nafasi za Wanawake
46. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)	-	Jimbo la Mtoni
47. Mhe. Jaku Hashim Ayoub	-	Jimbo la Paje
48. Mhe. Khadija Omar Kibano	-	Jimbo la Mtambwe
49. Mhe. Machano Othman Said	-	Jimbo la Mfenesini
50. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti	-	Jimbo la Mtopepo
51. Mhe. Makame Said Juma	-	Jimbo la Kojani
52. Mhe. Maryam Thani Juma	-	Jimbo la Gando
53. Mhe. Masoud Abrahman Masoud	-	Jimbo la Bububu
54. Mhe. Miraji Khamis Mussa	-	Jimbo la Chumbuni
55. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha	-	Jimbo la Mtambile

56. Mhe. Mohamed Said Mohamed - Jimbo la Mpendae
57. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini
58. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini
59. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake
60. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole
61. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani
62. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake
63. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake
64. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani
65. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani
66. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni
67. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde
68. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake
69. Mhe. Rashid Makame Shamsi - Jimbo la Magomeni
70. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Nafasi za Wanawake
71. Mhe. Said Omar Said - Jimbo la Wingwi
72. Mhe. Said Hassan Said - Mwanasheria Mkuu
73. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma - Nafasi za Wanawake
74. Mhe. Salma Mussa Bilal - Nafasi za Wanawake
75. Mhe. Shaib Said Ali - Jimbo la Chonga
76. Mhe. Simai Mohammed Said - Jimbo la Tunguu
77. Mhe. Sira Ubwa Mamboya - Uteuzi wa Rais
78. Mhe. Suleiman Makame Ali - Jimbo la Ziwani
79. Mhe. Suleiman Sarahan Said - Jimbo la Chakechake
80. Mhe. Tatu Mohamed Ussi - Nafasi za Wanawake
81. Mhe. Ussi Yahya Haji - Jimbo la Mkwajuni
82. Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Nafasi za Wanawake
83. Mhe. Wanu Hafidh Ameir - Nafasi za Wanawake
84. Mhe. Yussuf Hassan Iddi - Jimbo la Fuoni
85. Mhe. Zaina Abdalla Salum - Nafasi za Wanawake
86. Mhe. Zulfa Mmaka Omar - Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem - Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Kumi - Tarehe 22 Mei, 2017

(Kikao kilianza Saa 3.00 Asububu)

DUA

Mhe. Spika *(Zubeir Ali Maulid)* alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana na Wanawake na Watoto kwa mwaka 2017/2018.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha

Mhe. Maryam Thani Juma (Kny: Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake Habari na Utalii): Hotuba ya maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii kuhusu Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kazi Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto kwa mwaka 2017/2018.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 174

Kutekelezwa Ahadi Zinazotolewa na Mawaziri Ndani ya Baraza

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:

Katika Baraza la Wawakilishi kumekuwa kukitolewa ahadi mbali mbali na Mawaziri kutokana na hoja za wajumbe, hali inayoonekana kama ni masihara na utani kutokana nakutotekelezwa kwa ahadi hizo.

(a) Hatua gani Serikali inachukuwa kwa Mawaziri na Watendaji wao ambao wanatoa ahadi ambazo hawazitekelezi

(b) Kutotekelezwa kwa ahadi zinazotolewa ndani ya Baraza Waziri haoni kuwa ni sawa na kuvunja kanuni za Baraza hili.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais – Alijibu**:**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 174 lenye vifungu (a) na (b), naomba kutanguliza maelezo yafuatayo:-

Mhe. Spika, naomba kutoa maelezo mafupi kweli katika vikao vya Baraza la Wawakilishi kumekuwa kukitolewa ahadi mbali mbali na Mawaziri au Manaibu Mawaziri za utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa Kiongozi wa Serikali kutoa ahadi katika chombo hiki cha kutunga Sheria hakuna nafasi ya utani au masihara. Hivyo ni wajibu wetu sote tuliomo ndani ya vikao hivi kuelewa kuwa tunatakiwa kuwa makini ili kuweza kutekeleza majukumu yetu.

Baada ya maelezo hayo naomba kumjibu kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, Serikali imekuwa ikiwakumbusha Mawaziri na watendaji kuzipitia ahadi zinaotolewa na Wizara zao ili zitekelezwe na ndio wajibu wa kila kiongozi inapotokea kutotekelezwa wajibu huu, ni mamlaka za juu ya kiongozi huyo ndio zenye uwezo wa kuamua kwa mujibu wa taratibu zilizopo.

(b) Mhe. Spika, Kanuni za Baraza la Wawakilishi zimeweka mamlaka ya kufuatilia utekelezaji wa ahadi zinazotolewa na Wizara zinazosimamiwa na kamati husika. Hivyo, pamoja na Mawaziri wana jukumu la kutekeleza ahadi walizotoa kwenye Baraza. Kanuni zetu zimeweka jukumu hilo kwa kamati husika ili kuhakikisha kuwa ahadi hizo zinazotekelezwa ipasavyo. Utaratibu huu ni muhimu kwa kuwa baadhi ya ahadi hushindwa kutekelezwa kutokana na sababu za msingi kama vile ukosefu wa fedha kwa kipindi fulani. Kwa msingi huo, Kamati husaidia kufuatilia utekelezaji wa hadi hizo kwa kuikumbusha Wizara hasa pale hali ya fedha inaporuhusu.

Mhe. Spika, ni imani yangu viongozi wote wa nchi wanajitahidi kutekeleza ahadi zao na ikitokea baadhi ya ahadi kutotekelezwa ni vyema tukatumia utaratibu wa kukumbushia utekelezaji wa ahadi hizo iwe kwa maandishi au kuonana na kiongozi husika.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri na kwa vile aliwahi kutokea *backbencher* anajua kadhia hii, kwa kuwa ahadi zinazotolewa wananchi wanasikiliza.

a) Lini Serikali itaweka utaratibu wa kila ahadi inafuatiliwa na mimi nina ahadi karibu kumi mpaka kumi na tano, utakuwa tayari muda gani nikueleze ili uzichukulie hatua kwa Mawaziri ambao wako chini ya Ofisi yako.

b) Ahadi zisizotekelezeka ni tatizo la muda mrefu, Serikali inachukua hatua gani hasa kwa Mawaziri ambao hawataki kufika au kushuhudia kero zinazostahiki kwa wananchi pamoja na kulalamikiwa katika Baraza hili na nyengine hazihitaji hata fedha.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

a) Ni kweli ahadi zinazotolewa katika chombo hichi kitukufu ni ahadi ambazo wananchi wote wa Zanzibar na Tanzania kwa jumla wamekuwa wakizisikiliza na sio dhamira ya Serikali wala sio dhamira ya Wizara, wala sio dhamira kwa Waziri husika, lakini kila kiongozi ana dhamira ya kutekeleza ahadi ambazo amekuwa akizitoa katika chombo hiki husika. Kama ambayo nimejibu katika jibu langu la msingi ahadi mara nyingi inapotolewa bado viongozi waliokuwepo katika chombo hichi tuna wajibu wa kushirikiana, tuna wajibu wa kusaidiana na tuna wajibu wa kupeana maelekezo hasa pale tunapokwenda katika Kamati kadri ambayo uwezo wetu unakuwa unaturuhusu kama Wizara tumekuwa tukitekeleza ahadi hizo.

b) Mhe. Spika, Mhe. Mjumbe ameuliza ahadi ambazo hazitekelezeki. Tukiri ama tukubali kwamba inawezekana zikawa zipo ahadi ambazo hazitekelezeki kwa mujibu ambavyo anaona yeye, lakini kwa mujibu ambao Serikali inaona, Serikali haiwezi kusema jambo ambalo haliwezi kutekelezeka. Lakini kila jambo ambalo Serikali imekuwa ikiahidi imekuwa ikitoa umuhimu kutokana na mahitaji na tukio lililokuwepo katika taifa. Kwa maana hiyo ni wajibu wetu sote kutoa ahadi ambazo zimekuwa zikitekelezeka hasa kwa manufaa ya watu wetu.

Nakushkuru Mhe. Spika.

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, kuhusu utaratibu.

Mhe. Spika: Naomba ukae Mhe. Jaku.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza.

Mhe. Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na umma au wananchi wote wamepata na wamefahamu, pamoja na hayo swali langu lipo hapa.

Kwa kuwa kipindi cha Maswali na Majibu ni kipindi muhimu kwa watendaji wa Wizara mbali mbali au taasisi zinazohusika na tumeshuhudia hapa ukiacha Wizara ya Ardhi, Maji na Nishati na Wizara Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji ambao wanahudhuria watendaji wake kila mara au kila siku kwa masuala yao.

Je, hizi Wizara nyengine Mhe. Spika, kwa kuwa hawahudhurii. Wizara inatoa wito gani kwa Wizara zinazohusika na taasisi kuhudhuria siku za majibu na maswali ili wajue kinachozungumzwa kumsaidia Waziri.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Tunakubali na tunakiri kwamba wakati wa kipindi cha Maswali na Majibu watendaji wanapaswa kuwepo katika kipindi cha Baraza, lakini bado tuna mfumo ambao watendaji wetu wote wamakuwa wakitufuatilia taarifa zetu, wamekuwa wakifuatilia matukio yanayofanyika kupitia vyombo vyetu vya habari hasa kupitia *ZBC, TV* na Redio pale ambapo wapo katika mazingira yao ya kazi. Haitokuwa wakati mwengine jambo la busara kama kila wakati tunawahamishia watendaji wetu wote maofisini kufika hapa na kuacha shughuli nyengine maofisini kuwa zinasita kuja kufuatilia masuali na majibu.

Lakini yale masuala ambayo tumekuwa tukiahidi bahati nzuri tunawashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu Mawaziri wamekuwa wakifanya jitihada za kipekee hivi sasa kwa yale masuala ambayo wamekuwa wakiahidi kuyajibu kwa maandishi kuyarejesha katika taasisi zao na kuwaletea majibu ili kuweza kuhabarisha umma hata kama watendaji watakuwa hawajafika pale juu.

Nam. 89

Watuhumiwa Kusafirishwa kwa Gari za Abiria

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:

Kumekuwepo na malalamiko kutoka kwa watuhumiwa walioko rumande kupelekwa kwenye Mahakama kama vile Makunduchi kwa gari za abiria badala ya gari za Chuo cha Mafunzo.

(a) Je, suala hili ni kweli na kama ni kweli Serikali imechukuwa hatua gani kutafuta usafiri kwa watuhumiwa kufika Mahakamani.

(b) Kwanini Serikali isiweke bajeti ya kutosha kwa ajili ya kununuwa gari za kusafirisha watuhumiwa kwenda Mahakamani.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 89 lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo na kabla sijafanya kazi hiyo ya kujibu swali naomba nitoe maelezo yafuatayo.

Mhe. Spika, naomba ifahamike kuwa kazi ya kuwapeleka Mahakamani mahabusu inafanywa na Jeshi la Polisi, Chuo cha Mafunzo kina jukumu la kuwawapeleka Mahakamani wanafunzi wanaotumikia vifungo vyao ambao tayari wameshahukumiwa na iwapo watakuwa na kesi nyengine za kujibu Mahakamani.

Baada ya maelezo hayo mafupi, sasa naomba kujibu swali Na. 89 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

(a) Ni kweli mahabusu na wanafunzi waliokuwepo Chuo cha Mafunzo wanapelekwa Mahakamani kwa kutumia gari za abiria badala ya uhaba wa gari kwenye Chuo cha Mafunzo kuwapeleka Mahkamani. Kutokana na kuwepo Mahkama hizo katika maeneo mbali mbali kama vile Vuga, Mwanakwerekwe, Mwera, Mfenesini, Mkokotoni na Makunduchi kwa upande wa Unguja na Chake Chake, Wete, Mkoani na Konde kwa Pemba. Chuo cha Mafunzo hulazimika hutumia gari za abiria pamoja na gari za Polisi zinapokuwepo ili kuweza kuwapeleka katika Mahakama husika kwa wakati.

(b) Suala la upatikanaji wa gari maalum za kuwasafirisha watuhumiwa kwenda Mahakamani linahitaji kuwekewa mpango maalum kulingana na hali halisi ya kifedha na Mahakama zinazohusika na umbali uliopo. Chuo cha Mafunzo kimejipanga kutayarisha mpango huo ambao utabainisha gharama halisi za usafiri unaohitajika, gharama za uendeshaji ikiwemo mafuta na matengenezo pamoja na vifaa vya ulinzi kwa wanafunzi.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Waziri, nimshukuru kwanza kwa kukiri kuwa hili tatizo lipo, maana yake wengine sisi tunapopanda magari kuelekea kwetu Makunduchu tunashuhudi wanafunzi wale wanapelekwa Mahakamani kwa gari za abiria nimshukuru sana Waziri kukiri.

Lakini hapa alipokuwa anajibu anasema Mahakama kumekuwapo na upungufu wa magari, mimi nahisi kama pana upungufu wa mafuta, maana yake gari unaweza ukakodi hata kwa mwezi ikakutumikia, wangeweka bajeti ya mafuta kwa wanafunzi hawa na juzi tumepitisha bajeti hiyo na bahati katika kupiga buti hapa kidogo akapapatua Mhe. Waziri…

Mhe. Spika: Naomba uulize swali Mheshimiwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ni lini wataweka bajeti hii ili kuwanusuru wanafunzi wale kuhangaika katika gari za abiria. Hilo ni la kwanza.

La pili kimsingi tunapitisha bajeti na wananchi wanatusikia utaratibu huu kweli ni mzuri kumtendea mwanafunzi kama huyo.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalumu za SMZ: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mjumbe maswali yake ya nyongeza yenye (a) na (b) kama ifutavyo.

a) Kwanza aelewe kwamba nimekiri kuwepo kwa upungufu wa magari na ni kweli Mahabusu au wanafunzi wanapelekwa kwa gari ya abiria. Katika jibu langu mama nilisema kwamba Serikali inao mpango wa kuweka mpango madhubuti kwa ajili ya utafutaji wa gari pamoja na uwekaji wa bajeti katika kuhakikisha magari hayo yanakuwa yanafanya kazi kwa wakati.

b) Lakini jukumu la msingi au suala lake la msingi Mhe. Spika, niliema kwamba jukumu la kupeleka mahabusu Mahakamani ni jukumu la jeshi la Polisi, Mahabusu ni amana inayoletwa na Jeshi la Polisi kwenye Vyuo vya

Mafunzo. Kwa hivyo sisi kazi yetu ni kuwatunza wanapokuwepo Chuo cha Mafunzo, wakati wa kuwapeleka Mahakamani jukumu la msingi la jambo hili ni la Jeshi la Polisi. Hata hivyo kama nilivyosema katika jibu langu mama kwamba Serikali sasa hivi inao mpango madhubuti kwa ajili ya kutafuta gari na kuweka fedha za kutosha za mafuta kwa ajili ya kuwapeleka Mahakamani wanafunzi walioko Chuo cha Mafunzo.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Spika, kwanza nampongeza Mhe. Waziri kwa dhamira nzuri ambayo wanatwambia kwamba huko mbele fedha zikipatikana utaratibu huo utaondoka kwa ajili ya kufikisha salama katika Mahakama zetu wafungwa hao.

Lakini swali langu lipo hapa kwa kuwa Polisi wana dhamana ya kuwachukua watuhumiwa hao na kuwapeleka katika Mahakama ambazo zimetajwa kupitia gari za abiria,

Je. Mhe. Waziri haoni hiyo ni hatari wakati watuhumiwa wale wana kesi mbali mbali kuwaunganisha pamoja na raia wema kuja kuleta athari kwa maisha yao.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalumu za SMZ: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Serikali inaona athari hiyo na sisi kama Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ tutawasiliana na wenzetu wa Jeshi la Polisi ili kuona tatizo hilo wanakabiliana nalo vipi.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii kwa kuuliza swali la nyongeza kama ifutavyo.

Kwa kuwa Mhe. Waziri amesema katika majibu kwamba ana mpango madhubuti wa kutafuta hizi gari. Je, ni lini mpango huu madhubuti utakamilika.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mpango huu utakamilika wakati tutakapotekeleza bajeti ya mwaka 2017/2018.

Nam. 79

Unafuu wa Bei za Bidhaa kwa
Mwezi Mtukufu wa Ramadhani

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, kwanza nichukue fursa hii kuishukuru Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa umakini wake na kwa kuwajali wananchi hasa katika mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani. Niipongeze sana Serikali chini ya utawala wa Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein na Waziri makini Dkt. Khalid.

Mhe. Spika: Mheshimiwa unaliza swali lako.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kwa hiyo naliondosha swali, nimshukuru Mhe. Waziri. Mhe. Spika, ninaondosha utekelezaji ushafanyika. Mhe. Spika, utekelezaji ushafanyika tusimtese Waziri wetu ana kazi nyengine mbele.

Mhe. Spika: Umeliondoa. Ahsante.

(Mhe. Mjumbe aliyetaka kuuliza swali hilo ameliondoa)

Nam. 30

Hali ya Majengo ya Makumbusho

Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Aliuliza:

Katika miaka ya karibuni hali ya majengo ya makumbusho yetu imekuwa sio nzuri na baadhi ya vifaa vimezidi kuchakaa hivyo kupunguza hamu na haiba ya wananchi na watalii kutembelea maeneo hayo na kupunguza mapato muhimu kwa nchi yetu.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuimarisha makumbusho hayo katika kipindi cha 2017/2018.

(b) Je, ni wananchi na watalii wangapi waliotembelea makumbusho hayo.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa idhini yako napenda kumjibu Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa swali lake Nam. 30 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kabla ya kumjibu Mhe. swali lake naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, hali ya baadhi ya majengo ya Makumbusho yetu na maeneo ya kihistoria imekuwa sio nzuri na baadhi ya vifaa vimezidi kuchakaa, hivyo kupunguza hamu na haiba ya wananchi na watalii kutembelea maeneo hayo na kupunguza mapato muhimu kwa nchi yetu. Hata hivyo katika mwaka wa Fedha wa 2016/2017, Serikali imefanya matengenezo baadhi ya maeneo ya kihistoria yakiwemo Makumbusho ya Mnazi Mmoja, Makumbusho ya Pete, Ngome Kongwe, Manga Pwani, Dunga na Hamamni.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo mafupi sana naomba nimjibu Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa swali lake Nam. 30 kama ifuatavyo:

(a) Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imepanga kuimarisha maeneo yake ya kihistoria ili kuendeleza yawe katika hali nzuri na kuweza kudumu kwa muda mrefu zaidi. Katika mwaka wa fedha 2017/2018, Serikali imekusudia kuyafanyia matengenezo makubwa maeneo ya kihistoria ya Fukuchani kwa kulifanyia matengenezo jengo lenyewe na kuanzisha makumbusho mpya katika eneo hilo. Vile vile, Serikali imepanga kuyaimarisha maeneo ya kihistoria ya kwa Bi. Khole, Unguja Ukuu na makumbusho ya Chake Chake – Pemba.

(b) Mhe. Spika, kuanzia mwezi Julai 2016 hadi Machi 2017, Idara ya Makumbusho imepokea jumla ya wageni 33,136. Kati ya hao watoto ni 309 na watu wazima 12,046. Pia wageni wa ndani waliotembelea makumbusho na maeneo ya kihistoria ni wanafunzi ni 18,443, wageni maalumu 186, watu wazima 2,129 na watoto 23.

Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa: Ahsante Mhe. Spika, nashukuru sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri lakini nilikuwa na swali moja la nyongeza kidogo nataka kujua.

Katika Mwaka 2016/2017 ni kiasi gani cha fedha kimeingia Serikalini kupitia utalii.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante Mhe. Spika, Mhe. Spika kwa idhini yako napenda kumjibu Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa, swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, kwa kuwa swali hili ni la takwimu na sisi tunatakiwa tujibu majibu ya uhakika. Kwa hivyo namuomba Mheshimiwa jibu nitamjibu kwa maandishi. Ahsante *(Makofi)*

Mhe. Ali Khamis Bakar: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kwa kuniona na kunipa nafasi ya kuweza kuuliza swali moja na nyongeza.

Kwanza nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa majibu ambayo ametupatia lakini naomba niulize swali dogo. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri kwa kuwa swali la magofu huingiza taifa fedha za kigeni ambazo ni muhimu sana katika nchi yetu kwa kukuza uchumi. Je, magofu yaliyo Chwaka-Tumbe katika jimbo langu ni lini yataimarishwa ili kukuza hadhi ambayo ilikuwepo tangu zamani.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante Mhe. Spika, Mhe. Spika kwa ruhusa yako napenda kumjibu swali lake la nyongeza kama Mhe. Ali Khamis Bakar kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, kama nilivyojibu katika swali mama au jibu mama kwamba sasa hivi tumo katika utaratibu wa kuyafanyia ukarabati na kuyaendeleza magofu haya ili yalete haiba nzuri kwa wananchi wetu lakini na watalii ambao wanaokuja nchini mwetu.

Namuahidi Mhe. Ali Khamis Bakar kwamba, tumo katika utaratibu wa kuyafanyia matengenezo magofu haya na likiwemo gofu lake na Tumbe katika jimbo lake la Tumbe. Kwa hivyo nimuombe tu Mheshimiwa azidi kustahamili na tulalifanyia kazi. Ahsante *(Makofi)*

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru Mhe. Spika, na mimi awali ya wote napenda nimshukuru Mwenye ezi Mungu kwa kuniamsha salama salmini.

Mhe. Spika, kwa majibu nampongeza sana Mhe. Naibu Waziri lakini kwa sababu sioni matangazo yanayotangazwa katika maeneo yetu yote, sehemu za

utalii wala wapi. Nataka kumuuliza Mhe. Naibu Waziri mtalii wa nje au mtalii analipa shilingi gapi katika viingilio na mtalii wa ndani analipa shilingi katika sehemu zetu za utalii.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Suleiman Sarahan Said swali lake kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, kuna *fees* ambazo wanalipa wageni wetu kutoka nje yaani watalii, lakini pia kuna *fees* ambazo wanalipa wazawa au Wazanzibari. Nimjibu tu Mhe. Mwakilishi kwamba *fee* ya wageni sina uhakika nayo, lakini *fee* ya wazawa wanalipa shilingi 1,000/- wakati wanapoingia katika magofu yetu, lakini ninamuhakikishia Mheshimiwa kwmaba nitalifuatilia kwa kina na nimpe majibu sahihi ya wageni *fee* gani tunapata. Ahsante. *(Makofi)*

Nam. 43

Vibali vya Kazi kwa Wageni

Mhe. Abdalla Maulid Diwani - Aliuliza:

Kwa kuwa na kuwepo ugumu wa upatikanaji wa fursa za ajira kwa Wazanzibari na hivyo kupelekea malalamiko kwa vijana wa Zanzibar, kutokana na nafasi nyingi za ajira kupewa wageni kwa sababu ya utashi wa wamiliki wa taasisi hizo wakati wapo Wazanzibari wenye sifa za kupewa nafasi hizo na hawapewi.

(a) Kuna wafanyakazi wangapi toka nje ya nchi ambao wanafanyakazi hapa Zanzibar.

(b) Ni sifa gani za ziada walizokuwa nazo wageni za kupewa ajira ambazo Wazanzibari hawana.

(c) Je, kwanini Serikali inatoa vibali vya kazi kwa wageni ambao wanafanyakazi ambazo zinaweza kufanywa na wazawa.

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto - Alijibu:

Bismilah Rahman Rahim Mhe. Spika, awali ya yote kwanza naomba niendelee kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye na yeye anaendelea kunipa pumzi zake

na asubuhi hii nikaweza kusimama katika Baraza lako Tukufu nikiwa katika hali ya uzima na afya njema.

Mhe. Spika, baada ya kumshukuru Mwenyeezi Mungu kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Abdalla Maulidi Diwani swali lake Nam. 43 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi naomba nitoe maelezo mafupi.

Mhe. Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Ajira Nambari 11 ya mwaka 2005, hakuna muajiri anayeruhusiwa kuajiri mfanyakazi wa kigeni kwa utashi au umiliki wa taasisi yake isipokuwa pale hakuna raia wa hapa nchini (kwa maana ya Mtanzania) mwenye sifa zinazotakiwa kujaza nafasi hiyo. Pia kwa upande mwengine Sheria ya Kukuza na Kulinda Vitega Uchumi ya Zanzibar ya mwaka 2004, muajiri anaruhusiwa kuajiri mfanyakazi wa kigeni anayemtaka katika nafasi ya uongozi. Hali hiyo ina maana kuwa uajiri wowote wa wafanyakazi wa kigeni hapa Zanzibar unafanywa kwa mujibu wa Sheria na taratibu zilizopo na sio kwa sababu ya utashi wa mmiliki wa taasisi husika.

(a) Hadi kufikia mwezi Machi, 2017 wapo jumla ya wafanyakazi 1,026 wa kigeni ambao wameajiriwa hapa Zanzibar hasa katika sekta ya utalii na miradi maalum ya ushirikiano baina ya Serikali na Washirika wa Maendeleo katika nyanja za afya, elimu, miundombinu, mawasiliano, habari, michezo na hata sekta ya utalii.

(b) Katika utaratibu wa kawaida muajiri anapaswa kutangaza nafasi za ajira kupitia vyombo vya habari hapa nchini na iwapo hakupatikana mwananchi mwenye sifa zilizotajwa, muajiri anaruhusika kuajiri mfanyakazi wa kigeni. Miongoni mwa sifa za ziada ni pamoja na viwango vya elimu, ujuzi na uzoefu katika kada na fani husika kwa maeneo yaliyoyatajwa.

Wafanyakazi wa kigeni huajiriwa pale tu sifa kwa nafasi zinazotakiwa kujazwa kwa Wazanzibari wamekosa sifa hizo.Kwa mujibu wa Sheria ya Ajira Namba 11 ya mwaka 2005 Kifungu 36 (1) (a) na (b) kinasema naomba kunukuu, “hakuna mwajiri anayeruhusiwa kuajiri raia wa kigeni isipokuwa katika mazingira yafuatayo”:-

(a) Iwapo hakuna Mtanzania wenye sifa zinazohitajika kwa nafasi hiyo.

(b) Iwapo nafasi ya uongozi ambayo muajiri ameruhusiwa kuajiri mtu kutokana na matakwa yake, kama ilivyoelezwa kwenye Sheria ya Kukuza na Kulinda Vitega Uchumi ya Zanzibar ya mwaka 2004.

Mhe. Spika, naomba kutoa wito hasa kwa wazazi ya kwamba ni busara kuwatayarisha vyema vijana wetu kielimu, kiujuzi na fani ili waweze kufikia viwango vinavyokubalika na kuingia kwenye ushindani wa soko la ajira na pia kwa kuzingatia Itifaki la Soko la Ajira la Afrika ya Mashariki.

(c) Mhe. Spika, hakuna ajira au kazi isiyohitaji sifa za kitaalamu na ujuzi hata kama ni huduma za usafi, utunzaji wa bustani, ulinzi na nyingine zinazofanana na hizo. Pamoja na sifa za kielimu na kitaalamu lakini pia kutengeneza mvuto wa kibiashara kwa mteja wakati wa kutoa huduma inayotakiwa jambo ambalo ni adimu kwa vijana wa Zanzibar.

Pamoja na utangulizi huo Serikali kupitia Wizara yangu haitoi vibali vya kazi kwa wafanyakazi wa kigeni katika maeneo ambayo wapo wazalendo wenye sifa hizo. Kwa maelekezo ya Sheria ya Ajira Namba 11 ya mwaka 2005, kibali cha kazi hakitatolewa pale ambapo nafasi hiyo ya ajira inaweza kujazwa na mzalendo. Serikali inalazimika kutoa vibali vya wafanyakazi wa kigeni ambazo sifa kwa kwa Wazanzibari zimekosekana.

Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Abdalla Maulidi Diwani: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mnakashi mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri.

1. Je, yuko tayari Waziri kufuatana na mimi na kumuonesha wageni ambao hawana sifa za wafanyakazi ambao zinakosekana hapa Zanzibar wanafanyakazi na atachukua hatua gani nikithibitisha hilo.

2. Yuko tayari kufuta vibali vya wafanyakazi ambao hawana sifa lakini wamepewa vibali hivyo wanafanyakazi hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana na Watoto: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi wa swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

(a) Niko tayari kufuatana na Mhe. Mwakilishi kwenda kuangalia hao watu.

(b) Niko tayari kwenda naye nikaangalia hao watu ambao wameajiriwa na wakati sifa hizo za Wazanzibari wanazo, basi niko tayari kushirikiana naye na kuhakikisha kwamba nafasi zile zinachukuliwa na Wazanzibari. Ahsante.

Mhe. Bihindi Hamad Khamis: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuweza kumuuliza Mhe. Naibu Waziri maswali mawili ya nyongeza.

Mhe. Naibu Waziri, kwanza kabisa nikushukuru kwa majibu yako mazuri lakini pia nikuulize maswali mawili ya nyongeza.

(a) Mhe. Naibu Waziri, Wazanzibari wengi huwa wanakwenda kutafuta ajira nchi za Arabuni lakini huwa wanapata uzalilishaji mkubwa na wengine hadi kufa. Je, wizara yako ina mpango gani kutoa taaluma kwa Zanzibari ili kadhia hiyo isiwafike.

(b) Mhe. Waziri je, wizara yako imeshirikianaje na Ubalozi wa Arabuni ili kuweza kuyajua matatizo haya na kuwaondoshea na kuyapatia ufumbuzi. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Mheshimiwa hili swali haliendani na swali la msingi. Ni swali la ajira la Arabuni lakini Waziri mwenyewe nafikiri kama utakuwa na majibu ninaweza nikaruhusu ujibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana na Watoto: Mhe. Spika kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Bihindi Hamad Khamis swali lake la nyongeza lenye sehemu (a) (b) kama ifuatavyo:

(a) Mhe. Spika, napenda kumhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba Wizara yangu inashirikiana vizuri pamoja na Mabalozi wa Tanzania waliokuwepo katika nchi hizo ambazo watu wetu wanakwenda wakifanya kazi. Lakini Mhe. Spika kabla sijamjibu

swali lake (b) naomba nitowe wito kwa Baraza lako hili Tukufu kupitia kwa Waheshimiwa Wawakilishi wenye majimbo na vitu maalum katika Mikoa yao hata Majimbo yao.

Kwamba kwakuelimisha wapiga kura wao wanapokwenda kufanya kazi katika nchi hizo, tunawaomba sana waweze kupitia katika wizara yetu ili waweze kutoa taarifa zao. Wanapotokea matatizo kule iwe wizara ni vizuri sana kuweza kupata fursa mara moja kuweza kujua matatizo yanayowakumba wananchi wetu. Kwa sababu Mhe. Spika, kuna tabia imetendeka sasa hivi, wananchi wetu wanapokwenda kufanya kazi kule wanashindwa kupitia Wizarani na wanaposhikwa na matatizo ndipo wanapofika wizarani. Kwa hivyo wizara tunafanya kazi lakini yanachukua muda mrefu kupata majibu ya mtu yule kutokana na kwamba hakuweza kupitia wizarani na tukapata maelezo yake.

Mhe. Spika, Mhe. Mwakilishi arudie swali lake jengine.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri mwenyewe kwa majibu ya nyongeza.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, ahsante napenda nimshukuru Naibu Waziri wangu kwa jitihada ya kuweza kujibu. Swali la nyongeza alilouliza nadhani anataka kujua kama tunachukua hatua gani kwa kupitia Mabalozi.

Mhe. Spika: Mhe. Kaimu Makamu wa Rais naomba urudi katika kiti chako. Mhe. Waziri naomba uendelee na majibu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Mhe. Waziri endelea na majibu.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mheshimiwa swali alilouliza ni kwamba anasema tunashirikiana naje kuangalia ni watu waliokwenda na wamepata matatizo.

Nataka kukuthibitishia kwamba mpaka sasa hivi tuna kesi kiasi tatu ambazo zinafuatiliwa kwa karibu kabisa ya watu ambao wamefanyiwa kadhia katika nchi za nje. Wengine ambao wamefariki na kurejeshwa na wengine ambao wamekwenda tunaendelea kufuatilia kila sehemu kwa kutumia mawakala binafsi, ambao wamekwenda pasipo pitia kwetu lakini pia tunashukuru Serikali kwa kuweza kuweka Mabalozi katika maeneo hayo, tutaendelea

kufuatilia kwa karibu zaidi zile kesi zote ambazo zimeletwa ambazo hasa zimeletwa ikiwa watu wamefariki.

Lakini pia hata wale ambao wanakwenda tunawasihi sana wazazi msipeleke watoto pasipo kutaka ushauri. Sisi tunapowasiliana nao tunaandika mikataba kabisa, tunawaelimisha, tunahakikisha wanakwenda kule na wakifika kule wanaweza kufanya kazi na kurudi kwa ajili ya mapumziko na tunawatafutia utaratibu wa kuhakikisha kwamba wanapokuwepo nje wanaweza kujiunga na Mfuko wa *ZSSF* kwa ajili ya kuweka akiba yako watakapokuwa wamechoka katika kazi hizo kwa hiyo.

Kwa hivyo naomba ushirikiano wa karibu ili tuweze kuendelea kufanya kazi vizuri. Ahsante sana

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana, Mhe. Spika, kwanza kabla ya kuuliza swali hili naomba ni-*declare interest* kuwa mjumbe wa Kamati hii.

Lini atafanya angalau kuwachukua Wajumbe wa Kamati kwenda kuhakikisha usalama wa wafanyakazi waliokuwa Qatar kwenda kuhakikisha usalama wao wananchi hao.

Mhe: Spika: Mhe. Waziri usalama wa wafanyakazi wetu waliokuwepo Qatar.

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana,Wanawake na Watoto: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu swali lake la nyongeza Mhe. Jaku Hashim Ayoub kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba niko tayari kuichukua Kamati kwenda kuangalia, lakini kutokana na ufinyu wa bajeti sasa hivi itakuwa ni ngumu. Lakini In shaa Allah Mwenyezi Mungu akitujaalia bajeti ikituruhusu basi niko tayari kuwachukua Wajumbe wa Kamati kwenda kuangalia usalama kazini.(*Makofi*).

Nam. 19

Uendelezaji wa Uvuvi kwa Utoaji wa Elimu

Mhe. Said Omar Said – Aliuliza:-

Mhe. Spika, itakumbukwa kwamba serikali ilianzisha utoaji wa elimu ya uvuvi katika Chuo cha Uvuvi hapo Lumumba kwa lengo la kuwapatia wanafunzi

wetu taaluma ya uvuvi na hivyo tunaweza kupata wanafunzi wenye taaluma hiyo.

Je, serikali itawaendelezaje wale wenye taaluma hiyo kwa faida ya Wazanzibari.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi - Alijibu:

Mhe. Spika**,** kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 19 kama ifuatavyo:

Kwanza naomba nitoe maelezo mafupi kabla ya kujibu swali lake kama ifuatavyo:

Mhe. Spika: Waheshimiwa samahani sana upande wa serikali naomba mumpe nafasi Mhe. Waziri ajibu.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, ni kweli Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilianzisha mitaala maalum ya mchepuo kwa kuendeleza sekta ya uvuvi nchini kwa iliokuwa Skuli ya Sekondari Lumumba tokea Mwaka 1977.

Lengo la kuwapatia wanafunzi hao msingi wa taalma hiyo ya uvuvi ilikuwa iendane sambamba na baadae kuweza kuwaunganisha katika Vyuo Vikuu vya Uvuvi kwa lengo la kuwaendeleza Wazanzibari kupata taaluma ya aina hiyo.

Mhe. Spika, idadi ya wanafunzi inayokaribia 34 kwa mwaka waliunganishwa na mitaala hiyo kwa muda wa miaka karibu minne ambao walianzia kidatu cha kwanza *(Form I)* hadi kufika kikato cha nne *(Form IV)*, pamoja na mafunzo mengine ya kawaida yaliyokuwa yakitolewa katika Skuli hiyo ya Sekondari Lumumba.

Mhe. Spika, sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam . 19 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwa kuwa mpango kamili wa kuwaendeleza vijana hao ulitakiwa kwenda pamoja na baadae kuwawezesha kujiunga na Vyuo Vikuu kwa kukamilisha taaluma hiyo, jambo ambalo halikuwezekana kwa sababu mpango huo haukuweza kuendelea kama ulivyopangwa na hivyo kusababisha mambo yafuaatyo:-

1) Baadhi ya wanafunzi hao walipatiwa ajira kupitia Wizara ya Elimu kwenye Taasisi mbali mbali na Serikali kwa upande wa Unguja na Pemba.

2) Mhe. Spika, na baadhi ya wanafunzi walijiendeleza wenyewe katika mitaala ya sayansi nje ya sekta ya uvuvi.

Mhe. Spika, kwa hivi sasa kupitia Wizara ya Kilimo imeanzisha zoezi kama hilo kwa wavuvi wazalendo, ikishirikiana na Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu kusomesha masomo ya muda mfupi kwa wavuvi vijana 69 (MENAI 20, MIMCA 25, PECCA 21) Mabaharia 2 na 1 kutoka kisiwa cha Kojani katika awamu tofauti kuanzia mwaka 2014 hadi 2016 katika Chuo ha Uvuvi Mbegani Tanzania Bara ambao baadae huendelezwa na ajira zao wenyewe.

Mhe. Omar Ali Said: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii basi nimuulize Mhe. Waziri swali moja tu la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Waziri huoni kwamba Wizara yako kuanzisha mradi wa maendeleo ya nchi bila ya kujipanga ni kudhoofisha juhudi za wakwezi na wakulima wa nchi hii.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, kwanza utaratibu huu ulianzishwa mwaka 1977 na ilikuwa ni vyuo viwili; Chuo na Fidel Casro kilipangwa kuwa Chuo cha Kilimo na Lumumba ilipangwa kiwe ni Chuo cha Uvuvi. Bahati mbaya wakati huo kilitengenezwa kitengo kidogo tu katika Chuo cha Lumumba kufanya kazi hii ya kutoa taaluma ya uvuvi. Kwa hivyo sio mpango wa Wizara, ulikuwa ni mpango wa Serikali kwa jumla lakini ni mpango ambao kwa bahati mbaya haukupangwa vizuri katika ule mpango mzima wa kwamba watoto hawa wafuzwe na waendelezwe mpaka juu.

Mhe. Spika, ndiyo maana kama mnafuatilia hotuba ya Mhe. Rais katika Baraza hili la Wawakilishi wakati alipozindua alisema kwamba, "Sekta ya Uvuvi inahitaji kupewa msukumo maalum". Katika kutekeleza hilo Baraza la Mapinduzi hivi karibuni lilipitisha maamuzi kwamba Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi na Wizara ya Elimu ikae sasa ili itengeneze mitaaala ambayo itapelekwa kwenye maskuli mbali mbali ya kufundishwa sekta ya uvuvi. Maamuzi hayo yapo na tuko karibu kuyatekeleza, tutaunda Kamati maalum na hatimaye tutarudi kwenye Baraza la Mapinduzi kupata idhini juu ya mitaala hiyo itakapokubalika ili iweze kufundishwa ndani ya maskuli yetu.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza kwa Wizara hii ihusianayo na masuala ya Mali Asili, Kilimo, Mifugo na Uvuvi.

Mhe. Spika, kwa kuwa serikali ina mpango wa kununua meli ya uvuvi ili tuweze kuvua bahari Kuu. Je, serikali imejipanga vipi katika kuwaandaa vijana na mafunzo ya uvuvi wa bahari kuu.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, kwanza nimshukuru sana Mhe. Mwakilishi kwa swali lake zuri.

Pili nikubaliane na yeye kabisa kwamba Serikali katika mipango yake hata ukisoma kwenye hotuba ya Mhe. Rais, ukisoma kwenye muongozo wa CCM unaeleza wazi nia ya Serikali katika kuwaendeleza vijana wetu kuingia katika uvuvi wa bahari Kuu.

Mpango wa Serikali kwanza ni kutaka hii sekta ya uvuvi sasa irasimishwe kwa wananchi. Huko nyuma wavuvi wote wa bahari kuu ni wageni. Kuna meli kama 100 mpaka 60 wakati mwengine mpaka 200, lakini zote zilikuwa ni za kigeni zinavua na kuchukua samaki na kuondoka.

Ndiyo maana hivi karibuni Serikali ikaanzisha Kampuni ya Uvuvi ya *ZAFICO* ambayo tayari imeshaanzishwa na karibuni tunategemea atapatikana Mwenyekiti wa Bodi. Nashukuru sana mashirika ambayo yameshiriki katika kununua hisa katika Kampuni hii na sasa hivi wanazo karibu bilioni 7. Moja ya madhumuni yake ni mambo mawili:

1) Kuhakikisha kabisa sekta ya uvuvi, serikali na yenyewe inashiriki kikamilifu kwa kupitia Shirika lake.

2) Kampuni hii itoe taaluma kwa vijana wetu waweze kuvua katika maeneo ya bahari kuu lakini siyo bahari kuu tu, hata maeneo yanayovuliwa hivi sasa tusivue tena kienyeji na tuvue kisasa ili mapato yaweze kuongezeka na ajira iweze kuongezeka.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuuliza swali la nyongeza.

Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kumuuliza swali dogo la nyongeza.

Mhe. Waziri katika vijiji ambavyo kwamba vinajishughulisha na uvuvi wananchi wakipewa taaluma ya uvuvi kupitia njia ya sinema. Mpango ule umeondoka.

Je, ni lini mpango ule utaanzishwa tena ili kwamba wananchi waonyeshwe ile sinema na kuacha kuvua uvuvi haramu na kuyatunza mazingira ya baharini.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante Mhe. Spika, kwanza ni kweli kabisa huko nyuma tulikuwa tukitumie sinema kwa kuwaelimisha wananchi. Lakini kama unavyofahamu sasa hivi Mhe. Spika, nyumba zetu karibu asilimia 60 zina televisheni na tunazo *program* ambazo tunazitumia kwenye televisheni. Vile vile tunazo *program* ambazo tunazitumia kwenye redio. Lakini bado tunazo *training program* ambazo tunazozifanya.

Nitatoa takwimu za *training program* tunazozifanya katika hotuba yangu ili muone kwa kiasi gani tumeweza kuwawezesha watu wetu kupata taaluma.

Lakini suala la Uvuvi wa haramu Mhe. Spika, ni suala la tabia mbovu ya watu wetu, pamoja na taaluma waliyonayo, pamoja na athari tunayoipata kubwa ya uvuvi haramu, lakini bado watu wetu hawajakubali kushirikiana na vyombo vyetu katika kupambana na uvuvi haramu. Kwa hivyo Sio suala la sinema na taaluma, ni suala la hulka ya watu wetu kutokutunza mazingira yetu na hilo ndiyo tatizo la msingi.

Naomba tuli-*address* kwa pamoja kama ni viongozi kwamba ni tatizo la msingi na ni tatizo kubwa sio dogo, ukenda sasa hivi matumbawe yote yamemalizika. Zanzibar hii ndiyo inayoongoza duniani kwa kuwa na matumbawe mengi. Leo katika matumbawe zaidi ya milioni kumi yaliyokuwepo yamebaki kama laki moja na tisini na tisa elfu na bado tunaongoza katika dunia. Lakini nenda kaangalie hali iliyokuwepo sasa hivi, yote yamepigwa mabomu, yameharibika samaki hawaonekani.

Tunao wajibu mkubwa sana Wazanzibari wote na Watanzania kwa jumla kutunza mazingira yetu ya baharini na ya nchi kavu ili vizazi vyetu viweze kufaidika baadae na mapato yaweze kupatikana katika nchi.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru Mheshimiwa Ahsante sana. Kwanza nimsifu Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri.

Mhe. Spika, nikikumbusha kwamba katika bahari yetu tuna samaki wakubwa wazuri kama majodari, nduwaro, kambisi, *kingfish*, ni samaki gani aliyekuwa

hatarini kuondoka au wapo wachache. Ni samaki wa aina gani ambaye ni wachache kuweza kuhama au kuondoka kabisa.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, nakushukuru sana na nimshukuru na Mhe. Sarahani kwa swali lake. Hili swali kidogo linahitaji takwimu na taarifa sahihi.

Naomba nimpatie taarifa sahihi na za kitaalamu ili niweze kumpatia majibu sahihi.

Nam. 106

Mrundikano wa Wagonjwa wa Macho
Katika Hospitali ya Mikunguni

Mhe. Omar Seif Abeid - Aliuliza:-

Mhe. Spika, Hospitali ya Mikunguni ambayo inatoa huduma ya matibabu ya macho inakabiliwa na tatizo kubwa la mrundikano wa watu unaosababishwa na ufinyu wa jengo na eneo sambamba na upungufu wa wafanyakazi.

(a) Je, serikali ina mpango gani wa kuimarisha Hospitali hiyo kwa kuongeza ukubwa wa jengo hilo au kupatiwa jengo jengine ambalo litakua na nafasi kubwa sambamba na kuongeza huduma za upasuaji macho angalau siku 4 kwa wiki jambo litakalosaidia kupunguza msongomano wa wagonjwa.

(b) Je, wagonjwa wangapi hukimbilia hospitali hiyo pamoja na kwamba zipo hospitali nyengine zinazotoa huduma kama hizo.

(c) Je, serikali ina mpango gani wa kutenga fedha kwa ajili ya kununua miwani kwa ajili ya wagonjwa wa macho ambao hufanyiwa *"operation*" na hawana uwezo wa kununua miwani hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mwakilishi swali lake Nam. 106 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza kabisa naomba nitoe shukurani za dhati kwa Mhe. Omar Seir Abeid kwa kuona umuhimu wa Hospitali ya Mikunguni pamoja na

huduma na changamoto zake. Nimshukuru pia na kumpongeza sana Mhe. Hamza Hassan Juma pamoja na wananchi wa Jimbo la Kwamtipura kwa kuvumilia hali ya kuongezewa uzito wa huduma wa Hospitali ya Mikunguni lakini pia kwa mashirikiano yao makubwa kwa wafanyakazi na wagonjwa wanaofika kupata huduma mbali mbali ikiwemo huduma ya macho katika hospitali hiyo ya Mikunguni.

(a) Mhe. Spika, Hospitali ya Jimbo la Kwamtipura iliyopo Mikunguni imekuwa ni tegemeo kubwa kwa wagonjwa wa maeneo hayo na mengine ya jirani, hasa baada ya kupelekwa huduma za macho kutoka Hospitali ya Mnazi mmoja. Hii ilitokana na kuharibika kwa jengo la macho katika Hospitali ya Mnazi Mmoja miaka kama mitatu iliyopita.

Hata hivyo hali hii ni ya muda tu na Wizara ya Afya tayari imo katika taratibu za kulifanyia matengenezo makubwa jengo la huduma za macho katika Hospitali ya Mnazi Mmoja na kutoa nafasi zaidi kwa huduma nyengine za afya katika kituoni au Hospitali hii ya Mikunguni. Huduma zote za upasuaji wa macho kwa sasa bado zinaendelea kufanyika na kutolewa katika Hospitali ya Mnazi Mmoja.

(b) Mhe. Spika, Hospitali hii kwa sasa inapokea wagonjwa 70 hadi 100 wa macho kwa siku wakiwemo wale wa moja kwa moja na wale waliopata rufaa kutoka vituo vyengine vya Afya hapa Unguja.

(c) Mhe. Spika, serikali kupitia Wizara ya Afya imekuwa ikitoa huduma ya macho ikiwemo ya miwani bure kwa wananchi wake. Ni kweli kwamba upatikanaji wa huduma ya miwani umekuwa na changamoto kidogo kutokana na kiwango kikubwa cha mahitaji ya huduma hii kwa wananchi walio wengi. Hali hii inapotokezea, wagonjwa hutakiwa kuchangia ununuzi wa miwani hiyo.

Mhe. Spika, Wizara ya Afya kwa kushirikiana na wahisani mbali mbali imekuwa ikitoa miwani bila ya malipo katika vipindi tofauti kupitia huduma za kawaida hospitalini au wakati wa kambi maalum za huduma za macho katika maeneo mengine mbali mbali. Serikali kupitia Wizara ya Afya itaongeza utoaji wa huduma hii bila ya malipo kadri upatikanaji wa fedha utakavyowezekana.

Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

Nashukuru sana kwanza Mhe. Naibu Waziri wa Afya kwa majibu mazuri ambayo tumeyasikia na mimi yamenifurahisha. Lakini kuna kitu kidogo naomba nimuulize kwa kuwa idadi ya wagonjwa pale ni wengi, ukenda utajionea jinsi walivyokuwa ni wengi wenye mahitaji yale na idadi ndogo ya wafanyakazi waliopo pale.

a) Je, Wizara ina mpango gani wa kuongeza wafanyakazi pale ili kupunguza ule msongamano wa wagonjwa wanaokwenda pale kusubiri zile huduma. Kwa sababu wafanyakazi pale waliopo ni kidogo.

b) Tumekiri kwamba habari ya miwani kuna mchango unatakiwa kidogo utolewe wakati wa kupewa hiyo miwani pale inapopatikana. Lakini kuna wananchi wetu wengine ni maskini kabisa. Je, Wizara yako ina mpango gani kwa wale watu ambao hawajiwezi kabisa kuwapa kipaumbele ya kuwapa miwani pale wanapotokewa na tatizo hilo wakafika hospitalini pale. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Omar Seif Abeid swali lake la nyongeza lenye (a) na (b) kama ifuatavyo:

a) Mhe. Spika, kutokana na idadi ya wafanyakazi ambao tumepewa ruhusa na serikali kuongeza, Wizara imekusudia kupeleka wafanyakazi watano (5) katika Hospitali ya Mikunguni.

b) Mhe. Spika, inapotokea hali kama hii ya kukosa miwani, maana siyo mara nyingi, mara nyingi miwani za akiba zinakuwa zipo. Sasa inapotokea hali kama hii ya kukosa miwani kuwa imemalizika, mara nyingi wagonjwa wale ambao wanahitaji miwani wanaambiwa wachangie kupata miwani. Lakini yule ambaye anaonekana yupo katika hali mbaya basi Wizara huwa inafanya kila linalowezekana kuhakikisha kwamba anapata miwani. Lakini hata hivyo mara nyingi tunapata miwani kutoka kwa wafadhili mbali mbali na inakuwepo kutoa huduma kwa wananchi wetu.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Spika, kabla sijauliza swali langu dogo la nyongeza ningeomba uniruhusu niweke *Hansard* sawa ya muuliza swali Nam.

106 pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri. Katika swali Mhe. Naibu Waziri alipojibu wameandika Hospitali ya Mikunguni.

Mhe. Spika, Mikunguni hatuna hospitali tuna soko ambalo linaitwa soko la Mapinduzi. Hospitali hii inaitwa ni Hospitali ya Kwamtipura ambayo ipo Shehia ya Mkele. Baada ya kuweka *Hansard* sawa Mhe. Spika, nataka nimuulize Mhe. Naibu Waziri wa Afya, kama ifuatavyo:

Mhe. Naibu Waziri kama ulivyojibu swali lako hospitali hii kweli ina mrundikano wa watu na jitihada zinafanyika. Mimi nilitaka kujua tu. Je, Hospitali hii ya Kwamtipura ambayo ipo Shehia ya Mkele, ina gari la kubebea wagonjwa pale inapotokea dharura ya wagonjwa kuzidiwa na kama haina Wizara yako ina mpango gani wa kuweka gari ya kubebea wagonjwa katika hospitali hii.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mnadhimu wangu swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, Hospitali ya Kwamtipura kama alivyorekebisha Mhe. Mwakilishi ina gari moja, gari lile linatumiwa na wafanyakazi lakini pia ndilo hilo hilo ambalo kuwa linachukua wagonjwa, hakuna *ambulance*. Lakini lipo gari ambalo wanatumia wafanyakazi lakini hilo hilo huwa ikibidi wanachukuliwa wagonjwa wale ambao wanakwenda kufanyiwa *operation* Hospitali ya Mnazi Mmoja kama nilivyoeleza katika jibu langu la msingi. *Operation* za wagonjwa wa macho hapa zinafanyika Hospitali ya Mnazi Mmoja. Sasa gari lile huwa linatumika kuwachukua na kuwarudisha. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Zulfa Mmaka Omar: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mhe. Naibu Waziri tunajua kwamba macho ni kiungo muhimu katika mwili wa binadamu. Swali langu mimi lina (a) na (b).

a) Je, ni lini Wizara yako itafikiria kununua vifaa vya kisasa katika sekta ya macho katika Hospitali ya Chake Chake.

b) Je, ni lini Wizara yako itafikiria kumuaajiri mtaalamu wa kutibu masuala ya macho na uchunguzi mbali mbali katika Hospitali ya Chake Chake ili kuachana na kutegemea wale madaktari ambao wanaokuja kwa vipindi kuja kuchunguza watu macho.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake lenye (a) na (b) kama ifuatavyo.

(a) Mhe. Spika, Hospitali ya Chake Chake inavyo vifaa vya kutolea matibabu, ingawaje ni vifaa ambavyo vimechakaa. Mara nyingi inapotokea *operation* kufanywa basi vinatumika vifaa ambavyo vinakwanda na madaktari pale wataalamu kufanyia operesheni hizo. Wizara imo mbioni kuweka vifaa siyo vya kutengenezea au kushughulikia wagonjwa wa macho tu, lakini vifaa vya fani zote za *department* zote, Wizara iko mbioni kuhakikisha seti mpya za vifaa katika hospitali zote na sio hospitali za Chake Chake peke yake.

(b) Mhe. Spika, kuhusu kuajiri wataalamu wa fani ya macho katika Hospitali ya Chake Chake, Mheshimiwa hili nilikuwa namuomba Mhe. Mwakilishi awahamasishe vijana au wananchi na hususan katika mji wa Chake Chake au Kisiwani Pemba wajitokeze sana kusomea katika fani hii. Kwa sababu Serikali inawasomesha vijana katika fani hii na ushahidi upo, wapo wafanyakazi ambao wamesomeshwa na badala ya kufanya kazi katika hospitali zetu, walipoanza tu kufanya kazi walitoroka na wakenda Tanzania Bara, hadi sasa hawajarudi na Serikali sasa inatumia wafanyakazi waliopo.

Kwa hivyo tunaomba Mheshimiwa uwahamasishe wananchi wazalendo waliopo katika mji wa Chake Chake au na vitongoji vyake kuchukua au kusoma fani hii, baadae waombe na wasaidiwe kuajiriwa katika hospitali ile ili tuhakikishe pana mtu ambaye ni mzalendo na anaweza kuitumikia hospitali ile kwa manufaa ya wananchi wa Chake Chake.

Ahsante Mheshimiwa.

Nam. 3

Taratibu za Kufungwa kwa Barabara

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Aliuliza**:**

Moja kati ya changamoto kubwa inayowakabili wananchi wa Zanzibar wakati wa kutekeleza majukumu yao ni ufungaji wa Barabara za Umma (*Public Road*) kinyume na taratibu na bila ya taarifa yoyote.

(a) Ni sababu zipi zilizopelekea kufungwa kwa Barabara ya Mahakama Kuu (Vuga), hali ambayo inapelekea usumbufu mkubwa kwa watumiaji wa Barabara hiyo kwa shughuli za kila siku.

(b) Je, kufungwa kwa Barabara hiyo kumefuata taratibu za kisheria na kutoa taarifa kwa watumiaji kabla ya hatua hiyo kuchukuliwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu**:**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kuchukua nafasi hii kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 3 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, Sheria nambari 7 ya mwaka 2003 inayohusu barabara yaani *"Road Transport Act"* kupitia kifungu namba 154 kinampa uwezo Waziri mwenye dhamana ya kushughulikia barabara kufunga barabara yoyote ile pale panapoonekana kuwepo haja ya kufanya hivyo. Hivyo ufungaji wa barabara ya Mahakama Kuu Vuga ni kutokana na sababu ya taratibu za udhibiti wa magari na usalama katika eneo hilo ambapo pia lilikuwa ni agizo kutoka Ofisi ya Mhe. Rais Ikulu.

(b) Mhe. Spika, ufungaji wa barabara hiyo umetekelezwa kwa mujibu wa kifungu cha 154 kama nilivyosema mwanzo cha Sheria ya Usafiri wa Barabara na Waendesha Vyombo vya Moto pamoja na wananchi kujulishwa kuhusu suala hilo kabla ya kuchukuliwa hatua hiyo. Aidha, Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji iliwaandikia rasmi Taasisi pamoja na vyombo vya habari kuhusu uamuzi huo. Baadhi ya Taasisi na vyombo hivyo ni Idara ya Habari Maelezo, Gazeti la Zanzibar Leo pamoja na Shirika la Utangazaji Zanzibar. Aidha, *"legal notice"* kuhusuana na ufungaji wa barabara hiyo vile vile ilitolewa. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Mhe. Mwanaidi naona ameridhika. Mhe. Wanu Hafidh Ameir kwa swali la nyongeza.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa ruhusu kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Kwa kuwa barabara zetu za Mji Mkongwe ni chache na mara nyingi kunakuwa kuna foleni ya kuingia katika mji huo.

a) Je, Waziri haoni ipo haja ya kufunga barabara ile kuanzia saa 12:00 jioni kwa sababu, sababu alizosema ni za usalama mpaka saa 12 asubuhi kama wanavyofanya Ikulu Bara.

b) Kwa kuwa amesema kwamba sababu kubwa ni usalama wa ile sehemu yenyewe. Je, Mhe. Waziri haoni kwamba pia kunasababu kuna sababu wa kuifunga barabara inayopita eneo la makaazi ya Mhe. Rais ili kumpatia utulivu na pale.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Wanu Hafidh Ameir kuhusu swali lake lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

a) Kama tulivyosema mwanzo tunapotoa *Legal Notice* maana yake tayari ni utaratibu mzima ambao tumeutumia kufunga ile barabara. Kwa hivyo tunavyoifunga ile barabara katika *legal notice* yetu tumesema kwamba tutaifunga kwa muda wote. Kwa hivyo hiyo ndio *legal notice* ilivyo. Lakini kuhusu suala la msongamano tunajua kwamba kuna msongamano katika maeneo tofauti ya Mji Mkongwe na hapo hivi sasa tuko katika utaratibu hata kuhakikisha kwamba tunatumia utaratibu gani katika kuhakikisha ule msongamano unaondoka.

b) Lakini kuhusu kifunga barabara ambayo anayosema ambayo ile kule ni barabara kuu kwa hiyo itakuwa tabu kuifunga ile hasa kwa sababu inatumika na watu wengi na ni njia kuu.

Ahsante Mhe. Spika

Mhe. Spika: Ahsante Waheshimiwa Wajumbe naona maswali yamemalizika ijapokuwa kwamba muda bado upo. Nashukuru sana sasa nimwite Katibu kwa shughuli inayofuata.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Mwaka 2017/2018 - Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Spika: Ahsante Waheshimiwa kwenye orodha yangu hapa nina mchangiaji wa mwanzo leo hii Mhe. Ali Salum Haji (Mnadhimu).

Mhe. Ali Salum Haji: Ahsante Mhe. Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi ya mwanzo siku ya leo kuweza kuchangia.

Mhe. Spika, mimi michango yangu sio mingi sana na zaidi nimeelekeza katika sekta kubwa sana sekta ya michezo na tasnia ya habari.

Mhe. Spika: Samahani kidogo Mhe. Ali Salum Haji naomba nimpishe Mhe. Naibu Spika, karibu

(Hapa Mhe. Naibu Spika alikalia kiti)

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Ali Salum endelea

Mhe. Ali Salum Haji: Nakushukuru Mhe. Naibu Spika, mimi nasema michango yangu ni midogo na zaidi nitazungumzia katika tasnia kubwa ya michezo na habari.

Mhe. Naibu Spika, nianze kwa kumshukuru Mhe. Waziri kwa jitihada kubwa anayoifanya tangu achukuwe majukumu ya Wizara hii na tumeanza kuona mabadiliko makubwa katika Wizara yake na Wazanzibari wote wameanza kufarajika kutokana na jitihada anazozifanya, lakini kwa ujumla pia niwapongeze wote kwa jumla Mhe. Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote, Wakurugenzi kwa jitihada ambazo wamezionesha.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, mimi kwanza kabisa nataka Mhe. Waziri anisaidie maelezo katika kitabu chake amezungumzia juu ya suala zima la ujenzi wa viwanja vya mpira vya Mawilaya. Na kwa bahati juzi Mhe. Jaku Hashim Ayoub alipokuwa akichangia hapa alisifu Kiwanja cha Kitogani. Mimi nataka kujua hiki Kiwanja cha Kitogani ndio kimo katika ile programu ya viwanja wa Mawilaya. Kama kimo *is Okay*, lakini kama hakimo basi niwaombe wafanye jitihada lakini nataka kujua na haya maeneo mengine, maana yake hizi Wilaya nyengine hatua ambazo Wizara imefikia tayari wameshapima viwanja na tayari wana hati ya viwanja hivyo na kama hawana lini viwanja hivyo vinapimwa na vianze kufanyiwa kazi ya ujenzi.

Lakini Mhe. Naibu Spika, kipindi kimekuwa kirefu na maneno yamekuwa mengi katika suala zima la ujenzi wa viwanja vya Mawilaya na vimepelekea viwanja uwanja wetu wa mpira kupata kazi kubwa ya kutumiwa na mashindano mbali mbali ambayo mashindano ya mpira. Juzi tumeanza kushuhudia kuna mashindano mapya yameanza kushindaniwa katika ule mpaka mashindano ya nage yanashindaniwa yanashindaniwa Amani, gwaride na mambo mengine, yote haya inatokana na ufinyu wa viwanja katika nchi yetu.

Kuna taarifa kwamba kuna Kampuni kutoka kutoka Afrika ya Kusini wameonesha dhamira nia ya kutaka kuisaidia Serikali ya kujenga viwanja hivi vya Mawilaya, na wapo tayari kujenga pasipo na Serikali kutia hata senti yake moja. Mhe. Naibu Spika, nataka kujua tu kwamba hili suala lipo katika Wizara yake na kama lipo Mhe. Waziri ametoa ushirikiano gani kwa hii kampuni ya Afrika Kusini ambayo imekuwa na muda sasa hivi kufuatilia kutaka kuwekeza kuisaidia Serikali kujenga viwanja hivi ili kuondosha matatizo ya viwanja katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea nataka Mhe. Waziri aje kunisaidia maelezo kidogo. Kwa kipindi kirefu Mhe. Naibu Spika, kumekuwa na matatizo na migongano ya ndani kwa ndani katika taasisi zake anazoziongoza. Mhe. Naibu Spika, kumekuwa kuna tatizo katika Baraza la Michezo la Taifa Zanzibar. Taasisi hii ndiyo taasisi ambayo tunaitegemea isimamie masuala la michezo katika nchi yetu, lakini wanafikia pahala wanafanya kazi ambazo haziwastahiki. Kwa sababu wao kama chombo cha kusimamia lakini wanafikia wakati, wanataka kufanya kazi za kiutendaji na wamekuwa wanapotaka kufanya kazi za utendaji, kunaingia migongano na migogoro baina yao na baina ya vyombo vinavyohusika.

Mhe. Naibu Spika, jambo hili sitaki kuliingia ndani sana kwa sababu ni jambo kubwa, lina mambo mengi ambalo ushahidi wa kutosha ulijitokeza hata kutokutoa ushirikiano wakati Mhe. Waziri alipopata uwanachama wa *CAF* wakati anarejea, na yametamkwa matamko mbali mbali, kufika pahala hata Baraza likasema halifahamu, halielewi na kutokutoa ushirikano wa mapokezi katika tukio muhimu na la kihistoria katika nchi yetu.

Lakini ukiachilia hilo Mhe. Naibu Spika, kumekuwa kuna migongamo mikubwa katika Baraza la Michezo na *FA* hapa nchini. Mhe. Naibu Spika, matatizo haya sio katika masuala ya Chama cha Mpira tu, lakini katika vyama vyote baada ya kwenda mbele, sasa hivi tumekuwa tunarudi nyuma, kutokana na kutokuwa na ushirikiano wa pamoja baina ya Baraza la Michezo na vyombo vyetu hivi. Mhe. Naibu Spika, tulikuwa tukishuhudia mambo mengio nchini hapa ambayo yalikuwa yakifanyika kila mara.

Mhe. Naibu Spika, mbio za *Marathon* tumekuwa tumeshazowea kila kipindi, tulikuwa tumezoea masuala ya mbio za baiskeli, yaani michezo yote baada ya kwenda mbele sisi tunarudi nyuma kutokana na kutokuwa na ushirikiano baina ya chombo hiki na chombo chengine. Mimi nataka kujua Mhe. Waziri atakapokuja hebu anieleze, kuna tatizo gani hasa BTMZ na kuna watu wanazungumzwa *direct* ambao wanavuruga taasisi zetu hizi. Mhe. Naibu

Spika, Mhe. Waziri Serikali inatumia pesa nyingi, Serikali inawekeza sana katika masuala haya. Nataka kujua tatizo la BTMZ kwa kufanya kazi za kiutendaji baada ya kazi za kusimamia kama kazi za Kiserikali katika maeneo yao.

Mhe. Naibu Spika, nataka niende katika eneo jengine hilo hilo la sekta la mchezo, nataka nizungumzie Uwanja wa Amani. Mhe. Naibu Spika, nilimuomba hapa Mhe. Waziri hapa aje anipe masuala ya hatua zilizofikia na watu ambao walifika Ofisini kwake kutaka kuwekeza katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, Uwanja wa Amaan unapoteza haiba. Tuna uwanja mzuri lakini uwanja ule tusipofanya maamuzi ya haraka ya kujenga viwanja wa Mawilaya vya haraka, uwanja ule Mheshimiwa tutaupoteza. *Pitch* ya Amaan sasa hivi imekufa, hatujua Serikali ina mpango gani na jitihada gani ya kuurejesha, wachezaji wamekuwa wanateleza ovyo. Jana mechi zimeshindwa kufanyika kwa sababu *drainage* hazifanyi kazi. Sasa hili ni tatizo, tumefanya ukarabati juzi, hatuna hata muda. Tunafikia pahali uwanja unakuwa haufai lakini uwanja huo huo Mhe. Naibu Spika, umekuwa sasa hivi unaonesha matatizo. Mara nyingi taa za Uwanja wa Amaan mara kwa mara zinakuwa zikizima. Nimeshuhudia mwenyewe mechi karibuni tatu zinafika pahala dakika kumi kumi na tano taa zinazima, watu wanatulia mpaka mataa sijui yavute kasi, imekuwa kama tunataka kukimbia *marathon.*

Sasa hili ni tatizo. Mechi tunasubiri lakini kwa sababu uwanja huu tunautumia katika shughuli kubwa za Kiserikali namuomba Mhe. Waziri atafute jitihada za kutosha kurekebisha suala lile, tunaweza tukaja tukatoa mtafaruku, tukaja kuhatarisha usalama kwa sababu Uwanja wa Amaan unakwenda viongozi wengi, ni hatari kwa usalama wa viongozi kuja kuzima mataa uwanja ule ukaja kuwa kiza, ikawa mtu hajui pa kupitia wapi na wapi pakukimbilia.

Lakini hilo Mhe. Naibu Spika, lisitoshe. Nimshukuru kama nilivyomshukuru mwanzo Mhe. Waziri ametuletea uwanachama wa *CAF* ambao wengine hapa waliopita walidiriki kusema maneno mengi tu ambayo yalitukatisha tamaa Serikali hii, walituambia kwamba uwanachama huu hautoweza kuja mpaka Serikali hii tuondoke katika Muungano, wengine walisema mpaka tupate Serikali tatu lakini hayo hayakufanyika na uwanachama tumeupata na sasa hivi tuna matumaini baada ya muda mfupi Mheshimiwa atatuletea uwanachama wa *FIFA* katika nchi yetu.(*Makofi*).

Mhe Naibu Spika, hivi vyama vya soka vina taratibu zake na sheria zake. Moja katika taratibu ambazo sasa hizi zinatumika ni masuala ya magoli ambayo

yamekubalika na *FIFA* ni magoli ambayo nyuma hakuna vyuma, yaani hakuna posi ndogo za ndani ambazo zilikuwa zikipelekea utata wa kutokujua wakati mwengine mpira unaweza kupiga posi ya ndani ukatoka bila refa kuelewa, tukiachilia mambo mengine ya teknolojia ambayo hata mimi yamenitia unyonge kutokana na timu yangu ya Negro kutopanda daraja, mpira ulidunda ndani umevuka chaki kwa sababu teknolojia hakuna, nikaambiwa mpira haukuingia. Matokeo yake mechi ilikuwa droo na timu yangu haikupanda.

Mhe. Naibu Spika, nawashukuru waliopanda Africa Coast na Villa United, lakini mambo haya yanayotupelekea utata wa kutopata haki zetu, haki zetu za vilabu tunakosa kutokana na matatizo ambayo mpaka sasa hivi yanaendelea. Mhe. Naibu Spika, masuala ya magoli sheria imebadilishwa tangu mwaka 1999 duniani, sisi bado tulikuwa tunaendea, inawezekana tulikuwa tunaendelea kwa sababu hatujapata uwanachama wa *CAF*, tumepata uwanachama badilisheni magoli.

Mhe. Naibu Spika, magoli ya sasa posi zake nje zinakuwa *angle* ziko nje, hakuna ndani, ndani inabakia nyavu tupu, mpira ukiingia maana yake hautoki na kuondosha migogoro. Mhe. Naibu Spika, nakuomba Mhe. Waziri fanya marekebisho haraka ili tuendane na hilo ambalo tumelipata karibuni.

Mhe. Naibu Spika, nataka nizungumzie kituo cha michezo cha *Dole Olympia Africa*. Mhe. Naibu Spika, niliona kupitia *ZBC* Mkurugenzi wa Kituo hiki akilalamika juu ya viwanja vya eneo lile vya kituo vile kutokufanyiwa ukarabati mzuri na kupoteza haiba na malengo ya Serikali. Mhe. Waziri atakapokuja anijibu. Nini mipango ya Serikali katika kukiendeleza kituo kile ili malengo na dhamira ya Serikali iweze kufikiwa.

Mhe. Naibu Spika, nataka nizungumzie *ZBCTV*. Mhe. Naibu Spika, nimpongeza Mkurugenzi, mabadiliko yamefanyika, mambo mengi tunayaona *Alhamdulillah* kasoro za kibinadamu haziachi kutokezea na zinapotokeza mara nyingi, wenzangu wanasema hawaombi radhi, mimi sijapata kuona katika kipindi hiki sijapata kuona matatizo makubwa ambayo yanajitokeza katika *ZBC-TV*.

Lakini Mhe. Naibu Spika, nataka nimwambie Mhe. Waziri kwamba moja katika maeneo makubwa ambayo dunia sasa hivi wamewekeza ni sekta ya michezo na katika kila eneo watu wanatoa kipaumbele katika masuala mazima ya michezo. Wenzetu Tanzania Bara wana vipindi vingi ambavyo wanarusha matangazo ya michezo mara kwa mara. Sasa kwa upande wetu tulianzisha kipindi *ZBC TV* ambacho kilikuwa kinarushwa kila siku ya Jumamosi.

Lakini Mhe. Naibu Spika, cha kusikitisha kipindi hiki kilikiwa kinarushwa kwa muda wa saa moja lakini mimi nilifikiri baada ya kuongezwa masaa kutoka na upendo wa michezo, kipindi hiki kimepunguziwa muda wa nusu saa. Namtaka Mhe. Waziri atakapokuja aniambie sababu, lakini kipindi hiki nacho kimekuwa *recorded*, hakiko *live*. Jambo linapokuwa *live* lina haiba yake Mhe. Waziri lazima tukubaliane.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, juzi nilikuwa namuangalia sana Mhe. Waziri kwa sababu hali yangu kiafya haikuwa nzuri, sikuweza kufika katika harambee ile, lakini jimbo langu nimeweza kuwakilisha timu yangu ya Negro imeweze kutoa mchango mkubwa tu. Sasa kwenda *live* kwa *funds raising* ile kumepelekea kuongeza makusanyo kutokana na wananchi wengi kupiga simu, kupeleka mameseji katika kuchangia, hata UWAWAZA nilisikia *message* yao Mhe. Naibu Spika, ya kuchangia. Sasa jambo la *live* lina raha yake, jambo la *live* linaleta nguvu na uimara wa kuboresha kitu. Niwaombe kipindi hiki kirejeshewe muda wake lakini pia kiwe kinarushwa *live* baada ya kuwa *recorded*.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, nataka Mhe. Waziri aje anisaidie hapa karibuni viongozi wetu wa sekta ya michezo, nilisikia kwamba wamefungiwa maisha. Mimi nikataka kujiuliza tatizo nini. Hivi sheria zetu za michezo kuna kifungo cha maisha na kama kipo Mhe. Waziri naomba Kanuni, ukashirikiane na Vyama vinavyohusika kuzibadilisha.

Mhe. Naibu Spika, suala la kufungiwa maisha ni suala zito sana. Nafikiri katika makosa ya jinai basi labda mtu anayeuwa mara nyingi au anayetumia silaha nzito katika masuala ya ujambazi, ndio anafungwa maisha. Mhe. Naibu Spika, kumfungia maisha mwana michezo, tena mahiri ambaye ameacha kazi zake za tasnia zake, alikuwa ni mwalimu wa sayansi, ametoka amekuwa mkufunzi, na alipokwenda kwenye ukufunzi pia mnamwambia asifanye kazi zake. Mhe. Naibu Spika, huu ni upendeleo. Tuache chuki za binafsi katika kuendeleza masuala ya soka Zanzibar. Mhe. Naibu Spika, tunapoendeleza chuki, tunapoendeleza fitna, tunapoendeleza husda, vyama vyetu havikuwi. Kama kuna matatizo basi watu wakae kwenye meza wayaamua na wayatafutie ufumbuzi, kama kuna mtu ana kosa basi ahukumiwe kwa mujibu wa taratibu.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, hivi karibuni nilimsikia Maalim wangu anafungiwa maisha, tatizo nini? Maalim Masoud Atai amefungiwa maisha kutokujishirikisha na masuala ya michezo. Mhe. Waziri nataka uniambie tatizo ni nini na nataka tatizo hili kama lipo litafutie ufumbuzi yeye na ndugu Hussein Ali Ahmada.

Mhe. Naibu Spika, kama tunaanza utaratibu huu mimi sifikirii kama tutafika huko tunakoelekea, tunajua kila mtu ana kosa, hata hawa waliowafungia na wao wana makosa yao tunayajua tele tu. Kama tutaaamua kufungiana maisha hapa mpira hauchezwi Mhe. Waziri hata siku moja, watu wanakula rushwa, marefa wanakula rushwa, viongozi na wao ni mashaka. Tumekusudia juzi tu Mhe. Naibu Spika, tuna mashindano ya daraja la pili ngazi ya taifa timu sita bora, timu tatu haziji uwanjani kwa mipango tu ya rushwa ili timu zao nyengine zifaidike na hakuna hatua yoyote ambayo inachukuliwa, inakuwaje watu hawa wawili wafungiwe maisha.

Mhe. Waziri nasubiri majibu ya kutosha…

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa una dakika moja imebaki.

Mhe. Ali Salum Haji: Ahsante Mhe. Naibu Spika, dakika moja nitamalizia hiyo hiyo.

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana, Mhe. Waziri atapokuja aniambie tulikuwa tuna nyumba za *ZBC Radio* hizi ambazo ziko katika maeneo tofauti kama Chukwani, Kwamchina na Kikwajuni. Nyumba hizi zinasemekana kwamba zimeanza kutumika katika utaratibu usio stahiki, kwa sababu nyumba hizi lengo na madhumuni yake ilikuwa ni kuja kuwaweka wageni ambao wanaokuja kutusaidia katika masuala ya taaluma katika kitengo chetu hiki. Sasa nyumba hizi inasemakana haziko katika hali nzuri.

Mhe. Naibu Spika, jambo jengine la kumalizia sekunde 30 zako na la mwisho kabisa niwashukuru sana watu wa *ZBC,* lakini nawaomba sana vipindi vyetu vya *ZBC Radio* ama *TV* mara nyingi vimekuwa vikitoa habari za mjini baada ya vijijini na hii ni kutokana na mapungufu yaliyokuwepo. Mapungufu ya usafiri na mapungufu ya vifaa. Nimuombe Mhe. Waziri ajitahidi kuboresha haya maeneo ili baadae yaweze kufanya kazi kwa umakini kabisa.

Mhe. Naibu Spika, sina dhamira ya kuzuia fungu lolote. Mhe. Waziri kama nilivyosema mwanzo umejitahidi sana na tunampongeza, lakini namuomba atakapokuja yale maeneo ambayo nimetaka maelezo na nimetaja anijibu basi aje anijibu kwa kina na kwa ufasaha.

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kwahani naunga mkono hoja. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mhe. Ali Salum. Mchangiaji wetu anayefuata ni Mhe. Ahmada Yahya na baadae mchangiaji wetu wa mwisho kwa upande wa *backbencher* atakuwa ni Mhe. Miraji Khamis Mussa.

Mhe. Ahmada Yahya Abdul-Wakil: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii kwa mara ya mwanzo.

Kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu muumba mbingu na ardhi aliyetuwezesha kufika hapa tukiwa katika hali ya amani na utulivu mkubwa. Hapo hapo napenda kumshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuniteua kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi kwenye chombo hiki. Naahidi kwamba nitatoa ushirikiano mkubwa kwa chombo hiki kwa ajili ya ustawi wa nchi yetu. Nakwenda katika hoja. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa napenda kumshukuru sana Mhe. Waziri kwa juhudi zake kubwa alizochukua katika kuiongoza wizara hii. Nilikuwa nakipitia kitabu chake cha bajeti asubuhi hii, kwa kweli kimeandaliwa kisayansi sana tena, kwa vile najua ana wataalamu mahiri sana kwenye fani ya uandishi na takwimu. Shukurani hizi na pongezi zaidi zinajikita katika ukurasa wa 33 "Zanzibar kuipatia uwanachama wa Shirikisho la Mpira la Afrika (*CAF*)".

Mhe. Naibu Spika, kama mwezi mmoja na nusu asubuhi *ZBC* ilikuwa inamuhoji kuhusu masuala ya upatikanaji wa uwanachama. Kwa kweli wanachama 31walikataa pale kwamba Zanzibar isipewe uwanachama. Juhudi aliyoifanya Mhe. Waziri ya kutulia na kujenga hoja na mifano mbali mbali duniani aliyoitoa ambao wamepata uwanachama hadi *FIFA*, basi wajumbe wale wote aliwabadilisha mawazo na wakakubali kwamba Zanzibar iweze kupatiwa uwanachama *CAF*. Mhe. Waziri hongera sana. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, hii moja kwa moja inaipelekea kwamba sasa umefika wakati wizara hii ijipange kisawa sawa kwa kushirikiana na wataalamu wake na wengine na wafahamu ni wana michezo mahiri, kusudi tuelekee katika kupata uwanachama wa *FIFA*. Haya yote yatakuja tu masuala ya viwanja, usaidizi wa mipira, usaidizi mwengineo baada ya kupata uwanachama wa shirikisho hili la *CAF* na naamini muda si mrefu juhudi atafanya ili tuingie uanachama wa *FIFA*.

Mhe. Naibu Spika, lakini tuna haki kuipongeza Serikali hii ya Awamu ya Saba inayoongozwa na Dkt. Ali Mohamed Shein ya kusimamia kikamilifu na kuipa hadhi leo kuwa inatambulikana kimataifa kuhusu habari ya michezo. Leo hii timu yetu ya taifa itakapokwenda nchi yoyote Mhe. Naibu Spika, tuna fursa ya

kupigwa wimbo wetu wa taifa wa Zanzibar. Hili ni jambo kubwa sana katika nchi yetu. Tukenda Nigeria, Niger, Somalia, Sudan, Congo na nchi zote, tunayo haki hata kuhoji wimbo wetu wa taifa na bendera yetu iko mbele. Kwa haya machache Mhe. Naibu Spika, nakupongeza mimi naunga mkono hotuba yake kwa asilimia mia moja.

Ahsante Mhe. Naibu Spika. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Ahmada ni mwanzo mzuri sana, tunakutarajia utakuwa mchangiaji mzuri sana. Tunaendelea mchangiaji wetu wa mwisho kabisa kwa upande wa *backbencher* atakuwa Mhe. Miraji Khamis Mussa na Mhe. Said Soud Said ajitayarishe.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi asubuhi hii ya kuchangia hotuba ya bajeti ya Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo ya kaka yangu Mhe. Rashid Ali Juma.

Mhe. Naibu Spika, kwanza naanze kwa kumpongeza Mhe. Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wa wizara na taasisi za wizara hii kwa ubora wao waliotekeleza katika kuleta kitabu hiki, mambo mengi yamejitosheleza na mimi nitataka kidogo kuchangia katika maeneo mafupi sana.

Baada ya pongezi hizo naomba niende kwenye fungu Nam. 15 ambalo linaelezea pesa za mradi wa ujenzi wa Uwanja wa Mao-tse-Tung. Kuna fedha za serikali, katika bajeti ya 2016/2017 walitenga milioni 400, lakini serikali ilichochangia ni milioni 315,750,000. Lakini mara hii pia tumetakiwa tuidhinishe bajeti ya milioni 500 kupitia mchango wa serikali. Sasa kwa ujumla nilikuwa nataka kujua kwa sababu inawezekana programu hii ikawa endelevu, kile kiwango cha mchango wa fedha za SMZ kwa ujumla wake ili tuone mwaka huu tumefanikiwa kupeleka hiki, mwaka huu tumetenga lakini tumepeleka hiki lakini mwisho tutajua tu kwa sababu tutafuatilia ule msururu wa pesa tunazowatilia lakini na bajeti wanayotuletea. Sasa hapa nataka kujua kiasi gani cha fedha ambacho serikali imetakiwa kuchangia hapa.

Mhe. Naibu Spika, eneo hilo hilo katika kitabu hiki Mhe. Waziri ametuandikia kuwa hana maelezo ya fedha zilizopatikana katika mchango ule unaotoka katika Serikali ya Jamhuri ya China. Mimi nikawa napata mashaka sana kwa sababu tunakwenda kwa mikataba na wajenzi, lakini tunakwenda na makubaliano na mtu ambaye anataka kutupa fedha, fedha itaingia katika Serikali Kuu, lakini baadae itahamishwa kwenda aidha wizara au kwa mtu ambaye kashinda tenda ya ujenzi ule.

Mhe. Naibu Spika, sasa *transactions* zote hizi mbili toka kuingia kwa fedha lakini na kuzipeleka kwa mkandarasi moja kwa moja, leo tunaambiwa wizara haina takwimu ya fedha zilizopatikana katika mchango huu wa wenzetu wa serikali. Maana bajeti iliyopita wametuletea fungu la bilioni 5,597,000,000 lakini na bajeti hii wamelirejesha vile vile. Kwa maana ni sawa sawa na tumeanza ujenzi lakini tuko kwenye ziro la kupata msaada kwa wale wenzetu. Lakini kama tumepata kwa nini kisipungue? (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, nilikuwa napata mashaka sana kabla ya kuanza ujenzi tuna washauri elekezi ambaye kila *package* ya ule mradi anatuletea hii lipa, hii subiri. Sasa Mhe. Waziri atakapokuja anipe sababu za kutosha kwenye fungu hili la mradi huu vyenginevyo programu nitakuwa nazuia fungu mpaka zile sababu ziniridhishe. Kwa hivyo hapa kabisa naweka shilingi. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, niende katika programu ndogo Nam.3 ya utangazaji na uhamasishaji wa utalii. Tulitenga pia kwenye bajeti 2016/2017 makadirio yalikuwa ni milioni 208,505,000 lakini zilizopatikana ni milioni 196,130,000. Kiukweli Mhe. Waziri kama tunataka tu-*invest* kweli katika utalii, hatuwezi kuwa na pesa hii kwenda kuutangaza utalii. Utalii katika sura ya kawaida na mfumo tunaokwenda nao ni *win to win situation*, hatuwezi ku-*invest* milioni 196 katika kwenda kuutangaza utalii, ikesha leo tukategemea kupata watalii. Kama tunategemea kuendelea kupata vishuka ambao havina tija kubwa katika *investment* ya hapa, tuendelee maana yake kila siku tutenge pesa hizi hapa. Lakini ukitizama katika ile programu ya kuratibu ule utalii wenyewe zilitengwa milioni 900 na zaidi, lakini zimepatikana milioni 682. Ukichanganya kwa zote kuratibu, kuutangaza haujafika hata bilioni 1.

Mhe. Naibu Spika, Kamisheni hii ya Utalii tuko *serious* kweli katika kuiwezesha kufika katika malengo tunayoyata Mhe. Waziri, hii ni pesa ndogo sana. Ukiangalia katika nchi zile zinazoongoza hizi kwa watalii kwenye Bara la Afrika tu, wewe nenda Mauritius wanatumia bilioni 2 ya bajeti yao kwenye utalii, wana-*invest* hapo lakini karibu bilioni 10 wanatengeneza. Leo tunarudi hapa sisi tunakwenda hata bilioni 1 ukizichanganya pesa ambazo tunataka kuwekeza kwenye utalii hazifikia.

Mhe. Naibu Spika, sasa Mhe. Waziri mimi nilitaka kujua hii mikakati ya hii taasisi katika kuiendeleza ili tuweze kutengeneza pesa kwa ukweli umejipangaje, maana hii pesa ndogo. Mimi nilikuwa namuangalia Mwenyekiti wa Bajeti pale, kama kuna fungu jengine ambalo linahamishika basi tulikuwa tuwaongezee hawa Kamisheni ya Utalii tutoe pesa tutengeneze pesa, hii pesa ndogo Mhe. Waziri.

Mhe. Naibu Spika, naomba twende kwenye eneo hilo hilo katika mikakati na uundaji wa sheria ya utalii kuna Kanuni pia. Kuna muda mimi nilikuwa nafuatilia sana kwenye eneo hili tulianzisha utalii kwa wote (*tourism for all*), kuna kamati tukaziratibu Kimikoa, tukaziratibu Kiwilaya na Kishehia. Lakini katika kitabu hiki kizima huoni maeneo ambayo ya kutenga bajeti ya kuwezesha kamati hizi. Mhe. Naibu Spika, hebu Mhe. Waziri ukija katika ile dhana nzuri ambayo sisi sote tuliifurahia, mkakati gani katika eneo hili kwa kuwezesha programu hii ndogo ambayo sisi wenyewe kwa hiari yetu tuliona tuiweke.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, lakini nirudi Mhe. Waziri ili utalii huu twende vizuri umetoa maelezo mengi, lakini kile kitengo cha *marketing* ambacho ndio kitafanya kazi nzuri, hebu ukija twambie ili hili Baraza lipate sura, una waataalmu wangapi katika kitengo cha *market*, na wangapi wamepata mafunzo ya utalii ambao tukisema tunawatengea pesa kwenda kutangaza watangaze kweli. Sasa utakapokuja hapa nambie.

Mhe. Naibu Spika, lakini utalii katika visiwa vyetu hivi viwili kuna Unguja na Pemba, ile namba nataka ya Pemba nzima wafanyakazi wanaofanya kazi katika sekta hii ya utalii. Mimi kuna muda nilikuwa nafuatilia takwimu ulikuwa una wafanyakazi siku tisa tu hii, lakini hebu twende ishapita miaka ya fedha miwili tokea takwimu hizi. Sasa hivi hebu tuone una wafanyakazi wangapi kwenye eneo hili, kweli tujue kuna taswira nzuri ya kukuza utalii katika maeneo yote ambayo utalii unaruhusu ndani ya visiwa hivi viwili.

Mhe. Naibu Spika, naomba niende hapo hapo katika utalii kwenye *tour operators.* Sheria yetu tunakwenda katika *local tour operator.* Lakini Mhe. Waziri kwenye eneo hili ziko *tours* wenzetu wanafanya *sabotage*, wanajaribu kumuweka mtu lakini shughuli zote za uendeshaji, zote zile zinazoendeshwa na *tours* hizi zinaendeshwa na wageni. Kwa hivyo ule mchango kupitia *tours* hizi, kwa maana ukienda *ZRB* utakuta kuna asilimia ndogo sana ya mchango wa *tours* zile. Kwa sababu wote wale wanafukuzia katika *tours* ambazo zinaongozwa na hawa wageni.

Mhe. Naibu Spika, mimi Mhe. Waziri kwenye eneo hili nakupa mbili tu leo, nenda kaichunguze kwa makini *flash tour*, ukisha jibu njoo uninong'oneze tu, kwenye eneo hili mimi sitaki kuzuia fungu lakini kaichunguze kwa makini *flash tour* na *expanded tou*r. Hizi wale waendeshaji wa *tours* hizi ni akina nani? Ikisha leo tunataka kuziboresha *tours* hizi ili tupate ile *standard tourism*, utazipata wapi watu wamekuja kutengeneza pesa na kuondoka nazo. Mhe.

Waziri eneo hili nakupa kazi lakini nibaki katika Kamisheni ya Utalii hiyo hiyo. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, nataka nimwambie Mhe. Waziri kama anakumbuka na ukifuatilia kabla ya kuwepo wewe hapo kuna *promotion* nyingi zilifanyika na kuna maeneo tulifunga mikataba. Mimi nilitaka uje uniambie mpaka bajeti hii inakuja ule mkataba wa India hauja-*expire* na kama ume-*expire* mpaka bajeti yake unaileta hapa, utaratibu gani ambao umekuja kutuletea sisi tupitishe kitu ambacho hata ile mikataba ya uendeshaji wa vituo hivi haupo. Kwa hivyo ukija Mhe. Waziri eneo hili wewe unitamkie tu ime-*expire* kweli, lakini tumeleta bajeti yao, lakini kwa nini kitu kime-*expire* umekileta humu ndani, unipe maelezo tu ya ujumla, mimi sina tatizo sana. Mhe. Nabu Spika, isipokuwa kule mwanzo nitazuia fungu, hapa nikipata maelezo ya kina mimi sitakuwa na tatizo na wewe.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri lakini nikupongeze kwanza kwa uzinduzi wa Bodi ambayo kuna siku niliichangia hapa ambayo ni Bodi ya Kamisheni ya Utalii, imezinduliwa, nikupongeze sana. Lakini bajeti yao mara nyingi inapokuja hapa Barazani hawa wanatakiwa waipitie, toka siku uliyozinduliwa Bodi hii na bajeti ametuletea hapa hawajaiona. Hii Bodi ya Makamishna hawa ndio Bodi ambayo inasaidia uratibu na kuelewa bajeti ya taasisi husika, lakini tunasimama hapa leo tunapitisha bajeti ya utalii, wale makamishna hawaijui. Hivi kweli Mhe. Waziri tuna ushirikishwaji mzuri wa Bodi hii ambayo ni taasisi tunayoitegemea iendeleze ule utalii wenyewe, bajeti waione.

Mhe. Naibu Spika, leo mimi nimepitia bajeti hii kwa kina, sijaona hata eneo moja la kwenda kuwa-*train* hata wale Wajumbe wa Bodi. Wajumbe wengine wametokea kwenye *ZATO,* sijui wapi unajua huyu akienda kule ndio katokea kwenye utalii, lakini Wajumbe wengine wametoka mitaani, hakuna programu hata moja ya kuwa-*train* hawa au ya kuwatoa kwenda ku-*study* katika nchi nyengine.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri leo katuletea bajeti ambayo wale wahusika wakuu hawana hata sehemu ya mafunzo ambayo watayapata. Mimi eneo hili Mhe. Waziri naomba uje uniahidi na unieleze vya kutosha. Hapa pia ninazuwia fungu.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, naomba niende katika eneo la programu ndogo ya usambazaji wa maudhui. Mhe. Waziri siku nikichangia maelezo ya Kamati nilisema, hapa serikali iliweka pesa kama ni *capital investment,* nikataka kujua ni kiasi gani cha fedha toka eneo hili la *ZMUX* limeingiziwa. Lakini mpaka

sasa hivi ule uwekezaji wenyewe ambao ilikuwa ni dhamira kubwa ya serikali, kiasi gani serikali imerejeshewa. Lakini nikauliza la pili Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri sikupata majibu. Lakini leo na hapa nazuwia fungu, uniambie. Kwa sababu kitengo hiki cha usambazaji wa maudhui kinatakiwa kibakie *ZBC*, lakini kinaongozwa na wizara, mumeondoa wafanyakazi, wameondoa wataalamu wamewaleta huku Wizarani. Kwa nini wasibaki pale, kuna tatizo gani la kubaki kule na kuendesha hizi shughuli zao wenyewe. Leo wizara huku sisi tutakuwa tunaona humu ndani kama mna-*interest* fulani, lakini kama hamna. Kwa nini hiki kitengo kisibaki kule kikaendeshwa, kuna Mkurugenzi kachaguliwa na Rais kama walivyofika pahala mukateuliwa nyinyi, hamuaminiani au labda kama munaaminiana kuna tatizo gani. Mhe. Waziri ukija humu unambie, hapa nazuwia shilingi.

Mhe. Naibu Spika, huko kote nimeweka shilingi hapa ninapochangia sasa hivi sitoi shilingi ila naomba niseme Mhe. Waziri nipongeze sana jitihada za *ZBC TV* na Redio. Jitihada nzuri lakini niseme tu kuna eneo la redio lile halijanikalia sawa. Vipindi vyake wanavyoviratibu wakati mwengine unaona shida hata kusikiliza, ukiacha ile taarifa ya habari labda usikilize kuna baadhi ya watu wameteuliwa, matangazo ya vifo lakini ukiacha hapo tena wanatutilia muziki hiyo kila siku programu hizo hazi-*change*. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, eneo hili Mhe. Waziri lazima watu wetu wabadilike, watuletee vipindi ambavyo hii redio itakuwa ina mvuto wa kuisikiliza. Huku kwenye televisheni haijambo sana lakini huku hakuna mabadiliko, yaani ukifuatilia vipindi hivyo unaweza kukuta wiki nzima wanakwenda na *trend* hiyo hiyo, yaani unafika pahala unasema kuna tatizo gani. Sasa kama hana wataalamu kwenye eneo hilo, somesha watu Mhe. Waziri tuone mabadiliko ya redio yetu.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, mimi nimefuatilia kuna taasisi fulani walifanya utafiti wa redio zilizosikilizwa nyingi, *ZBC Radio* ikawa ya mwisho. Aah! nikasema mtihani lakini Mhe. Waziri nimuombe kwenye maeneo haya basi tuwaendeleze watu wetu, tuwafunze ili tuone tunasogeza mbele jitihada za maeneo haya.

Mhe. Naibu Spika, mimi leo sina mengi nilikuwa nasema maeneo hayo ambayo nimechangia naunga mkono hoja hii kwa asilimia 50 na 50 zote za maeneo yale niliyoyataja nipate ufafanuzi, ili nimuache Mhe. Waziri akatumie kwa mujibu wa utaratibu ambao ataidhinishiwa na Baraza hili.

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Miraji Khamis Mussa. Mchangiaji wetu wa mwisho anayefuata ni Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiye na Wizara Maalum) karibu.

Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiye na Wizara Maalum): Mhe. Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia hii nafasi. Lakini awali ya yote kwanza nampongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa jitihada zake za kuirudishia Zanzibar uhalisia wake kwa habari.

Zanzibar ni nchi ya mwanzo duniani katika Afrika Mashariki kuzungumzia mambo ya kutoa habari, magazeti na mambo mengine na watu wengi wamekuja kusoma Zanzibar, kwa sababu ya umahiri wake. Sasa pongezi nyingi nampelekea Mhe. Rais kwa kuliona hili na kuweza kuandaa utaratibu wa kupata kiwanda cha kuchapisha magazeti, jambo ambalo sasa ni changamoto kwetu sisi Wazanzibari, kwamba kiwanda hiki kisitumike tu kwa kutengezea Gazeti la Zanzibar Leo, bali kinaweza kutengeneza vijarida vya wiki, kinaweza kutengeneza magazeti ya Kiingereza, kinaweza kutengeneza magazeti ya Kiarabu hata kama ni wiki mara moja, lakini tunayo haki ya kutengeneza magazeti haya kulingana na Zanzibar ilivyo katika mazingira mazima ya watu kupata habari.

Mhe. Naibu Spika, Zanzibar ilikuwa inatengeneza magazeti ya Kipanga, Kweupe, Dira na mpaka sasa tunakwenda na Gazeti hili la Zanzibar Leo. Kwa ufupi ni kwamba Zanzibar inapiga hatua katika mazingira ya kutafuta habari. Baada ya hapo pia nimpongeze Mhe. Waziri na ndani ya kumpongeza kwake naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja kwa sababu hoja zake zimejipanga na yeye mwenyewe sasa amekuwa jasiri kiasi kikubwa katika kutetea hoja za habari, michezo, utalii katika visiwa vya Unguja na Pemba.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, baada ya hapo nilikuwa nataka nisome kidogo Katiba ya Zanzibar, Sura ya Tatu Kifungu cha 11(2) kinasema:-

"Kila mtu anastahili heshima ya kutambuliwa na kuthaminiwa utu wake".

Katiba hiyo hiyo ya Zanzibar Sura hiyo ya Tatu kifungu cha 12(3) kinasema:

> "Haki za raia, wajibu na maslahi ya kila mtu yatalindwa na kuamuliwa na Mahkama pamoja na vyombo vya nchi na vyenginevyo vilivyowekwa na sheria".

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na Katiba ya Zanzibar Kifungu cha 18(2) kinasema kwamba:

> "Kila raia anayo haki ya kupewa taarifa wakati wote kuhusu matukio mbali mbali nchini na duniani kote ambayo ni muhimu kwa maisha na shughuli za wananchi, na pia juu ya masuala muhimu kwa jamii".

Mhe. Naibu Spika, Katiba ya Zanzibar jinsi ilivyoweza kutoa uhuru wa watu kupata habari. Sasa nilikuwa nataka niseme kwamba habari ziko namna nne. Kuna habari kama habari kama habari. Kuna habari inayoitwa uzushi, kwa lugha nyengine tulikuwa tunatambua inaitwa *drip.* Hili ilichukua muda mrefu katika visiwa vya Unguja na Pemba, hili neno "*drip*". Hii ilikua ni habari ya uzushi iliyokuwa haina mashiko.

Mhe. Naibu Spika, pia nataka niseme kwamba kuna habari inaitwa *rumor*. *Rumor* ni kitu ambacho kinazuka lakini hakina uhakika, hakina mashiko, wapi kimetoka hujui. Na suala la nne ambapo ni kifungu cha nne cha habari Mhe. Naibu Spika, hii habari inaitwa umbeya. Umbeya ni kitu ambacho kinakuja lakini yule mtoaji hajapewa *mandate* ya kutoa hiyo habari. Kwa hivyo ukiipokea unaipokea katika mazingira ambayo unangojea itakapotoka ili wewe sasa uithibitishe. Hiyo inakuwa habari.

Mhe. Naibu Spika, katika hali kama hii hali ambayo Katiba imetoa mamlaka kitaarifa. Katiba imetoa mamlaka kwa kila mtu kupata habari. Sasa mimi nimepata mshangao mkubwa Mhe. Naibu Spika, kwamba leo nchi yetu hii yanaweza kutokea mambo ambayo wananchi wanataka wapate habari, lakini habari zinazimwa. Nikizungumza hivi nazungumza zaidi waandishi wa habari wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wa redio, televisheni na magazeti.

Mhe. Naibu Spika, mwaka 2010 palitokea maafa hapa. Meli ya kwanza MV. Fatih ilizama. Mwaka 2011 yalitokea maafa mengine ya meli ya *MV. Spice Islander* ilizama na watu wamekufa, meli zote hizo zimeuwa watu. Na mwaka 2013 *MV. Skagit* nayo ilizama.

Mhe. Naibu Spika, meli zote hizi zilizama na zikauwa watu wengi sana, Wazanzibari wengi sana na Watanzania wengi sana. Maana nikisema Wazanzibari, nikisema Watanzania ndani ya meli hizi kulikuwa na ndugu zetu wanatoka Shinyaka wanakwenda Pemba kufanya kazi zao za kilimo wakafa, kulikuwa na ndugu zetu wanatoka Dar es Salaam wanakuja Zanzibar kwa ajili ya safari za kwenda Pemba au kubakia Unguja meli ikazama wakafa. Kwa hivyo Watanzania wengi walipoteza roho zao kwa hoja hii.

La kushangaza basi, habari zimekwenda mpaka mwisho zimefifia hazijulikani kesi hizi zimekwenda wapi. Vyombo vya habari viko huru vinapewa mamlaka ya kuandika habari lakini tunashangaa kwa nini habari hizi zimekwisha hivi hivi. La kusikitisha basi, Serikali kama Serikali ilijitahidi kwa nguvu zake zote kupita nyumba kwa nyumba kupeleka rambi rambi na watu wengi walifaidika kwa kupitia rambirambi, lakini hakuna kampuni ya meli hizi zilizopita kulipa fidia. Hakuna mtu alilipwa fidia. Kwa nini hakulipwa fidia kwa sababu zilizamishwa habari hizi kupitia vyombo vya Mahakama.

Mhe. Naibu Spika, sasa mimi ninachotaka kusema ni kwamba waandishi wa habari waisaidie serikali katika hali ya kuisafisha na kuonekana kwamba sasa serikali inafanya kazi zake vizuri. Sheria zinatumikiwa, sheria zinatungwa hapa na zinafanya kazi yake. Mhe. Naibu Spika, lakini hatuwezi kwenda tuna waandishi wanalipwa pesa nyingi, tuna wizara zinatoa huduma lakini matokeo yake habari zinazama moja kwa moja. Kimsingi sasa kutokupatikana habari wananchi wanapata nafasi ya kuilaumu serikali.

Mhe. Naibu Spika, juzi nilisema hapa kwamba mimi jimbo langu liko Ikulu, sasa naona kwamba kuna watu wanacheza na utaratibu mzima wa utawala kwa misingi hiyo sikubaliani nayo na nikawahi kusema kwamba kuna watu wako rumande miaka saba, wengine wakajaribu ku-*publish* hao wa miaka saba nani. Mimi nasema wako rumande miaka saba Unguja na Pemba, sio Bara au wapi, Unguja na Pemba wako.

Sasa hao wengine watakaochambuliwa kwamba wako rumande hawapo Unguja na Pemba. Mimi nazungumzia hawa wa Unguja na Pemba ambao nina uhakika. Kweli kuna sheria ambazo mtu hapewi dhamana. Lakini je, hahukumiwi? Mana hapewi dhamana lakini je, hahukumiwi akajua kwamba mimi nimehukumiwa kifungo cha maisha, mimi nimehukumiwa miaka 40, mimi nimehukumiwa miaka 30, je, hahukumiwi? Sheria na Katiba ya nchi hii kila mtu anastahili kupewa utu wake na aheshimiwe. Kwa hivyo haina maana kumuweka pale ndani kwa muda wote huo bila ya kumpeleka kwenye vyombo vya sheria akapata hukumu, tutakuwa hatuitendei haki hii Katiba, hatuwatendei haki wapiga kura.

Mhe. Naibu Spika, narudi nataka niseme waandishi wa habari sasa umefika wakati wa kufuatilia kesi hizi zimezama vipi. Nasema hivyo kwa sababu. Mimi kama *MBM*, Waziri nisiyekuwa na Wizara Maalum nitahakikisha kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inasimamia hoja hii, kwa maana ya kwamba watu waliokufa wapewe fidia zao na wale ambao walikuwa na kampuni hizi wanapewa onyo au wanapewa hukumu au wanalipa fidia kwa mujibu wa sheria

za Mahakama watakavyoona. Lakini mimi siwezi kunyamaza juu ya hoja hii. Kwa sababu mimi ni Mzanzibari niliye na haki za msingi Kikatiba humu, kwa mujibu wa sheria nina haki zote za kusimamia hoja na maslahi...

Utaratibu

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiye na Wizara Maalum) naomba ukae kwanza. Mhe. Mohamed Said Mohamed.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Naibu Spika, nilikuwa nampa taarifa mzungumzaji. Mzungumzaji ni MBM ambaye amekula kiapo cha Uwaziri na maneno ambayo anayoyazungumza hapa ni ya kwenda kuzungumza kwenye Baraza la Mapinduzi kutetea hoja yake wala sio hapa kwa wananchi, anakiuka maadili yake.

Tungemuomba tu yale ambayo yanahusu MBM aende akazungumze kwenye Baraza la Mapinduzi ili asizungumze hapa nashukuru.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa endelea na hoja yako. Sitaki ujibu kama kujibu najibu mimi wewe endelea.

Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiye na Wizara Maalum): Mhe. Naibu Spika, pamoja na yote nilikuwa nataka niseme tu kwamba mchangiaji aliyepita sasa hivi alikuwa ananitanabahisha, lakini mimi kama mwakilishi na hiki ni chombo cha Uwakilishi, nalazimika kuwakilisha Wazanzibari wote na sijawakilisha jimbo wala sijawakilisha kijiji, nawawakilisha Wazanzibari wote waliokosa haki hapa.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa muda wako unakaribia kumalizika, jenga hoja yako.

Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiye na Wizara Maalum): Mhe. Naibu Spika, naomba nizungumzie kidogo utalii.

Mhe. Naibu Spika, utalii katika nchi hii unakua na wizara hii inalazimika sasa kufanya utaratibu wa kuandaa utalii wa ndani ili wananchi waweze kupewa au kushajihishwa namna ya kutembelea sehemu mbali mbali. Haya yanaweza kufanyika hata kama Mhe. Waziri kupitia wizara yake ataandaa utaratibu wa wizara maalum, kila wizara kuipangia siku yake kwa ajili ya kwenda kutembelea sehemu mbali mbali, kwa maslahi ya kujipatia wizara hii mapato. Wananchi washajihishwe namna ya kutembelea sehemu muhimu za visiwa vya

Unguja na Pemba. Kimsingi ni kwamba mambo hayo hayawezi kufanyika bila ya kuweko vishajihisho, vipeperushi na mambo mengine yatakayoiwezesha hii wizara kupiga hatua.

Mhe. Naibu Spika, suala la utalii linaweza likaimarisha mambo mengi ndani ya nchi yetu na mambo mengi yaliyojificha yakaonekana na uchumi ukakua ndani ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, nikija kwenye hoja ya michezo. Nchi yetu sasa imekuwa na michezo mingi ya kisasa, lakini ile ya zamani mingi imeachwa. Zamani tulikuwa na mchezo wa ngoma ya beni. Beni kitaratibu za Zanzibar mwisho ni saa 12. Mpigaji wa beni *physically* anaonekana ni mtu aliyejitolea kuimarisha ngoma ile na kushajihisha ngoma ile ili watu waweze kuwa na mvuto. Mhe. Naibu Spika, haya yameondoka. Wizara hii naiomba kupitia watendaji washajihishe.

Mhe. Naibu Spika, tulikuwa na ngoma ya kibati. Ngoma hizi zilikuwa ni maarufu sana katika visiwa vyetu hasa kwa maharusi. Inaonekana wazi kwamba sasa ngoma hizi zimekufa, zinapigwa siku za sherehe za serikali, lakini hazipigwi tena katika sherehe za wananchi kufurahisha nafsi zao au kufurahisha matokeo muhimu ya ndani ya nchi.

Vile vile Mhe. Naibu Spika, ngoma hizi sasa hazipigwi tena na watu wazima, wanaopiga ngoma hizi ni watoto wa maskuli, wakiletwa watu wazima basi ni wale wasanii maalum walio ndani ya ajira zao wanakwenda kushereheka pale. Sasa turudishe utamaduni kwa wananchi vijijini kuhusu ngoma hizi, zikiimarishwa Mheshimiwa utalii ambao ndio kivunio kikubwa cha fedha za kigeni. Mimi nadhani utaongezeka mara mbili zaidi. Kwa sababu kama utakwenda hoteli, kama utakenda kijijini wakipigiwa ngoma hizi tunaweza tukapata pesa zitakazosaidia.

Mhe. Naibu Spika, nilikuwa nataka niseme kwamba michezo nayo pia imekuwa ikidharauliwa na sasa naona kidogo wizara imejikaza na inajitutumua juu suala zima la michezo. Lakini mimi wenyewe binafsi Mhe. Naibu Spika, kwa taarifa ya Baraza hili nataka nianzishe mchezo wa ng'ombe kisiwani Pemba na nitagharamia gharama zote na ng'ombe nitanunua mwenyewe. Na ukishaimarisha sawa sawa basi nitamwita Mhe. Waziri wa Habari aje azinduwe ili aone kwamba utamaduni nimeusimamia vile unavyotakiwa.(*Makofi*).

Baada ya hapo Mhe. Naibu Spika, naona umeshaanza kunitiza tizama sana narudia tena kusema naunga mkono hoja kwa asilimia mia chini ya mia. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mhe. Said Soud Said (Asiyekuwa na Wizara Maalum). Sasa namwita Mhe. Salama Aboud.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishat na Mazingira: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako na mimi naomba nichangie Wizara hii ya Habari, Utalii na Michezo.

Kwanza naomba nianze kwa kumshukuru sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Rais wetu mpendwa Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuhakikisha kwamba sekta hizi za michezo, utalii basi zinazidi kuimarika katika nchi yetu.(*Makofi*).

Lakini niendelee pia kumpongeza Mhe. Waziri na watendaji wake wote kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kuhakikisha kwamba nchi yetu hii inapata bahari sahihi na kwa wakati. Kwa kweli niwaponegeze Chuo cha Habari kilichokuwepo hapa kimeleta tija kubwa ndani ya nchi hii, vijana wengi wameweza kusoma na wameweza kujiajiri wenyewe katika sekta hii ya habari. Naomba nichukue nafasi hii kuwapa pongezi maalum Wizara hii kwa kazi hii na kuwawekea mazingira mazuri waandishi wetu kuhakikisha wanafanyakazi zao bila ya kikwazo chochote.

Mhe. Naibu Spika, naomba nichangie pia hoja katika sekta ya utalii. Wenzetu wamefanya kazi kubwa. Sekta ya utalii inatangazwa kila kona. Leo hii unapanda ndege unaingia kwenye *Qatar Airways* unakuta matangazo ya utalii, lakini unakaa hoteli umesafiri unakuta matangazo ya utalii na unaiona Zanzibar unajikumbusha nyumbani. Kwa hivyo inaleta raha na inaleta hamasa. Kwa kweli wanafanyakazi kubwa utalii umetangazwa kwa kiasi kikubwa sana. Pamoja na vivutio vingi ambapo sasa hivi wananza kuviweka, kuweka matamasha maalum lakini kuweka nyumba zetu zile za makumbusho na kumbukumbu katika hali yake. Niwaombe tu wenzetu wa Wizara waendelee kuendelea kuweka vivutio vingi na vile ambavyo bado havijafanyiwa kazi yale magofu na mengine basi waweke utaratibu ili waweze kuendeleza.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, katika sekta hii pia naomba nizungumzie nyumba ile iliyozungumzwa kuhusiana na nyumba ya Makunduchi ambayo ilikuwa nyumba ya Shirika la Utalii. Nyumba ile naomba niwaambie ndugu wananchi na Waheshimiwa Wawakilishi wa Baraza hili la Wawakilishi. Nyumba ile ni

nyumba ya serikali, nyumba ile si nyumba ya mtu binafsi, nyumba ile iko pale kwa mkataba maalum ambao serikali imeingiana nao na kampuni ya *CAA* ya Switzerland, mkataba ule ni mkataba ambao bado serikali imeingia nao lakini ni mkataba ambao bado Serikali inamiliki nyumba ile. (*Makofi*).

Kwa hivyo naomba niwatoe hofu, naomba niwaambie wananchi ambao wanaotusikiliza kwamba nyumba ile si nyumba ya Mwalimu Haroun Ali Suleiman, nyumba ile ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na itaendelea kuwa ni nyumba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Nasikitika sana muulizaji wa swali lile hayupo lakini najua atapewa taarifa na naomba nimwambie kwamba nyumba ile ni ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, lakini pia niwashukuru sana wenzetu wa Wizara ya Habari kwa suala zima la kukuza michezo na kukuza vipaji vya vijana wetu, wanafanya kazi kubwa. Watoto wetu sasa hivi tumeshuhudia ndani ya maskuli na maeneo mbali mbali wanajikita katika suala zima la michezo, na hata sasa hivi programu maalum wameanzisha kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu katika kukuza sekta hiyo. Lakini pia hapa naomba niwaombe sana Wizara hii ya Habari, Utalii na Michezo kwamba katika skuli zetu za Maandalizi pia tuziangalie, kuna michezo yetu ile ya asili ambayo waendelee kushirikina na Wizara ya Elimu, kuna michezo kama Hadi Mfundo, Kinyuki Kipenya penya, michezo yote hii tulicheza.(*Makofi*).

Lakini leo hii kama Umeta, Ukuti na mengine ambayo sasa hivi watoto wetu wengi hawaijui. Watoto wetu wamejikita sana katika undawazi wa simu na mambo mengine. Niombe tu katika Skuli ya Maandalizi basi tuanze programu ya kurejesha ile michezo yetu ya zamani ili watoto wetu waweze kuelewa kwamba nini kipo na nini kilikuwepo sisi wazee wao ambao tuliifanya. Kwa hivyo, naomba sana hili pamoja na pongezi na kukuza vipaji vya watoto wetu katika mipira. Lakini pia waangalie na watoto wanawake katika kukuza vipaji vya *netball* na michezo mengine.

Mhe. Naibu Spika, lakini vile vile naomba nizungumzie suala la utamaduni pamoja na kazi kubwa wanayoifanya. Sasa hivi ukisikiliza Redio Zanzibar unaona raha, unasikia pia hata zile nyimbo za zamani zinarudiwa za wazee wetu. Kwa hivyo bado waendelee na jitihada ile ile, nawapongeza sana kwa kazi kubwa wanayoifanya.

Lakini ukiangalia vipindi vyetu sasa hivi vya *ZBC* redio na televisheni wanafanyakazi kubwa na wanafanyakazi kubwa ya kuelimisha jamii, wanafanyakazi kubwa ya kuwakumbusha wananchi na wanafanyakazi kubwa

hata ya kutukumbusha sisi viongozi wajibu na mamlaka yetu. Kwa hivyo naomba niwapongezee waendelee na hilo na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu ataendelea kuwasaidia. (*Makofi*).

Lakini katika hili pia nilikuwa naomba Mhe. Naibu Spika, katika yale mambo niliyoyasema tukumbushane hasa kwa *ZBC,* wakumbuke pia zile ngoma zetu za asili, kama "Lele Mama, Mwanandege, Kunguyia". Sasa hivi ni ngoma ambazo zinaendelea kupotea. Lakini tuanze kuzikumbusha katika kuzitoa vipindi maalum ili tuone wananchi wetu wanaweza kuzijua lakini hata katika maeneo yetu ya maskuli basi na hili pia likaweza kufanyiwa kazi.

Pia naomba nizungumzie suala hapa liliulizwa kuhusu nguzo za umeme katika viwanja vya mipira. Naomba niseme nimeshalijibu sana suala hili katika ukumbi huu huu, kama nirejee kwenye Kanuni kifungu cha 37 kile namba 3(2), kwamba suala hili tumeshalijibu zaidi ya mara tatu, lakini bado limeendelea kujikita katika wizara hii ambayo limesemwa.

Naomba niseme kwamba suala hili bado itabidi nikae na wenzangu wa Manispaa na wenzangu wa Wizara ya Habari na Michezo, basi tuone tunalifanyaje na kulitolea miongozo tutashauriana. Lakini ni suala ambalo sisi kwa upande wetu tumeona kwamba ni suala ambalo liko sawa kwa sababu tuliwekwa kwa utaratibu, kwa sababu sote tunapenda michezo. Lakini hao waliofanya kazi wanajua umuhimu wa viwanja vile. Lakini kwa sababu ya gharama kubwa mwanzoni mulizisema na nimeshajibu mara kwa mara kuna siku kuu lakini kuna sherehe na vitu vyengine, tukaona kwamba ni vizuri tukajiekeza ili tuweze kuendelea. Lakini tutaendelea kushirikiana na Wizara nyengine ili kuhakikisha kwamba suala hili tunalifanyia kazi kwa utaratibu maalum.

Mhe. Naibu, naomba niwapongeze sana, niendelee kuwashukuru sana wenzetu wa Wizara hii kuendelea kutukuzia vipaji kwa watoto wetu.

Baada ya hayo Mhe. Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja asilimia mia juu ya mia na naomba kabisa Baraza lako tukufu waweze kuipitisha bajeti hii wa Wizara ya Habari na Utalii bila ya tatizo lolote ni Wizara ambayo ina umuhimu wake katika kukuza maisha yetu ya kila siku.

Naomba kuunga mkono asilimia mia juu ya mia. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana nakushukuru Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji na Nishati. Sasa nimpishe Mhe. Naibu Waziri wa Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo naye kuweza kuchangia.

Mheshimiwa nakupa muda wa dakika kumi na tano. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia na kujibu baadhi ya hoja ambazo wamezitaka Waheshimiwa wachangiaji kupata ufafanuzi.

Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, naomba nimsaidie Mhe. Waziri baadhi ya hoja nitaenda katika sehemu ya michezo na utamaduni kwa baadhi ya hoja ili kuweza kumsaidia na kumpunguzia wingi wa hoja.

Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu Subhana wa Taala ambaye ametujaalia kuwepo hapa katika Baraza lako Tukufu. Lakini pia naomba kuchukua nafasi hii kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kututeua sisi na kusimamia hii Wizara pamoja na viongozi wote wa wizara hii.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, vile vile napenda sana nitoe shukurani kwa familia yangu akiwemo mume wangu mpenzi ambaye ananipa mashirikiano na kuweza kufanya kazi vizuri.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, naomba pia nimshukuru Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Habari na Utalii kwa kutuongoza vizuri na kutuelekeza baadhi ya majukumu au yale mambo yanatakiwa tuyatekeleze ili kuona kwamba Wizara inafanyakazi zake kwa uhakika na kupata matarajio yale ambayo wananchi wanayahitaji.

Mhe. Naibu Spika, pia naomba niwashukuru wale wote ambao wamechangia hoja yetu na bajeti katika Wizara yetu ya Habari na pia naomba sasa niende moja kwa moja katika hoja ambazo wametaka baadhi ya wachangiaji kupata ufafanuzi na kuona utekelezaji wake.

Mhe. Naibu Spika, naomba niende kwenye michezo. Mhe. Ali Suleiman Ali ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ametoa hoja kwamba Wizara isimamie migogoro kwa vyama vya michezo. Na Mhe. Abdalla Maulid Diwani pia naye alitaka kujua Wizara isimamie kati ya BTMZ na *ZFA* Wilaya ya Mjini na Mhe. Jaku Hashim Ayoub pia naye alitaka kujua elimu itolewe kupunguza mgogoro kati ya BTMZ na *ZFA*.

Majibu ni kwamba Wizara imepokea ushauri huo uliotolewa na Waheshimiwa wachangiaji katika kuona unasimamia migogoro iliyotekelezwa kwa Vyama vya Michezo, Baraza la Taifa la Michezo la Wilaya pamoja na kutoa elimu kwa BTMZ na *ZFA* kwa lengo la kupunguza migogoro.

Mhe. Naibu Spika, pia Mhe. Abdalla Maulid Diwani katika hoja yake alitaka kujua Chama cha Kunyanyua Vitu Vizito au Vyuma Vizito ni chama pekee kilichopata usajili duniani, lakini kukosa kupatiwa ruzuku za kushiriki mashindano mbali mbali pamoja na kulipia ada za kimataifa.

Jibu ni kwamba Mhe. Naibu Spika, wizara kupitia BTMZ inasaidia Chama cha Kunyanyua Vitu Vizito kwa kuwapatia fedha za kushiriki mashindano ya kimataifa yaliyofanyika nchini Jordan mwaka 2016/2017 na ada ya wanachama. Aidha chama kimewapatia fedha za kuendesha mafunzo ya mchezo huu yaliyofanyika Pemba. Wizara imeendelea kuvisaidia vyama vya mchezo kila hali itakaporuhusu.

Mhe. Naibu Spika, pia Mhe. Abdalla Maulid Diwani ametoa hoja kwamba kwa nini ruzuku ya Baraza la Michezo imepungua kutoka milioni thamanini na nne kwa mwaka 2016/17 mpaka milioni sabini na laki tisa kwa mwaka wa fedha 2017/18.

Jibu ni kwamba Wizara imeongeza fedha zaidi kwa kushiriki timu katika bajeti Idara ya Michezo mpaka wa fedha 2017/2018.

Pia Mhe. Naibu Spika, Mhe. Abdalla Maulid Diwani ametoa hoja kwamba wizara kuangalia suala la utitiri wa vilabu vya mpira wa miguu hadi kufikia kumi na mbili.

Mhe. Naibu Spika, jibu ni kwamba suala la utitititiri wa vilabu litatatuka mara tu baada ya *ZFA* kumaliza Ligi Kuu Zanzibar na baadae kucheza ligi maalum ya kuzipata timu 12. Lakini Mhe. Naibu Spika, pia Mhe. Hussein Ibrahim Makungu na Mhe. Dkt. Sira Ubwa Mamboya pia walitoa hoja kwamba Wizara ihamasishe vijana na wazee kushiriki katika mazoezi na michezo ili kujenga afya zao. Mhe. Naibu Spika, ushauri huu tumeupokea na tutaufanyia kazi.

Mhe. Naibu Spika, pia Mhe. Dkt.. Mwanyihaji Makame Mwadini pia ametoa hoja na ushauri sio kufungia kiongozi wa michezo miaka kumi. Jibu ni kwamba ushauri wake umepokelewa na utafanyiwa kazi kwa mujibu wa Sheria na Kanuni. Mhe. Naibu Spika, vile vile Mhe. Jaku Hashim Ayoub na Mhe.

Suleiman Sarahan Said pia na wao wametoa pongezi kwa kutiwa *tartan* ya kisasa kwa uwanja wa Gombani Pemba.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, pongezi hizi tunazipokea na pia wananchi nao wajue kwamba kuna umhimu mkubwa wa kuzitumia *tartan* hizi na wao pia wasivute sigara wakati wakiwemo katika mechi ambazo wamepangiwa.

Mhe. Naibu Spika, pia Mhe. Abdalla Maulid Diwani ametoa hoja kwamba mtaro uliopo viwanja vya Mnazi Mmoja ukamilishwe ili kupata nafasi kwa wanamichezo kuvitumia pamoja na kuondosha nguzo za umeme. Jibu ni kwamba ni kweli kuwa viwanja vya Mnazi Mmoja kuna mtaro pamoja na nguzo za umeme ambazo zinaleta usumbufu kwa wanamichezo. Wizara ikishirikiana na Manispaa na Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kuona mtaro unakamilishwa na nguzo za umeme zinaondolewa.

Mhe. Naibu Spika, sasa naomba niende kidogo katika suala la utamaduni. Mhe. Naibu Spika, Mhe. Hidaya Ali Makame, Mhe. Omar Seif Abeid hawa nao pia wametoa hoja wananchi wahamasishwe na waelimishwe juu ya matumizi sahihi na sanifu katika matumizi yao ya kawaida, na pia wamesema kwamba Kiswahili kiendelee kutumika vizuri katika Sheria, Baraza la Wawakilishi na kwa jamii. Mhe. Naibu Spika, ushauri huu tumeupokea na tunaufanyia kazi.

Mhe. Naibu Spika, pia Mhe. Suleiman Sarahan Said alitaka kujua idadi za ngoma za asili vipi zinaendelezwa. Mhe. Naibu Spika, kwa mujibu wa takwimu tulizonazo jumla ya ngoma za asili ni 263 Pemba na Unguja 410. Ngoma zinazosaidiwa ni vile vikundi vya ngoma vilivyosajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya mwaka 2015.

Vile vile Mhe. Naibu Spika, Mhe. Hidaya Ali Makame pia katika utamaduni katoa hoja kwamba vikundi vya ngoma asilia viimarishwe na viwezeshwe. Mhe. Naibu Spika, jibu ni kwamba kikundi cha Mchikicho tayari kinatambuliwa kisheria. Pili kinashirikishwa katika shughuli za kitaifa. Tatu kimeshaingizwa katika programu ya kupatiwa mafunzo. Vile vile tunaweka mikakati ya kuvijali vikundi hivi na sio kuwapa leseni tu.

Mhe. Naibu Spika, pia Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis yeye katoa hoja kwamba kuna tangazo ambalo linaonekana linawadhalilisha wanawake.

Mhe. Naibu Spika, naomba nimjibu Mhe. Mwantatu kwamba tangazo hili ni kweli lipo na hili tumelipokea tutalifanyia uchunguzi na tukihakikisha kwamba kuna maneno pale ambayo yanamvunja moyo mwanamke au yanamdhalilisha

mwanamke, basi tutalifanyia marekebisho, kwani yapo matangazo au baadhi ya matangazo ambayo yalionekana kwamba hayaendi vizuri na tumeyafanyia marekebisho na sasa hivi yanakwenda vizuri tu, kwani tunajua umuhimu wa mwanamke. Sio sisi tu hata katika Dini Bwana Mtume Muhammad (SAW) wakati inaanza kusambaa au inaanza kuenea Dini ya Allah Bi. Khadija alikuwa mbele na kumpa ushauri Bwana Mtume Muhammad (SAW) na akaweza kuendeleza Dini ile.

Ahsante Mhe. Naibu Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Naibu Waziri. Kabla ya kumpisha Mhe. Waziri wa Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo naomba nitoe tangazo la wageni wetu. Ni wageni wa Mhe. Nassor Salim Ali Al-Jazira Mwakilishi wa Jimbo la Kikwajuni, wanatoka Kikundi cha Sanaa cha Matofali *Art Creation Zanzibar*.

Wageni hao ni ndugu Mohamed Said ambaye ni Mkurugenzi wa kikundi, ndugu Peter Mashauri na Bi. Tatu Mwalimu. (*Makofi*)

Karibuni sana ndani ya Baraza letu.

Waheshimiwa Wajumbe wageni wetu hawa kwa kuwa ni wasanii, wamekuja na *CD* zao ambazo kwa sababu wao wanajua kwamba sisi ni wadau wakubwa wa wasanii wametuletea *CD* na kwa bei ndogo sana wanauza *CD* hizo. Kwa hivyo ningeomba sana kwa ajili ya kukuza sanaa Zanzibar, Waheshimiwa Wajumbe nakuombeni sana mtowe mchango kwa kununua *CD* ambazo wamekuja nazo.

Ahsanteni na karibuni tena. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe sasa nimpishe Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo aje ajibu hoja za Waheshimiwa Wajumbe. Mheshimiwa karibu sana.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: *Rabbi Shrahli Sadri wa* ***Y****assirli Amri Wahlul Uqdatan millisani Yafqahu Qawli, Bismillah Rahman Rahim.*

Mhe. Naibu Spika, awali ya yote kwanza nikushukuru wewe kwa jinsi namna unavyoongoza mijadala yako hii na kwa kunipatia fursa asubuhi hii ili kuweza

kusimama hapa kuendeleza kutoa ufafanuzi wa hoja ambazo zimetolewa na Wajumbe.

Baada ya kunipa fursa hiyo nimshukuru Mwenyezi Mungu Subhanahu Wataala, kwa kutujaalia uwezo kuweza leo kurudi kwenye Baraza letu hapa, tukiwa wazuri wa afya, wenye afya zilizotimia na *In shaa Allah* Mwenyezi Mungu ataendelea kutubariki, kutupa afya na pumzi ili tuweze kuendeleza shughuli zetu za kawaida siku hadi siku.

Mhe. Naibu Spika, kabla ya kutoa ufafanuzi wa hoja, naomba sana nitoe pole kwa familia na wana michezo wa kifo cha Mzee Mgeni Mwalimu Ali, mchezaji wa zamani na *captain* wa Timu ya Miembeni na Timu ya Taifa ya Zanzibar ambaye pia ni Mkurugenzi Mstaafu wa *Press* na Idara ya Michezo na Kamishna wa Tume ya Utumishi wa Umma Serikalini ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mwenyezi Mungu amjaalie makaazi mema, ampe kila lenye kheri katika kaburi lake na alizidishe kaburi lake kuliingiza nuru na *In shaa Allah* akapumzike salama.

Mhe. Naibu Spika, nimetoa pole hizi kwa sababu sekta yetu inahusiana sana na juhudi zilizofanywa na Marehemu Mzee Mgeni Mwalimu Ali. Kwa hivyo Mwenyezi Mungu namuomba kwa rehma zake na kwa niaba ya Baraza hili tukufu, amjaalie kumpa safari njema na sisi watarajiwa *Inshaallah* twende hali ya kuwa tunakwenda safari njema anayoielekea yeye.

Mhe. Naibu Spika, sasa nitoe ufafanuzi wa hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu la Wawakilishi katika kuchangia hotuba ya bajeti ya Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mhe. Naibu Spika, kwa mara nyengine tena naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa kunipa fursa hii kufanya majumuisho ya hoja, michango na mapendekezo yaliyotolewa na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu wakati wa kuchangia hotuba ya bajeti ya Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo kwa mwaka huu wa fedha tunaouombea bajeti.

Mhe. Naibu Spika, nichukue fursa hii hali ya kuwa najua kwamba tunatakiwa tujibu hoja kwa muda wa saa moja, kuwashukuru na kutoa shukrani zangu za dhati kabisa kwa Kamati ya Kudumu ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii ambayo imekuwa ikishirikiana na sisi tangu tulipoanza matayarisho hadi kuwasilisha hotuba hii, na leo tunaikamilisha mashirikiano yao bado ni makubwa sana, naishukuru sana Kamati. *(Makofi).*

Mhe. Naibu Spika, shukrani za pekee zimuendee Mwenyekiti wa Kamati hiyo Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Kijitoupele, ambaye katika hotuba yake aliyoiwasilisha kwa ustadi kabisa aliwahakikishia Wajumbe wote kwamba, michango na maoni waliyoitoa na itakayochangiwa kwa dhati na kwa umoja wao tutaipokea na tutaithamini na tuna ahidi tutaifanyia kazi ipasavyo kabisa. *(Makofi).*

Mhe. Naibu Spika, nawashukuru Wajumbe wote waliochangia hotuba yangu moja kwa moja na wale waliochangia kwa maandishi, na wale wote ambao hawakuchangia, kunyamaza kimya kwao kulikuwa kunaonesha ishara ya kwamba hotuba yetu wameifahamu vyema na michango yao ilikuwa imejibika bila ya kuitoa.(*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, mimi pamoja na Mhe. Naibu Waziri kwa niaba ya watendaji wa Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo tunazipokea pongezi za dhati kabisa zilizotolewa, takriban na Waheshimiwa wote wa Baraza lako Tukufu hili. Aidha, ushauri, maelekezo, muongozo, maswali na mapendekezo yote kwa pamoja yaliyotolewa, basi tunaahidi kuyafanyia kazi ili kuongeza kasi ya kuwaletea wananchi waliomchagua Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kishindo kikubwa na cha aina yake. Sasa wanapata maendeleo wanayoyatarajia, hili ni tegemeo letu. *(Makofi).*

Mhe. Naibu Spika, jumla ya Waheshimiwa Wajumbe 31 wa Baraza lako Tukufu walichangia hotuba yangu. Waheshimiwa Wajumbe 15 walichangia moja kwa moja na Waheshimiwa Wajumbe 16 walichagia kwa maandishi.

Mhe. Naibu Spika, kabla ya kutoa ufafanuzi wa hoja zilizowasilishwa naomba nitumie fursa hii kuwatambua kwanza Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii waliotoa msukumo mkubwa kwa michango yao kama ifuatavyo.

1. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) Mwenyekiti
2. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Hassan Khamis Hafidh Mjumbe
4. Mhe. Maryam Thani Juma Mjumbe
5. Mhe. Zaina Abdalla Salum Mjumbe
6. Mhe. Jaku Hashim Ayoub Mjumbe
7. Ndg. Hamid Haji Choko Katibu
8. Ndg. Haji Jecha Salum Katibu
9. Ndg. Amina Abeid Hemed - Mkalimani ambaye anatusaidia kuleta matangazo haya kwa kutumia lugha za alama.

Mhe. Naibu Spika, aidha sasa naomba niwatambuwe Waheshimiwa Wajumbe waliochangia moja kwa moja na kwa maandishi kama ifuatavyo.

Waheshimiwa Wajumbe waliochangia moja kwa moja ni:-

1. Mhe. Ali Suleiman Ali
2. Mhe. Abdalla Maulid Diwani
3. Mhe. Jaku Hashim Ayoub
4. Mhe. Mwantatu Mbarouk Khamis
5. Mhe. Suleiman Sarahan Said
6. Mhe. Hidaya Ali Makame
7. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu
8. Mhe. Abdalla Ali Kombo
9. Mhe. Mohamed Said Mohamed
7. Mhe. Nassor Salim Ali
8. Mhe. Miraji Khamis Mussa
9. Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil
10. Mhe. Ali Salum Haji
11. Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum)
12. Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Ujenzi, Nishati na Mazingira

Nawashukuruni sana kwa michango yenu na ninawashukuru sana kwa michango mliyoitoa kwa njia ya maandishi, ilikuwa ni *constructive* na ilikuwa kwa kweli inatulenga katika kutekeleza majukumu yetu. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, hoja za Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu wakati wa kutoa michango yao ilijikita katika maeneo mbali mbali yakiwemo maeneo makuu yafuatayo.

Moja, ilikuwa ni eneo la utalii ambalo liligusa zaidi utalii wa ndani na utalii wa kawaida, ukusanyaji wa takwimu sahihi za utalii, ukusanyaji wa mapato. Lakini vile vile kwa upande wa michezo ilizungumzia sana hoja za mgogoro wa *ZFA* na *BTMZ*, hoja katika ujenzi wa Uwanja wa Mao Tse Tung, ujenzi wa viwanja vya michezo vya Wilaya Unguja na Pemba, hoja ya maandalizi ya timu za vijana na taifa, vile vile na Zanzibar kujiunga na shirikisho la mpira wa miguu Barani Afrika (*CAF)*.

Aidha, maeneo ya habari, *ZBC* na maeneo mengine yaliguswa kwa uchache kabisa. Mhe. Naibu Spika, kwa mara nyengine nampongeza sana Mhe. Ali Suleiman Ali kwa niaba ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii kwa hotuba yake nzuri iliyoonesha matumaini kwetu, tena ni matumaini

makubwa na ya kujenga hoja ya kuendeleza na kuimarisha wizara yetu ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo.

Mhe. Naibu Spika, sasa kwa ridhaa yako na kwa ruhusa yako naomba kutoa ufafanuzi wa hoja kwa Waheshimiwa Wajumbe wote kwa mujibu wa muundo wa wizara yangu.

Mhe. Naibu Spika, nitaanza na sekta ya habari, kuweza kuwaeleza namna hoja zilivyotolewa. Namshukuru sana Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo kwa kupunguza kujibu baadhi ya hoja nyingi kabisa ambazo zimetolewa.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Abdalla Maulid Diwani na Mhe. Suleiman Makame Ali waliuliza hoja kubwa ya matangazo ya *ZBC TV* kwenye king'amuzi cha *Azam television* hayapatikani wakati mteja anaposhindwa kulipa ada ya mwezi. Nataka niwaambie kwamba ni kweli kwamba Kituo cha Televisheni cha Shirika la Utangazaji *ZBC*, ndio kituo pekee cha umma cha utayarishaji wa maudhui kinachorusha matangazo yake kote Unguja na Pemba, na kwamba Kituo cha Azam TV kinalazimika sasa kuibeba katika king'amuzi chake na kuonekana muda wote, hata mteja anaposhindwa kulipia ada ya mwezi.

Nataka ifahamike wazi kwamba kukosekana kwa matangazo ya *ZBC television* kwenye king'amuzi cha Azam *TV* na televisheni nyengine ambazo zimetajwa kinapokosa malipo ya mwezi ni tatizo linalotokana na utaratibu uliotumika awali. Lakini kwa uongozi wetu tuliokuwa nao basi tunawahakikishia suala hili tunalifanyia kazi, tunalifuatilia na litaondoka hapo tunapoendelea.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Mohammed Dimwa aliuliza juu ya ving'amuzi vipya vitafika lini, mchango wa *ZMUX* mita 250 ni mdogo mno angalau ufike 300, *ZMUX* ni idara au iko chini ya wizara. Napenda kumpa jibu sahihi Mhe. Mohammed Dimwa kwamba ving'amuzi vipya tayari vimeshafika, taratibu za mauzo zinakamilishwa. Muda mchache Waheshimiwa Wajumbe tutatoa bei na natumaini kwamba Baraza lako tukufu wote watanunua ving'amuzi hivyo ambavyo naamini vitauzwa kwa bei rahisi kuliko king'amuzi chengine chochote, lakini vitalingana na ving'amuzi vyengine.

Mhe. Naibu Spika, vile vile mpaka sasa *ZMUX* nataka kuwathibitishia kwamba ipo chini ya wizara tunasubiri maelekezo tu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, ili tupate muongozo wa kisheria ulio madhubuti kuiweka ile *ZMUX* kuwa ni kampuni au kuendelea kuwa ni ya wizara. Hivyo baada ya kupata ushauri kwa

Mhe. Mwanasheria Mkuu tunaweza tukawaelezea Wajumbe hapo uwazi *ZMUX* utakavyokua na muundo gani ambao inaweza ikatumia.

Mhe. Naibu Spika, hayo yalikuwa ni maelezo yanayohusiana moja kwa moja na Kitengo cha *ZMUX*, lakini nikaja kwenye Kitengo cha *ZBC* yenyewe. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis aliuliza suala zuri sana kutokuajiriwa kwa wakalimani wa lugha ya alama. Suala la kuajiriwa wakalimani wa lugha za alama limeshawasilishwa utumishi, elewa wazi kwamba Utumishi wa Umma umeshapokea maombi yetu katika mpango wa miaka mitano wa raslimali watu na wanatarajiwa kuajiriwa wakati wowote ifikapo Julai 2017. *(Makofi)*

Mhe. Mwantatu kuwa na faraja. Nataka kukujulisha kwamba kwa sasa hivi wako watatu ambao hulipwa posho kila mwezi. Ni matarajio yetu kwamba utaratibu wa kuhakikisha kwamba wanatangaza matukio muhimu ya kitaifa tumeupokea na tumeufanyia kazi na wakati wowote unaweza ukaonekana namna gani unatekelezwa.

Mhe. Suleiman Sarahan tena aliuliza suala la *ZBC*, Pemba haina vifaa vya kutosha, hivyo kushindwa kufanyakazi kwa ufanisi. Ni kweli *ZBC* ina changamoto ya vifaa kwa Unguja na Pemba na ndio maana tunasema tuko katika marekebisho. Vifaa vya utangazaji ni vya gharama kubwa, sote sisi hapa ni mashahidi namna gani tunavyoona bajeti zetu tunavyozipitisha kununua vitu hivyo.

Kwa hivyo basi kwa sasa *ZBC* Pemba nataka ifahamike kwamba inazo kamera mbili, ukiacha ile moja iliyoharibika maharibiko madogo. Hivyo zitakuwa ni kamera tatu. Lakini *ZBC* Dar es Salaam ina kamera mbili, vile vile *ZBC* Unguja ina kamera sita. Napenda nimueleze Mhe. Suleiman Sarahan kwamba kutokana na juhudi anazochukua Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika kuyatekeleza haya, basi tunaamini matatizo hayo yataisha kabla ya Disemba mwaka huu wa 2017.

Mhe. Suleiman Ali pia na yeye aliuliza kuhusu wafanyakazi wa kujitolea kuajiriw. *ZBC* imo katika *reform* hivi sasa. *Reform* maana yake ni marekebisho ya mfumo mzima wa utengenezaji wa Shirika letu la *ZBC* ili liweze kujiendesha. Kwa hivyo tunaelewa kwamba kwa sasa kwenye eneo la raslimali watu litafanyiwa kazi kwa kina kabisa na kwa mujibu wa taratibu, sheria na kanuni ambazo sheria hizo tumezitengeneza hapa Baraza la Wawakilishi kwa kuunda Sheria inayopaswa kuliweka Shirika la Utangazaji (*ZBC).*

Mhe. Nadir Abdul-latif na yeye kuhusu suala la mitambo aliulizia, vipindi kuimarisha mitambo na vipindi vya *ZBC* pamoja na kukatikatika kwa matangazo ya *ZBC*. Nashukuru sana suala hili limepata ufumbuzi wakati Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira amelijibu hapa kwa vizuri sana. Lakini kwa sasa nimejaribu kutazama hata kiooni mimi mwenyewe najiona na hakuna vimeme pale kwenye *ZBC television.(Makofi*).

Mhe. Maudline Castico na yeye alitoa pongezi za dhati kuandaliwe vipindi vya mjadala kwa wanafunzi. Tumelipokea ombi lako na ushauri wako na *ZBC* imelichukua suala hilo na kulifanyia kazi chini ya Wizara yetu ya Habari, Utalii, Utangazaji na Michezo.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi uliuliza sana juu ya *ZBC* ipatiwe vifaa ili iweze kufika mpaka vijiji kupata taarifa. Hili ni suala zuri sana na lina umuhimu mkubwa sana na tunaamini kwamba tupo hapa kwa kuwahudumia wananchi. Tunauchukua ushauri huu na tutaufanyia kazi kama nilivyoeleza *ZBC TV* na redio kwa sasa zipo katika kuimarishwa, baada ya muda mfupi Wahesimiwa Wajumbe nitawaomba mkatembelee katika *ZBC television* na *ZBC radio*, ili kuona matengenezo na matarajio tunayotaka kuyafikia.

Mhe. Shaib Said Ali na yeye alisema *ZBC* iimarishwe vipindi ili watu wengi waisikilize. Kama lilivyojibiwa na Mhe. Naibu Waziri pamoja na maoni ya Mhe. Riziki Pemba Juma kuhusu kipindi cha vuna kipaji, ushauri huo wote tumeupokea wa kutaka vitengo viliopo Pemba pamoja na waandishi wapatiwe vifaa na ajira. Ushauri huo tumeupokea na hatua tunakuhakikishia kwamba zinaendelea hivi sasa.

Mhe. Suleiman Sarahan tena ijengwe fensi kwenye kituo cha Pemba, tunajua fensi ile pale kweli ni udhia wa muda mrefu, lakini pamoja na vifaa vya kutangazia na gari ziwekwe nembo za *ZBC* kama inavyoonekana mabasi ya Uingereza yalivyotangaza utalii wetu hapa Zanzibar. *ZBC* hivi sasa ipo kwenye mradi wa kuliimarisha shirika. Narudia tena hivi sasa ipo katika ujenzi na maeneo mbali mbali hatua kwa hatua na hilo tumelipokea na ukuta Pemba utajengwa na ikiwezekana maandishi na mtangazo yatawekwa katika magari yetu yote ya *ZBC*.

Mhe. Abdalla Ali Kombo nyimbo za zamani hasa zile za dansi kama Tokomile tulivu, Mkude, Sikinde nazo ziwe zinapigwa kwa kirefu ndani ya redio. Lakini nataka kukuthibitishia kwamba mimi mweyewe vile vile ni mshabiki, mimi mwenyewe nipo katika uwanachama wa Sikinde. Kwa hivyo ngoma za Sikinde huwa tunazisikia kidogo kidogo. Nakuomba tu na wewe uwe msikilizaji mzuri

wa redio, ngoma hizo tushazirekodi za zamani tumeshazirudisha zipo. Kama zinavyopatikana hotuba za viongozi wetu na ngoma hizo ndio zinavyopatikana. Kuna taratibu za kuongeza vipindi Mheshimiwa utaburudika, lakini tunakuomba sana uwe mtazamaji mzuri wa televisheni vile vile uwe msikilizaji mzuri wa redio.

Mhe. Hidaya Ali Makame kuimarisha vipindi vya ngoma za asili na watangazaji kuvaa mavazi ya Kizanzibari. Ni suala zuri tunalikubali la kulinda mila yetu. Ushauri wako tumeupokea tutaangalia jinsi ya kuutekeleza kwa mujibu wa sheria na taratibu ziliopo, kwa sababu sheria ni kitu cha kukizingatia.

Lakini hapa hapa aliingia Mheshimiwa Ali Salum kipindi cha michezo kimepunguziwa muda na ombi lake ni kukirusha *live*. Nasema ombi lake ni zuri na lenye muelekeo wa tija kubwa sana katika kutengeneza na kuimarisha *ZBC* na redio. Lakini tumelichukua suala hilo na tutalifanyia kazi ipasavyo na matokeo Mheshimiwa kila yatakapokuwa yanabadilika tunachukua ahadi ya kuja kukunong'oneza kwamba sasa hivi matokeo yanaonekana mengine.

Kulikuwa na suala la mwisho kwa upande wa *ZBC* ambalo liliulizwa na Mhe. Abdalla Maulid Diwani juu ya malipo ya *contractor* Bwana Ayoub na vile vile *ZBC 2* ni ya nani natumaini buti lako hapa litagonga chini lakini kugonga chini kwake halitatoka mlio. Je, Serikali inapata faida gani juu ya hili ni masuala aliyouliza Mhe. Abdalla Maulid Diwani suala hilo tumelikuta tunajua na tumeliona na tumeanza kulifuatilia na kulifanyia kazi ipasavyo.

Nataka kukuthibitishia kwamba *ZBC 2* inamilikiwa kwa pamoja kati ya *AZAM PAY TV* na *ZBC* ni umiliki wa pamoja na nembo ya *ZBC* maana yake ni *Zanzibar Broadcast Corporation* kwamba yetu haina mjadala ambapo makubaliano yaliyofanyika ni kuwa *AZAM PAY TV* atatoa gharama zote za uendeshaji wa *TV*, kitu ambacho kwa *ZBC* isingekuwa rahisi kuzikamilisha katika kurusha televisheni ile kwenye *Satellite*. Namshukuru sana Mzee Bakharesa kutukubalia kubeba gharama zile na kuweza kuziweka gharama zetu zote kwenye *PAY TV* ya *AZAM*. Katika gharama zile alizozibeba inasababisha kabisa sisi kupata fursa kuitumia *ZBC* kwenye matangazo na kwenye hali yoyote ile tunayotaka kutangaza kupitia *ZBC*.

Hivyo basi kwa upande wa matangazo yoyote yatakayotangazwa na *ZBC* pamoja na yale yatakayotangazwa asilimia hamsini kwa hamsini zinapaswa kupatikana, kama kulikuwa kuna kasoro tumeziona tunazifuatilia na nakuhakikishia Mhe. Abdalla Maulid Diwani kwamba suala la *ZBC 2* karibu

litakuwa sio *issue* na litakuwa limekaa sawa. Lakini bado naendelea kumpongeza Mhe. Said Salim Bakharesa kwa jitihada yake ambayo anaendelea kutusaidia. Kampuni ya *AZAM* kwa kutupatia msaada mkubwa kabisa kama huu. Hivyo naomba tuendeleze mashirikiano yetu ya kampuni hiyo na *AZAM* na hata kama mkataba huo utakuwa umefikia mwisho *ZBC* pamoja na Wizara ya Habari, Utalii na Michezo itarudi kabisa kuweza kuendeleza mkataba huo kwa sababu manufaa makubwa ni kwa Serikali yetu na wananchi wetu wa Zanzibar.

Nikitoka katika hoja ya *ZBC* niingie hoja fupi zilizokuwepo katika magazeti Mhe. Abdalla Maulid Diwani ulitanda sana kuchapishwa gazeti Zanzibar ikiwa halifiki Tanzania Bara ilikuwa linaonekana ni tatizo, habari za michezo za Zanzibar hazipewi kipaumbele dhidi ya Tanzania Bara ndani ya gazeti letu. Kulikuwa kuna suala la Mhe. Suleiman Sarahan faida na hasara zinazopatikana katika kuchapishwa gazeti la Zanzibar, vile vile gharama kubwa za uchapishaji zilizokuwepo katika wakala wa uchapishaji Zanzibar, kulikuwa kuna suala la deni la Shirika la Magazeti kwa T*SN* ambalo limeulizwa na Mhe. Omar Seif Abeid.

Nataka niwajulishe kwamba mipango inaandaliwa kati ya uongozi wa Shirika la Magazeti, Wizara ya Habari, Utamaduni na Utalii kuhakikisha kwamba gazeti linafika Tanzania Bara na muono umeonekana. Nataka nitoe mfano mdogo tu hapa tumegundua kwamba kuna uwezekano wa gazeti kulichapa kabla ya saa 3.30 za usiku, endapo tutaweza kufanya hivyo tutashirikiana na wenye uchapaji na wanaweza kufanya hivyo. Naamini tutatizama kasoro zilizokuwepo ili tuziondoe ili gazeti liweze kuondoka na ndege ya Arusha inayotoka Saa 3.30 Zanzibar kulekea Dar es Salaam. Na *issue* ya gazeti kufika Dar es Salaam itakuwa sio *issue* tena nawaomba Waheshimiwa Wawakilishi msiwe na hofu katika hili.

Kubwa lililokuwepo hapa ambalo nilikuwa nataka niliseme tumeanza uchapishaji Zanzibar tarehe 10\5\2017 mpaka hii leo tarehe 22\5\2017 ni siku kumbi na mbili hata ingekuwa nimeambiwa leo nimeitwa baba na mtoto mchanga basi ingekuwa hajaweza kutamka kwamba mimi ndio baba yake, lakini vile vile mtoto mchanga huyo angekuwa hajatoka arubaini muda ungali mfupi tutulie kwa makini tutaweza kupanga mipango na gazeti nawahakikishia kwamba litafika Bara ikiwa tunajua gazeti la Zanzibar Leo ni kwa ajili ya sera za Serikali kuwapasha habari wananchi wa Zanzibar na sio kibiashara.

Mhe. Suleiman Sarahan Said nimekugusa sana tunatumai kiwanda cha Zanzibar gazeti linasomwa mapema sasa Zanzibar moja ni katika faida hiyo,

vile vile mimi nimekuja na mfano hapa saa 12.30 leo gazeti la Zanzibar Leo lote nimeshalisoma na nimejitahidi saa 1.00 niwaletee Wawakilishi wawe wameshalisoma hapa. Hii ni moja katika faida kubwa sana ya kuhakikisha kwamba gazeti letu linachapwa petu kwa ajili ya sisi na wananchi wetu. Naomba kuwaambia wenzangu hususan *back benchers* Waheshimiwa Wawakilishi tutukuze na tuimarishe chetu mpaka tusahau cha wenzetu, huo ni msemo wa Marehemu Mzee Abeid Amani Karume. Kwa hivyo tuendelee kulitukuza gazeti la Zanzibar Leo.

Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa) aliuliza sana juu ya habari za uchapishaji katika gazeti la *TSN* kama nilivyoeleza hapo nyuma pamoja na Mhe. Omar Seif Abeid lakini mazungumzo yanaendelea ili kiwango cha bei cha mchapaji wa Tanzania Bara kiwe sawa na kile cha Zanzibar. Hili tumelifikia hatua ya kuliamua na ndio maana ukaona magazeti hivi sasa yanachapwa kabisa, wachapishaji ni Serikali. Gazeti ni la serikali, kwa hivyo kufikia hatua za makubaliano kupata gharama zilizokuwa kule ni kubwa kuliko zetu linawezekana. Kubwa lieleweke kwamba gazeti la Zanzibar Leo sio gazeti la kibiashara, lakini katika kuchukua maoni ya Mhe. Juma Ali Khatib gazeti lifike mapema Tanzania Bara na yeye pamoja na Mhe. Yussuf Ali Hassan, Mhe. Shaibu Said wote walieleza kutaka kujua faida na hasara pamoja na usambazaji mdogo katika vijiji.

Nataka kuwajuulisha kwamba Waheshimiwa tumeweza kuleta sera hapa sisi ndio Wawakilishi wazuri wa kulisambaza gaeti vijijini, naamini kwamba kila Mwakilishi angeweza kuchukua kopi kumi kwa siku akapeleka katika Ofisi zake zilizokuwepo jimboni, basi gazeti lingekuwa linasambazwa vizuri katika taasisi zetu. Sera hiyo bado tutaendelea kuwasilisha hapa Barazani hata kama ilipigwa chini mara ya kwanza. Lakini sasa nitumie fursa hii niwaombe sana Waheshimiwa Wajumbe waweze kutukubalia, watukubalie basi angalau magazeti matatu na mawili wawe wanachukua kila Mwakilishi na sisi tutaendeleza kazi ya *marketing* kuwaletea kokote mliko magazeti ili muyanunue, sio gharama kubwa ni pesa kidogo tu hivi kama 350,000/= kwa mwezi. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, vile vile Mhe. Harous Said Suleiman naye aliuliza vyombo vya habari ikawa ni suala la mwisho kwenye suala hili namna gani vipatiwe vifaa kwa ajili ya utekelezaji na utendaji kazi. Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Magazeti imeandaa kabisa mpango maalum wa upatikanaji wa vifaa hivi na vinafanyiwa kazi.

Sasa niende moja kwa moja katika suala zima la Chuo cha Uandishi wa Habari. Huku hakukuwa na hoja ambayo ilikuwa imeelezwa zaidi ya kujua kwamba wanafunzi wangapi wameingia. Takwimu zile zilizotakiwa kuletwa. Nataka nimjuulishe tu kwamba kama alivyojibu Mhe. Naibu Waziri wanafunzi wote waliopo chuo hadi kufikia mwezi February 2017 ni 159 baada ya mitihani ya mwezi huu wa Februari, wanafunzi 49 wa cheti waliondoka wakabaki wanafunzi 150, katika udakhili uliofayika wanafunzi 49, wanawake 29 na wanaume 23. Lakini tarakimu ya wanafunzi 248 inajumuisha wanafunzi 99 waliohitumu mwezi February, 2017 ambao walikabidhiwa vyetu katika mwaka 2015/2016. Hizo zilikuwa ni hoja zilizokuwepo katika upande wa habari na mwisho kabisa niweze kutoa majibu kwa upande wa Habari Maelezo.

Mhe. Mwantatu Mbaraka, Mhe. Hidaya Makame, Mhe. Omar Seif Abeid wote kwa pamoja walikuwa wanataka kujua maeneo yaliyoonyeshwa sinema/filamu zenye kuonyesha unyanyasaji. Hili limejibiwa vizuri na Mhe. Naibu Waziri, wananchi wanafaidika vipi na sinema zinazoonyeshwa ni kuhusu kilimo cha mboga pamoja na ziara za Mhe. Rais Wilayani na nyenginezo na Mikoani na nyengine, namna ya kujikinga maradhi ya miripuko kipindupindu. Kwa hivyo ni faida kubwa wananchi wetu kupata elimu kupitia sinema hizo.

Mhe. Omar Seid Abeid mara nyingi nataka nikujuulishe kwamba makampuni yanayojishughulisha na utalii ndio huomba vibali vya kupiga filamu katika maeneo ya vivutio vya utalii. Makampuni yale yaliyoorodheshwa ambayo nimeyatoa katika hotuba yangu hapa mengi yao yalikuwa ni ya kitalii kutoka nje na mengine yalikuwa ni ya hapa Zanzibar.

Sasa niende moja kwa moja kwenye suala zima la sekta ya utalii. Nikenda kwenye sekta ya utalii Mhe. Naibu Spika, ni kwamba Mhe. Mohammed Said Mohamed aliuliza suala la kuimarishwa utalii wa ndani ikiwemo kuongezeka wingi wa maeneo ya utalii. Mfano mapango na maeneo ya historia ambayo Wazanzibari na watalii wanaweza kutembelea. Napenda nimjibu Mheshimiwa kwamba Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo inaendelea na juhudi za kuimarisha sekta ya michezo, utamaduni na historia ili zisaidie kikamilifu katika kukuza sekta ya utalii. Kazi hiyo inatekelezwa kupitia program ya maendeleo ya utamaduni, utalii na michezo kama nilivyoeleza katika hotuba yangu.

Wizara yangu itaendelea kushajihisha sekta binafsi kuweka bei maalum ya huduma wanazozitoa kwa wananchi, pia Wizara kwa kushirikiana na kampuni ya kuandaa misafara ya watalii yaani *Tours Operator* itaendelea kutekeleza program ya kuwapeleka wananchi ikiwemo mwanafunzi katika maeneo ya

utalii kwa lengo la kuhamasisha jamii kushiriki utalii wa ndani. Vile vile tutayaeleza masuala na madhumuni ya mapango ijapokuwa sisi tunakwenda mara nyingi huko kwa shughuli nyengine. Lakini nataka niwaeleze wazi kwamba mfumo wa ukusanyaji wa takwimu za utalii hauridhishwi na unahitaji kuimarishwa. Ahsante sana Mhe. Dimwa kwa maoni yako tumelikubali tutaendelea kuimarisha ni kweli lipo tatizo la upatikanaji wa takwimu sahihi za watalii linajulikana, kwa sababu vyanzo vya ukusanyaji wa takwimu hii ni vingi sana. Kwa hivyo takwimu zinapogongana zinakuwa zina hitilafu.

Hata hivyo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tayari imeunda kikosi kazi yaani *Task Force* kwa ajili ya kulitafutia ufumbuzi suala hilo. Pia Mhe. Dimwa uliomba kuzidisha juhudi za ukusanyaji wa mapato. Wizara inaendelea na jitihada za kukusanya mapato mengi zaidi ili kuhakikisha kwamba kazi hiyo inafanyika vizuri.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub alikuwa na suala moja zito akasema kwamba kama Kamisheni kupangiwa kukusanya kiwango kikubwa hicho cha fedha mwaka wa fedha, tunasema sawa tumelipoke hilo lakini tunataka tumthibitishie kwamba hiyo ni changamoto na sisi tumekubali kuwa ni changamoto tutaifanyia kazi, tutatizama matokeo yake kadri hatua zinavyoendelea, vyanzo vipo tutatumia vyanzo hivyo tutajitahidi kwa jitihada zake tuhakikishe kwamba mapato hayapenyi wala hayavuji na kuweza kuyakusanya yote kwa pamoja. Hapo tutakapofikia mwisho wa mwaka tutaweza kumueleza kwamba idadi hii ni kubwa au ni ndogo kwa mujibu wa ilivyopangwa.

Mhe. Suleiman Sarahan bado aliuliza sekta ya utalii inaendelezwaje ili kuondoa utalii wa msimu. Miongoni mwa malengo makuu ya Wizara yangu ni kuifanya Zanzibar kuwa kituo kinachotoa huduma za utalii kwa mwaka mizima. Lengo hili litafikiwa kwa kuongeza vivutio vya utalii ikiwemo matamasha na michezo kama vile *Marathon* tunapanga sana kuzirejesha, tunapanga sana kurejesha michezo mengine ambayo itafanyika wakati wa *low season* ili kuufanya utalii wetu uwe wa mwaka mzima.

Mhe. Suleiman Sarahan na yeye tena akaendelea kuuliza kiasi gani cha fedha kilichotumika kwa ada ya ushiriki wa Zanzibar kwa maonyesho ya Dubai, Ujerumani, faida gani inapatikana kwenda huko. Huku ndio kukuza utalii Mheshimiwa bila ya kwenda kutangaza wageni wetu hawajui huko kwamba kuna nini Zanzibar. Kwa hivyo faida kubwa inayopatikana tunapokwenda kutangaza ni kuongeza idadi ya wageni na idadi ya watalii kuja kwa wingi nchini petu. Lakini nataka nimjulishe jumla ya dola za Kimarekani 66 elfu zilitumika kwa ajili ya kulipia ada ya ushiriki kwa maonyesho ya *ATM* Dubai,

Dola 51 nako zilitumika kwa maonyesho ya *ITB Berlin* zilitumika dola elfu 15 miongoni mwa faida 66 yaani 51 na 15 *ATM* Dubai, 51 na 15 zilifanyika *ITB* Berlin, ujumla wake ni dola 66. Lakini miongoni mwa faida zinazopatikana kama nilivyosema mwanzo kwa ushiriki huo vile vile ni kuwawezesha wadau wa utalii wa Zanzibar kukutana na kufanya majadiliano ya kibiashara na ma-*agents* wa utalii wa kimataifa na baadae kuwezesha nchi yetu kutembelewa na watalii wengi zaidi hapa nchini.

Mhe. Suleiman Sarahan pamoja na masuala yako mengi sana uliuliza je Serikali inatoa msaada gani kwa wawekezaji wa utalii ili kuendeleza biashara zao. Sekta hutoa misamaha ya kodi na ushauri wa kitaalamu na huu ushauri wa kitaalamu ni *value* zaidi kushinda ile pesa yenyewe. Kwa sababu unapotoa utaalamu kama alivyouliza Mhe. Miraji Khamis Mussa kuwapa watu elimu kuwafundisha wakalijua jambo. Hiyo ni *investment* kubwa, ni hazina zaidi kulikoni kuwapa pesa ambayo itatoka leo, kesho itakawa imepotea. Vle vile Serikali huzihamasisha taasisi za fedha kuwapatia mikopo nafuu wawekezaji ili waendeleze bashara zao.

Mhe. Abdalla Ali Kombo namshukuru sana na Waziri wa Ardhi, Nishati, Majenzi kwa namna alivyoweza kutoa ufafanuzi wake wa hoja tatu. Lakini moja katika hoja yako kubwa ilikuwa kwenye utalii, Serikali kuangalia uwezekano wa kuweka kituo kimoja cha ulipaji wa kodi za utalii katika maeneo ya kuingia nchini. Ushauri wa kuanzisha kituo hicho kimoja cha ulipaji wa kodi ni mzuri umepokelewa na utafanyiwa kazi. Nakuahidi kwamba ushauri huu ni mzuri mazungumzo yanafanyika na taasisi husika ili tuweze kuwa na kituo kimoja cha kufanyia shughuli hizo.

Lakini vile vile ukauliza nyumba iliyokuwa inamilikiwa na Serikali inamilikiwa na nani. Suala hili limekuwa lina marejeo mara kwa mara Mhe. Abdalla Ali Kombo hii kiu inayotaka kukatwa ndani ya koo yako. Nataka kukwambia wazi kwamba Serikali inaendesha shughuli zake kwa mujibu wa taratibu, sheria na kanuni ziliopo. Kwa hvyo panapotokea suala kutoka hatua moja kwenda hatua nyengine Serikali hufuata zile sheria, kanuni na taratibu ziliopo. Nyumba unayoizungumza ni nyumba ya Serikali kama ilivyokwisha kujibiwa, hilo halina mashaka na nyumba ile kweli ilikuwa ni Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kupitia Shirika la Utalii wakati ule, lakini taratibu zote za Serikali zimefuatwa baada ya kuvunjwa shirika taratibu ni kuipeleka kule Wizara ya Fedha, kitengo cha uhakiki mali. Kwa hivyo inapopelekwa kule taratibu nyengine zinafuatwa ili kuweza kuhakikisha kwamba kipi kinaendelea.

Kwa hivyo kama kuna taratibu za mauzo kuna taratibu za kupewa mtu mwengine, kuna taratibu za maombi pale Wizara ya Fedha huwa inafuata zile taratibu na kuipeleka pale pahali ambapo inatakiwa. Kwa hivyo Mheshimiwa mimi naamini Serikali sisi tupo katika kuihamisha nyumba ile Wizara ya Fedha wapo katika kuipokea nyumba ile na taratibu zipo. Tunakuomba suala hili sasa hivi kulileta Barazani itakuwa ni kulizungumza hewani, lakini kupata vielelezo Wizara zetu tatu zina vielelezo vya kutosha, mimi mwenyewe nitakuchukua tukae pamoja na wewe nikuelekeze ili nikuoneshe vielelezo vilivyo, tutizame utaratibu uliopitwa uliofanyika, lakini hadi sasa hakuna utata kwenye nyumba hiyo. *(Makofi)*

Mhe. Nadir Abdul latif Yussuf, naye alitoa ushauri, ushauri wake mzuri tumeupokea juu ya kuchajiisha utalii halisi *Halal Toursim*, ushauri wa Kiislam. Lakini nashukuru sana kuna mahoteli mengi, ukienda sehemu za kusalia zipo vizuri, siku za kufunga wafanyakazi wanafunga na wale wanaokuja Kiislamu na wao wanapata huduma zao kwa kupitia Kiislamu. Kwa hivyo kuimarisha, ulinzi, usalama na usafi vile vile umechangia. Serikali inaendelea na jitihada za kuimarisha ulinzi na usalama na usafi.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi ulipongeza sana, tunapokea pongezi zako za dhati ulizotupa. Vile vile Mhe. Hussein Ibrahim Makungu na wewe ulitaka kutochanganya utalii na Dini. Suala hili tumelisikia, tumelipokea tunaelewa wazi shughuli zinazofanywa na Serikali juu ya kuchanganya Dini na shughuli nyengine ni athari kubwa sana. Kwa hivyo tunapokea ushauri wako na tutaufanyia kazi zaidi.

Kulikuwa vile vile suala la Mhe. Suleiman Sarahan Said ambalo ni suala la mwisho, kwa nini wengi wanaotokea Ulaya ya Mashariki na sio Dubai na Uingereza tulipofanyia *marketing*. Tumesema pale tunakwenda kufanya *marketing* Mhe. Suleiman Sarahan Said ni sehemu ya makutano tu ambayo tunabadilishana biashara.

Kule kuna mfano wa biashara *Business to Business, (B to B).* Kwa hivyo mnapofika pale mnafanya biashara, watalii, watembezaji watalii pamoja na watu wengine wanapata fursa ile kufika katika sehemu ile kujua, wapi pazuri wanaweza wakenda wakafanya utalii wao. Kwa hivyo unapokwenda sehemu kama ile unabahatika na wewe kupata wale watembeza wageni kuweza kukuletea pale.

Lakini vile vile kuna faida kubwa sana ya kuweza kuzungumza na mashirika ya ndege, makampuni ambayo yana mahoteli na wengi wanaofanya biashara za

utalii. Kwa hivyo sio lazima mgeni anayekutikana pale tulipokwenda kutangaza utalii ndio aje nchini kwetu. Mgeni kutoka Ujerumani anaweza akenda kwenye maonesho yaliyokuweko Uingereza na huko yeye akaja akashawishi watu Ujerumani ili waje Zanzibar. *(Makofi)*

Hivi ndio walivyoshawishika watu wa Ukrain na watu wa Mashariki ya mbali kule. Kwa hivyo na wao hivi sasa, ndio maana wanaonekana wanakuja kwa wingi. Lakini nashukuru sana na kulipongeza Shirika la Ndege la Turkish kwa jitihada zao zao wanazozifanya, kuendelea kutusaidia Zanzibar kutangaza utalii wetu hususan Uingereza ambao hivi sasa umeenea kote. *(Makofi)*

Mwisho Mhe. Naibu Spika, nataka kuingia katika hoja za michezo, hoja za utamaduni kwa wingi sana zimejibiwa na Mhe. Naibu Waziri. Nataka nikiri tu kwamba Mhe. Ali Suleiman Ali Mwenyeketi uliuliza vyema juu ya suala hili la utamaduni na suala la BAKIZA, ukusanyaji wa mapato kama nilivyolieleza mwanzo, lakini Mhe. Hidaya Ali Makame na kikundi chako na shukurani zako tumezipokea.

Mhe. Omar Seif Abeid kama lilivyojibiwa suala lile. Mhe. Riziki Pembe Juma na wewe umetoa mchango mzuri juu ya kueneza Kiswahili na lugha zake, vile vile, Mhe. Ali Salum Haji na wewe pia umeeleza katika suala hili na Mhe. Ali Suleiman Ali ukaeleza upungufu wa mapato katika sekta ya utamaduni, yale yote yaliyotolewa ilikuwa mwingi ni ushauri na sisi tumeupokea ushauri huo, pongezi tumezipokea pongezi na tunawaahidi kwamba hatutolewa na pongezi. Tutaendelea kufanya kazi na kuitumikia Serikali ili tuwape huduma wananchi wapate zile huduma ambazo wanazitarajia. Suala ambalo halikujibiwa ni la Mhe. Omar Seif Abeid juu ya wanafunzi wanaosoma nyumba ya sanaa kutokuwa na vyeti. Utaratibu unafanywa kama kuna makosa kama hayo na tunawaomba sana Waheshimiwa waweze kutoa hoja kama hizo. Mhe. Naibu Spika, waendelele sana kutuuliza masuala yale yaliyojificha, ili na sisi tuyasimamie kufanya kazi ipatikane tija kwa jamii yetu.

Suala la Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf, suala la Mhe. Hidaya Ali Makame nimejibiwa sana na Mhe. Naibu Waziri. Mhe. Hidaya uliuliza juu ya pango la Tazari. Je, tuna taarifa nalo. Mhe. Hidaya nimependa sana mchango wako ambao umetutolea safari hii. Lakini pamoja na mchango wako nataka nikujuulishe kwamba taarifa ya mapango yote, si hili tu tunayo ndani ya Wizara yetu. Tunayo kwa njia zote, tunayo kwa njia ya kutukuza utamaduni lakini vile vile tunayo kwa njia zile tunapokuwa na matatizo yetu, pia mara moja moja huenda kule tukaomba kusaidiwa. Kwa hivyo tunajua na hili pango la Tazari lina umuhimu wake. Ni pekee ambapo tumeona Wizara imeshatuma

ujumbe kwenda kulikagua pango hilo na lina umuhimu gani la kufanyiwa utafiti wa akialojia, ambapo pengine tunatarajia sisi Wizara kutatoka matokeo mazuri ya kuwepo kwa maisha ya watu ndani ya pango. Tuna imani kwamba mle ndani ya pango hata sauti huwa zinatoka.

Mhe. Naibu Spika, namshukuru sana Mhe. Balozi Seif Ali Iddi alitunasihi sana juu ya kuyafufua haya mapango na tuweze kuyaelezea historia zake na jinsi yanavyotumika.

Mwisho kabisa uliuliza suala la pango la Miza wa Miza, Kizimkazi, nalo tunalisema kwamba kimsingi pango hilo la Miza wa Miza ni eneo linalotambulikana vizuri, lakini nataka nikuthibitishie tu tatizo lililokuwepo kwamba pango hili liko kienyeji zaidi. Ndio maana asilimia ya mapato yanakwenda mikononi kwa wenyeji, tunataka tufanye jitihada ya kulisajili Kitaifa na Mataifa ili liingie katika urithi wa kale. *(Makofi).*

Mhe. Mtumwa Peya Yussuf nakushukuru sana na wewe kwa suala la Mangapwani linashughulikiwa kiasi gani. Eneo hili la Mangapwani linashughulikiwa kwa kiasi kikubwa ili liweze kuongeza mapato, zaidi kwa Serikali, tayari limeshapimwa na sasa yanatafutiwa hati miliki baadhi yake yamewekewa uzio kwa ajili ya kuhifadhi zaidi.

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye hoja nzito kabisa, nimalizie hoja za upande wa sekta ya michezo. Mhe. Ali Suleiman Ali, Mhe. Abdalla Maulidi Diwani, Mhe. Jaku Hashim Ayoub suala hili namshukuru sana Mhe. Naibu Waziri amelijibu kwa ufasaha, jibu ambalo limetoa mapokeo ya ushauri wenu alilolitoa. Vile vile tunataka tuwathibitishie zaidi Waheshimiwa waliochangia katika kuona inasimamia wizara yetu inasimamia migogoro inayojitokeza kwa *ZFA* na Baraza la Michezo, *ZFA* kwa viongozi, *ZFA* na Mahakama, suala hili tumelipunguza kwa kiasi kikubwa na tutaendelea kulipunguza mpaka niondoke kabisa.

Lakini Mhe. Abdalla Maulid Diwani bado alikuwa na suala kwa nini ruzuku ya Baraza la Michezo imepungua kutoka milioni 84,000,000 kitakwimu hadi 70,900,000. Ninataka kukudhibitishia wazi kwamba wizara imeongeza fedha zaidi ya ushiriki baada ya kutizama vizuri nilivyoandika hotuba na bajeti inaonesha wazi kwamba, timu katika bajeti yetu Idara ya Michezo na Utamaduni na vile vile, katika ujenzi wa viwanja vya michezo, bajeti ya Idara ya Michezo kwa mwaka huu imekuwa ni milioni 270,000,000 badala ya 164,000,000 kwa ujumla wake. Kwa hivyo kipengele hiki kuna kazi zimefanyika, kuna kazi hazihitajiki tena kuendelea kuingiza katika bajeti, ndio

maana ukaona kuna kitu kama hiki. Lakini kwa ujumla fedha zilizoingizwa katika fungu hili unaloliona zimezidi kutoka 164,000,000 hadi 270,000,000.

Waheshimiwa kwa pamoja Mhe. Ali Suleiman Ali, Mhe. Jaku Hashim Ayoub, Mhe. Suleiman Sarahan Said, Mhe. Hussein Ibrahim Makungu, Mhe. Omar Seif Abeid, Mhe. Mohamed Said Mohammed Said, Mhe. Shaib Said Ali na Mhe. Yussuf Hassan Iddi walitaka kujua Wizara kuchukua juhudi ya kufuatilia utekelezaji wa maagizo ya *CAF*, pongezi kwa Zanzibar kupata uwanachama *CAF*, Zanzibar wajipange katika kutekeleza maagizo ya *CAF, ZFA* kukaa pamoja na Kamati ya Mpira wa Miguu na kuacha mambo ya ubinafsi.

Silijibu hapa Mhe. Miraji Khamis Mussa suala lako na Mhe. Ali Salum Haji, nitalijibu wakati nitakapojibu majibu yenu kwa ujumla wake. Lakini nataka niwathibitishie hawa wote Waheshimiwa Wajumbe walioiuliza kwamba Wizara imepokea pongezi kwa zile pongezi, na Waheshimiwa na wachangiaji kuhusu Zanzibar kupata uwanachama wa *CAF* pongezi hizo tunazipokea na tunawathibitishia tutafanya jitihada zaidi, Serikali iendelee kututuma ili kupata uwanachama wa *FIFA*, tujimwange na nje zaidi ya dunia zaidi ya hapa tulipopata. *(Makofi).*

Mhe. Naibu Spika, lakini nataka niwathibitishie wazi kwamba mpaka sasa tayari *ZFA* wameshaanza kuandaa *Technical Development Plan* ambayo inakwenda sambamba na *CAF*. Tunahakikisha kwamba *ZFA* itafuata masharti yote ya *CAF* na wachezaji wetu wa mipira watafuata masharti ya *CAF* na waamuzi wetu watabidi waachane na mambo yao ya kuhongwa hogwa na kuchukua vile vitu wakatuharibia mpira wetu, waendelee kufuata masharti ya *CAF*. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, na utakapokamilika utaratibu wetu pamoja na sheria zetu, tutauwasilisha kwa wadau mbali mbali wa mipira mkiwemo nyinyi Waheshimiwa ili kutoa maoni yenu, namna gani mnaweza tukakamilisha suala hilo. (*Makofi*).

Mhe. Abdalla Maulidi Diwani, suala lako la wizara kuingia suala la utitiri wa vilalu limejibiwa vizuri na Mhe. Naibu Waziri, ukauliza tena kuandaa mpango maalum kupunguza timu za vikosi vya SMZ. Timu kila zikiwa nyingi ni mtihani, tunaelewa wazi. Lakini suala la kupunguza timu za Vikosi na kuangalia zaidi timu za mitaani zenye ushabiki mkubwa ni suala gumu kidogo, linahitaji angalizo kubwa kwani Sera ya Michezo ya Zanzibar inatilia mkazo maendeleo ya michezo kwa kujumuisha na timu za aina mbali mbali, ikiwemo Mashirika, Vikosi, Vyuo na kadhalika.

Kwa hivyo kadri tunapokuwa na vitu vingi kama hivi, ushindani unakuwa mkubwa na timu ya taifa inakuwa na upeo katika kuchagua wachezaji wenye vipaji. Kwa hivyo ni taratibu ambazo zinaweza zikapangwa kwenye timu zao, wanaweza wa-*merge* wakapata timu moja ikawa ya kweli kweli, lakini vile vile wanaweza wakawa na timu tofauti tofauti.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani uliuliza masuala mengi sana kusimamia viongozi na wana michezo, kuheshimu Sheria na Kanuni za michezo hasa mpira wa miguu. Ninakuhakikishia kwamba Baraza linasimamia hilo na linajitahidi katika kusimamia hilo, kama kutakuwa na mapungufu tunayapokea na tutayafanyia kazi. Lakini nguvu zinatiliwa zaidi kwa suala la kuheshimu Sheria na Kanuni za michezo husika ikiwemo *ZFA.*

Mhe. Naibu Spika, inawezekana suala hili likamgusa Mhe. Ali Salum Haji (Mnadhim), sheria zinaposimamiwa ipasavyo inawezekana zikaleta madhara kama hivi. Nilikuwa na taarifa kutoka *ZFA* kwamba tumemuita yule mwanamichezo wetu mahiri, aende katika vikao, amepangiwa vikao zaidi ya vitano hajaenda. Taarifa zile zinawezekana kuwa zina ukweli kuzizungumza huku, zina ukweli kuzizungumza huku. Lakini sisi kama wizara tuta-*balance* taarifa hizo na hatua tutazichukua na matokeo juu ya tukio lililotokea, kama alivyolieleza. Mhe. Ali Salum Haji basi litapatiwa ufumbuzi wake.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani, Mhe. Suleiman Sarahan Saidi umeuliza kuhusu kuwa kipimo cha kupimia wachezaji wetu wanaoshiriki mashindano ya ndani na nje, kuhusu utumiaji wa madawa ya kulevya. Mhe. Naibu Spika, mimi napenda sana, napenda hata hicho kipimo cha kutumia madawa ya kulevya kiwe karibu na Baraza la Wawakilishi ili tukiingia humu, wale waliokaa nao usiku nao wabakie bado hawapo.

Mhe. Naibu Spika, nimefurahi sana na suala hili na Mhe. Suleiman Sarahan Said (Jembe) na nipongeza sana jitihada za mchango wake huu alioutoa kwa kutaka kuwalinda vijana wetu, hasa wachezaji wa mpira wa miguu. Inafaa sana Mhe. Suleiman ushauri wako tumeupokea na tutaufanyia kazi na mimi nakukubalia, ni aibu kwa mchezaji wetu kutoka hapa akenda kushiriki *CAF*, kesho akaambiwa yule anatumia madawa, hii ni aibu kubwa sana. *(Makofi).*

Kwa hivyo kuanza mapema kutangulia kuwa na vyombo hapa, tukawa na vitu vya kuwapima ni ushauri mzuri, tumeupokea kwa nguvu zote na tutahakikisha kwamba tunalisimamia. Vyombo vya michezo viwe vinawapima wachezaji wetu kabla hawajafika kwenye shughuli zao zile za Kimataifa. Nakushukuru tena Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo kwa kulijibu suala

la Wizara kwa Mhe. Hussein Ibrahim Makungu kuwa wizara iwahamasishe vijana na wazee kushiriki katika mazoezi na michezo ili kujenga afya zao.

Waheshimiwa nataka nichukue fursa hii, kuwaomba Waheshimiwa wote wa Baraza la Wawakilishi kila tarehe moja ya mwaka unaoingia tunashiriki katika mazoezi wote bila ya kujali mkubwa, mdogo, mzee, sote huwa tunashiriki mazoezi na Mhe. Abdalla Maulid Diwani ni mmoja katika viongozi wazuri wanaoshajihisha katika suala hili. Kwa hivyo tunaomba na sisi tushiriki kama ilivyopendekezwa na Mhe. Hussein Ibrahim Makungu.(*Makofi*).

Lakini Mhe. Sira Ubwa Mamboya kwa ushauri wako umepokewa. Mhe. Mohammed Said Mohammed umesema wizara imejipanga vipi kuzisaidia timu zetu, kushiriki mashindano mbali mbali ya kimataifa. Kama nilivyoeleza katika bajeti tumeonesha fungu ambalo tunaliomba, wizara imetenga bajeti hiyo kupitia Idara ya Michezo na Utamaduni ili kuwezesha timu zetu kushiriki mashindano mbali mbali ya kimataifa.

Nataka niwaambie wazi tu, mategemeo yetu kwa *ZFA* ni kuendelea kuwa na utaratibu mzuri, pale tutakapopata uwanachama wa *FIFA*, tutakapopata uwanachama wa *CAF*, tunaamini tutakuwa na Ofisi zetu, tutakuwa na pato la kutosha na timu zetu zinaweza zikashiriki vizuri mashindano ya kimataifa.

Mhe. Mohammed Said Mohammed wizara ijipange kuziandaa timu yetu ya taifa ya mpira wa miguu. Mimi nasema na timu nyenginezo. Katika suala hili Wizara itashirikiana vyema na Vyama husika kufanikisha hilo. SMZ husaidia sana timu ya taifa kushiriki katika mashindano mbali mbali, na mashindano ya kimataifa ni lazima ishiriki na ndio maana inatoa bendera kule ukatambulikane unakokwenda kama alivyochangia Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil.

Mhe. Naibu Spika, ninashukuru sasa tunakokwenda ndani ya Afrika hata wimbo wetu wa Taifa utakuwa unapigwa na wimbo wetu hauna mbadala na wimbo mwengine. Mhe. Mohammed Said Mohammed umeendelea kuuliza suala kwamba Baraza la Michezo lina mpango gani katika kuimarisha michezo nchini. (*Makofi*).

Baraza tayari limeanza kuyapatia ufumbuzi matatizo ambayo ni kikwanzo kwa maendeleo ya michezo nchini, kama vile kuwapatia wana michezo viwanja, mafunzo ya utawala ya michezo, makocha na waamuzi pamoja na vifaa vyengine.

Vile vile umeuliza juu ya rasimu ile kufanya jitihada ya kuwafanya wana michezo wa mpira wa miguu kuwa wachezaji wa kulipwa. Rasimu ya Sera ya Michezo 2017 imelizingatia kwa kina hilo na mimi mwenyewe nimeipitia nimeona hilo na kulitia mkazo kuwa na wachezaji wa hiari na wa kulipwa. Ulitaka vile vile kujua kuundwa uongozi mwengine wa *ZFA* na kuwaondosha wale wanaoleta mazonge, siasa na ubadhirifu na kuweka *ZFA* mpya ili kuondoa utata na ugomvi. Haya mambo yote yanakwenda kwa mujibu wa sheria. Ninatumaini hata mimi leo siko tayari kwamba waletwe Wawakilishi wapya wengine humu kabla ya kufika 2020. Kwa hivyo na hili tusubiri muda wake utakapokwisha uongozi huo, taratibu za uchaguzi zitafanyika, taratibu za kisheria zitafanyika, sisi tunaokwenda kule tukapiga kura tuhakikishe tunapiga kura kama uongozi ule hatuutaki tuuondoe.

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini pamoja na kwamba umetoa michango mizuri, bado na wewe nakupongeza sana kwa ushauri wako. Umetoa ushauri juu ya kuwafungia viongozi wa michezo miaka kumi au maisha. Wizara imejipangaje pia kuiendeleza michezo ya ndani (*Indoor games)* ambayo imeshuka hadhi ikiwemo *table tennis* na *softball*. Ushauri tumeupokea kama nilivyokwambia Mheshimiwa, tumeupokea kwa nguvu zote, utafanyiwa kazi kwa mujibu wa sheria na kanuni.

Lakini vile vile Wizara imepokea ushauri wako mwengine katika ujenzi wa Uwanja wa *Mao Tse Tung* imezingatia suala hilo. Uwanja wa *Mao Tse Tung* kutakuwa kuna *Indoors*, kuna *football pitch* mbili na michezo mengine yote pale inaweza ikapatakana, tuombe tu Wachina watekeleze mradi wao kwa muda uliopangwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub pongezi zako tumezipokea. Mhe. Suleiman Sarahan Said pongezi nazo tumezipokea lakini vile vile ukataka kujua kwa nini Uwanja wa Gombani pamoja na pongezi hizo haufanywi kibiashara na kutangazwa. Tumelipokea shauri hilo kama kuna taratibu za kuzifanyia biashara pale maduka na vitu vyengine, usiwe kuuvamia kama ulivyovamiwa na wapasua mbao, isiwe kuuvamia kama ulivyovamiwa na nyumba nyengine ambazo zimefanya pale ujenzi kimakosa. Tufanye kibiashara kwa kuhuwisha ule uwanja basi ushauri huo tumeupokea.

Mhe. Shaib Said Ali naye pia ametoa ushauri na ametaka kujua Uwanja wa Gombani kuwa na mipasuko pasuko. Wizara inakusudia kufanyia matangenezo madogo madogo, tayari tumeweka azimio hilo Uwanja wa Gombani na matengenezo yenyewe ni kuweka plasta mpya na kupaka rangi eneo la mbele na nje, vile vile kupaka rangi ndani ya uwanja. Kazi hii inatarajiwa kufanyika

kabla ya kumalizika mwaka huu wa fedha 2016/2017. Kwa hivyo mipasuko inayohatarisha mle wakati wowote inaweza ikaondoshwa.

Mhe. Suleiman Sarahan Said umetaka kujua kutofunguka kwa mageti ya uwanja wa Gombani. Milango ya mageti ilikuwa na kasoro ndogo ndogo ambazo kwa sasa nakuhakikishia kwamba yameshafanyiwa kazi. Lakini mimi nitakuja kuwa wa kwanza kuja kufuatana na wewe, tukenda pale tukazingatia ipi ambayo haijafanyiwa kazi ili iweze kufanyiwa kazi ipasavyo.

Mhe. Suleiman Sarahan Said vile vile taarifa kuhusu gharama kamili ya ujenzi wa uwanja ya Mao Tse Tung kwamba haijulikani. Sambamba na suala la Mhe. Miraji Khamis Mussa, upande wa uhisani na lini utakamilika na wizara imejiandaa vipi kuhusu kufanya ukaguzi wa uwanja huo hatua kwa hatua.

Mhe. Naibu Spika, ninataka niwathibitishie kwamba hadi sasa jumla ya shilingi bilioni mbili, mia nne na sita, mia tisa na ishirini na tano zimeshatumika kwa ajili ya ujenzi wa kiwanja cha Mao Tse Tung. Mradi huu unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwaka 2018, kuwa *complete* kabisa, Kitengo cha Ufuatiliaji na Tathmini cha Wizara kitakuwa kikifanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa mradi huo kila baada ya kipindi fulani.

Baada ya kuona mchango ule umetokea, tumekwenda kuzitafuta gharama zilizotumika ni hizo. Ahsante sana Mhe. Miraji Khamis Mussa na Mhe. Suleiman Sarahan kwa umakini wenu.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri umebakisha dakika tano.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii na Michezo: Ahsante katika kumalizia dakika tano hizo naomba nimalizie karatasi yangu inavyonionyesha kila mmoja nitamaliza kwa dakika moja.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana, Mhe. Yussuf Hassan Iddi, Mhe. Omar Seif Abeid, Mhe. Nassor Salim Ali, pongezi zenu kwa pamoja tumezipokea. Mhe. Nassor Ali Salim alikuwa ana suala la kutaka kujua sababu gani zilizopelekea ujenzi wa Uwanja wa Mao Tse Tung kutoanza kwa wakati uliopangwa.

Mhe. Naibu Spika, nataka kumjulisha kwamba hali hii ilitokana na kuchelewa kufika kwa vifaa vya awali kwa ajili ya maandalizi ya ujenzi huo ikiwemo nyumba za dharura za wajenzi. Lakini kuanza kwa ujenzi usisubiri ukaliona leo kuta limefikia pale, hakuna aliyekuwa si shahidi, uwanja mzima

umezunguushiwa matofali, uwanja mzima pale tayari zimeanza kumwagwa kokoto, Wachina tayari wameweka mabanda yao ambayo yatawafanyia kazi na vifaa vingi vimeonekana kufika pale. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, na kwa upande wa Matumbaku tumeeleza wazi kwamba wamejenga zile nyumba zao, vifaa vingi sana vimo mle. Tunawaomba wananchi, wawape ushirikiano wale, tuwaambie sana wananchi wetu wawe makini. Tuna taarifa kwamba wananchi wetu hunyemelea sehemu kama zile kwenda kuiba vile vifaa vya Wachina. Lakini ninawaomba sana Waheshimiwa Wawakilishi ambao tunawasimamia wananchi wetu, tuwe makini hususan watu wa jimbo la aina lilokuwepo pale, tusije kupata aibu ambayo hatuitegemei.

Mhe. Naibu Spika, kulikuwa kuna masuala muhimu ya Mhe. Mohammed Said Mohammed alilouliza kwa ajili ya viwanja kwa michezo ya Wilaya na viwanja vyengine vingi vilivyoulizwa kwa sababu ya Wilaya. Nataka kusema wazi kwamba waliyouliza masuala haya akiwemo na Mhe. Miraji Khamis Mussa na Mhe. Ali Salum Ali.

Mhe. Naibu Spika, Viwanja vya Wilaya ni sera ya serikali kuvikamilisha. Viwanja vile kwa kila Wilaya ni utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015/2020. Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo haitamuangusha Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kupanga sera halafu isitekelezeke. Tunawahakikishia kwamba na tunashukuru sana pamoja na matangazo uliyoyatoa, naamini kule juu leo wapo wafadhili ambao wanahamu ya kujenga viwaja hivi vya Wilaya, fedha wanazo, wako tayari kuja kufanya kitu hicho. Ingawaje Mhe. Miraji Khamis Mussa kataka sana kiwanja kimoja kijengwe kwake, jitihada hizo tutazitizama na namna gani tuone tutazikamilisha. Lakini suala la kujenga viwanja vya Wilaya vitakamilika.(*Makofi*).

Mhe. Suleiman Ali uliuliza ujenzi wa viwanja vya Wilaya kama nilivyojibu, migogoro ya BTMZ nimejibu kama nilivyosema.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa ujali muda.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii na Michezo: Mwisho kabisa nataka kutoa pongezi za dhati Mhe. Ahmada Ahsante sana.

Pamoja na hayo yote Mhe. Miraji Khamis Mussa na Mhe. Ali Salim Hako na wale wote waliochangia mwisho, naomba majibu haya niliyokuwa nayo yaingie kwenye *Hansard* lakini na zile pongezi walizozitoa tumezipokea na ule

ushauri waliotupa tunawambia tutaufanyia kazi. Lakini tunawangoja kwenye buti ikiwa kutakuwa na buti basi masuala yale waka-*raise* Mheshimiwa tutakuwa tayari kuyajibu na tuko makini kuyajibu masuala hayo.

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika kwa kuwasilisha. Natumai Wajumbe wote tumewapatia majibu yao. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika: Toa hoja Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii na Michezo: Mhe. Naibu Spika, baada ya kueleza hayo yote na kutoa ufafanuzi juu ya michango ya Wajumbe, naomba kutoa hoja.(*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe hoja imetolewa na Mhe. Waziri, wale wanaokubaliana na hoja wanyooshe mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

Mhe. Waziri Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

(Hoja imetolewa iamuliwe)

(Hoja imeamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe kabla ya kuendelea kwa kuwa muda wetu uliobakia ni mdogo na tunataka kuingia katika vifungu, ningemuomba sana Mhe. Mwanasheria Mkuu atutengulie Kanuni ya Muda ili tuweze hata kama itakuwa muda umeshapindukia tutaweza kuendelea na kumaliza vifungu vya Wizara hii.

Mhe. Mwanasheria Mkuu karibu.

KUTENGA KANDO KANUNI 23(4) KUHUSIANA NA MUDA

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Naibu Spika, kabla ya hatujaingia kwenye Kamati na kupitia kifungu kwa kifungu, naomba nitoe hoja ya kutenga kando Kanuni ya Muda ambayo ni kanuni ya 23(4) ili tutenge kando Kanuni hiyo na tujadili hoja hii mpaka hapo bajeti hii itakapopitishwa na Baraza.

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe hoja imetolewa ya kutengua muda, wale wanaokubaliana na hoja hiyo wanyooshe mikono. Wanaokubali wameshinda.

Mhe. Waziri Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

(Hoja imetolewa iamuliwe)

(Hoja imeamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii na Michezo: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa Baraza limejadili na kuikubali hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Habari, Utalii na Michezo, sasa naomba Baraza lako Tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili kuvipitisha vifungu vya Matumizi vya Wizara yangu.

Ahsante Mhe. Naibu Spika.

KAMATI YA MATUMIZI

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe utaratibu wetu ambao tutautumia leo ni ule ule ambao tumeutumia katika kupitisha bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria. Kwa hivyo ningewaomba sana Waheshimiwa Wawakilishi kwa kuwa tunapita katika fungu kubwa, kwa hivyo kila mmoja ajue katika lile fungu kifungu anachotaka kupiga buti kinatokana na fungu gani kubwa na hapo unaweza kuhoji.

FUNGU J01 - WIZARA HABARI, UTALII, UTAMADUNI NA MICHEZO

Fungu J01 Wizara ya Habari, Utalii na Utamaduni na Michezo 468,303,000
Fungu J01 Wizara ya Habari, Utalii na Utamaduni na Michezo
Jumla ya Fungu **17,807,832,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Kifungu PJ0101 Programu Kuu ya Maendeleo ya Habari na Utangazaji

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa muongozo wako kwenye fungu hilo kubwa chini ukishuka kuna kifungu cha upatikanaji

wa habari, usambazaji na dogo lake ni usambazaji wa maudhui, ndiyo nilipo mimi.

Naomba Mhe. Waziri katika majibu yake nilimuuliza katika ile *capital investment*, serikali ilitoa kiasi gani na marejesho yake zimeanza kupatikana kiasi gani. Lakini pia nikamuuliza, hakunijibu hata moja, kwa utaratibu gani unaotumika hichi Kitengo cha Maudhui kuwepo kwenye Wizara, kisiwepo kwenye taasisi husika. Naomba majibu Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kama nilivyoeleza hapo mwanzo kwamba kwanza nasikitika sana kuona kwamba nimekosa muda wa kumjibu kwa ufasaha Mhe. Miraji Khamis Mussa, lakini nikaomba sana majibu yale yaingie katika *hansard*.

Kama tulivyoeleza kwamba mradi huu wa *ZMUX* ameuliza kuhusu kifungu cha Usimamizi wa Vyombo vya Habari na Utangazaji. Naomba arudie tena suala lake.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, naomba tufuate ule muongozo wako kwamba fungu kubwa lililosomwa ni la Maendeleo ya Habari na Utangazaji, lakini dogo ni utapatikanaji wa usambazaji wa habari.

Chini yake katika kifungu (h), (j) 0101 inamalizia 05 ni usambazaji wa maudhui ya utangazaji, ndio panapo *ZMUX* na ndiyo ninayoiulizia mimi. Suala langu lipo kama ifuatavyo.

Katika kuchangia nilitaka kujua ile *capital investment* iliyopewa hii *ZMUX* kuna marejesho, ni kiasi gani cha marejesho kimerejeshwa toka kupatiwa mtaji huu. Lakini nikauliza pia utaratibu gani unaotumika kwa hili suala liratibiwe na Wizara pasi na kwenda kuratibiwa na taasisi husika, kwa maana nakusudia *ZBC*, sijapata jibu hata moja.

Ndiyo suala langu lilipo.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba kutokana na suala lake marejesho tuliyoyapata kupitia kurusha maudhui ni shilingi mia tatu na saba milioni.

Lakini vile vile nataka nimthibitishie kwamba Kitengo cha *ZMUX* bado kipo chini ya Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo na nilimjibu wakati ule kwamba hapo baadae tunangoja ushauri wa Mhe. Mwanasheria Mkuu ili

tuelewe kwamba tutaifanya kuwa ni Kampuni katika Kampuni za Serikali au itabakia kwamba ni moja kwa moja ndani ya *ZBC*.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa kuendeleza hoja yangu hii.

Kwanza ninachosikitika sana kwa mujibu wa Mhe. Waziri maelezo yake mpaka *ZMUX* inatiliwa pesa serikali haijajua kama ni Kampuni au Idara, na sisi tunataka kujua na Mwanasheria Mkuu yupo na taasisi hii wameianzisha Serikali, mpaka wanaitilia pesa *method* gani iliyotumika ili kuonekana pesa hizi zinaingizwa pahala fulani bila ya kujua ni taasisi au ni kampuni.

Mhe. Mwenyekiti, nataka majibu.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nataka nimuhakikishie Mhe. Miraji kwamba serikali tunapopanga mipango hii huwa tunatumia mipango maalum. Katika kupanga mipango hii tunajua wazi kwamba katika mgawanyo wa habari ni wazi kwamba tumeona hatuwezi kuchanganisha kati ya shughuli za utayarishaji wa vipindi na urushaji wa maudhui. Kote huko ambako hawakufanikiwa basi walichanganisha vitu hivi. Sisi kwa sababu tulitafuta wataalamu kuja kufanya *study* maalumu. Makampuni zaidi ya matatu wote wametushauri kwamba ni vyema mkawa na taratibu za kuwa vitu hivi viko tofauti.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kwa hatua tulizokuwa nazo hazijakamilika. Ni matarajio ya Wizara kwamba kabla ya kumalizika bajeti hii tutalifanikisha suala hilo na hatutegemei kwamba majibu kutoka kwa Mwanasheria Mkuu yatakuwa ni marefu kiasi kufanya hivyo. Kwa sababu hiki ni kifungu kidogo cha huduma endapo itakubalika kufanyiwa kuwa ni kampuni, kwa hivyo ndio maana tukaona tutangulize bajeti hii hapa kama ilivyo, lakini itaonekana pengine inafaa kurudia kule kule, kwa hivyo fungu hili litasomeka kama ni fungu la *ZBC* la litajumuisha katika fungu kuu.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, bado nina masikitiko yangu Waziri hanijibu ninachomuuliza. Tulikuwa tunauliza kwa sababu serikali imetoa ile *capital investment* imepeleka kwenye Idara, imepeleka kwenye Kampuni, hakunijibu hata moja lakini tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Tunaendelea, tuendelee. Mhe. Suleiman Makame Ali.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Mhe. Mwenyekiti, sina lengo la kumkwaza rafiki yangu kwa sababu nilitoka kwenye Wizara yake kupitia Kamati.

Nilipokuwa nikichangia nilizungumza kwamba Zanzibar ni miongoni mwa Jamhuri ya Muungano, lakini leo *ZBC* haionekani kwenye ving'amuzi vya Azam mpaka ulipie. Sasa nikitaka hapa Mhe. Waziri anipe jibu kwamba ni lini *ZBC* itaweza kuonekana kwenye king'amuzi za Azam bila ya malipo kama inavyoonekana *TBC* na ukitazama Zanzibar nayo ni Jamhuri ya Muungano.

Mhe. Mwenyekiti: Najua umejibu hilo suala lakini naomba utoe majibu kwa ufupi.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utam na Michezo: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, napenda kumjibu Mhe. Suleiman suala lake kwamba ni kweli hii ya Jamhuri ya Muungano na itabakia kuwa Jamhuri ya Muungano na Muungano hautovunjika kwa siku mbili hizi tutaendelea kuwa nao. (*Makofi*).

Nataka nimthibitishie kwamba hili ni suala la kibiashara baina ya *ZBC* na Azam. Lakini nataka nimthibitishie tena kwamba *ZBC 11* ambayo pia ni *ZBC* moja kwa moja inaonekana kwenye king'amuzi cha Azam.

Kwa hivyo kama kulikuwa kuna taratibu hazijakamilika za kuifanya *ZBC 1* au *ZBC III*, kwa sasa hivi tuna *channels* mpaka nane zote zitakuwa ni *ZBC*. Kwa hivyo kama kulikuwa kuna taratibu tumesema kwamba tunapitia tena yale masuala ya mikataba ambayo tupo pamoja, kuna mambo mengine tunaweza tukayarekebisha na hiyo *ZBC* ikaonekana bila ya kuwa na hitilafu yoyote kupitia Azam. Ahsante sana.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, na mimi niende kwenye kifungu (h), (j) 010101 urushaji na vipindi. Nilipokuwa nikichangia nilizungumza azma yangu ya Zanzibar ni nchi kati ya nchi za Afrika zilizoingia katika *digital*. Mpaka sasa Zanzibar tunakwenda kwenye mpango wa *analogue*. Ni lini serikali imefanya mpango wa kudumu wa kuzima *analogue* tukaingia kwenye *digital* mpaka sasa hatujapata kuona.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mohammed Said Mohammed suala lake kwamba hivi sasa tulipo televisheni ile pale anayoiyona iko *half digital* au ipo *more than half digital*, lakini vile vile ipo kwenye *analogue*. Hatujakamilisha mpango wa kuizima *total* kutoka *analogue* kuingia *digital*, taratibu zote hivi sasa zimekamilika, tunasubiri tu serikali lini inaweza ikatupa tarehe rasmi ya

kuweza kusema sasa tunazima *digital completely*. Tunachokizingatia Mhe. Mwenyekiti, wananchi wetu ndio wanaopaswa kuona zile huduma za televisheni yetu ya *ZBC*.

Mhe. Mwenyekiti, hususan ukizingatia unyonge wa wananchi wetu. Kwa hivyo tupo katika kuhakikisha kwamba tutakapozima mitambo ya *analogue completely* hatutofika kuwa na wananchi ambao wanalalamika hawaioni *ZBC*.

Lakini wakati wowote kwenye mwezi wa Mei tunaweza tuka *completely* kuzima hiyo *analogue*. Ahsante sana.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, nimemfahamu sana Mhe. Waziri alipokuwa akisema nina *Hansard* mkononi kwangu ambayo mwaka jana alinijibu neno kama hilo na niko tayari kumpa *Hansard* ni maneno yake na maneno yangu, lakini nilikuwa nataka *commitment* ya Serikali ni lini tutafanywa hivyo.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi nakumbuka kweli hata mwaka jana tulivutana kwa kutaka *commitment*, lakini siwezi kumwambia lini tunaweza tukafanya kitu hichi kwamba kesho au keshokutwa au tarehe nne. Ninataka nimuhakikishe tu hivi karibuni wakati wowote tunaweza tukasema kwamba leo ni siku ya kuweza kuzima *analogue*.

Mhe. Mjumbe namuomba sana awe na uvumilivu ataona hali ya kuwa imekamilika ile *digital*, ahsante sana.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru lakini nimshukuru sana na Mhe. Waziri kuwa wananchi wameelewa kuwa hakuna *commitment* tuendelee.

Kifungu PJ0101 Maendeleo ya Habari na Utangazaji 4,814,166,000
Kifungu PJ0102

Mhe. Mwenyekiti: Ataanza Mhe. Suleiman Sarahani Said na atafuatia Mhe. Abdalla Maulid Diwani na nimekuona Mhe. Panya Ali Abdalla.

Mhe. Suleiman Sarahani Said: Nashukuru Mhe. Mwenyekiti, na mimi nitaanza na SJ020I "Uimarishaji wa Utamaduni na maeneo ya kihisitoria", lakini pia nitakwenda na SJ0202 "Uendelezaji wa Raslimali Watu katika utalii na Ukuzaji wa Michezo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nimwambie Mhe. Waziri nimesikia sana na Mhe. Naibu Waziri walipokuwa wakijibu katika hoja ya maendeleo ya historia, lakini sikuwahi kusikia kwamba kuna historia nyingi ambazo bado hazijajulikana kuwekwa katika vitabu vyetu, sikumsikia Waziri amejipangaje kuhusu kuziibua hizi historia, sikuwahi kuimsikia Waziri. Kwa hivyo ningemjuomba Waziri kwa yale maeneo yaliyokuwa hayajaibuliwa ananiambiaje au analiambiaje Baraza.

Lakini suala la pili Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa namsikiliza sana lakini sikuwahi kuutaja mchezo wa ng'ombe ambao ni *official* mchezo wetu wa Zanzibar, ambao nilimwambia kwamba mchezo huu ana kikundi gani ambacho cha mchezo wa ng'ombe ameweza kukitayarisha kama Wizara ya Habari, sikuwahi kumsikia kwa sababu sikuwahi kumsikia akitaja Kirumbizi kwa sababu mchezo ule unaendana na Kirumbizi.

Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, napenda kumjibu Mhe. Suleiman Sarahan Said ambaye alikuwa na michango mingi sana katika kuchangia kwake.

Ninataka nimueleze kwamba hatuwezi kuikamilisha historia yote siku moja ikawa tumeikamilisha, lakini bado jitihada za Wizara kuhakikisha kila historia ambayo inayotakiwa kuwekwa katika kumbukumbu, inawekwa katika kumbukumbu na jitihada hizo tunaziendeleza. Kwa hivyo kama yako mambo ambayo yeye anayaona kwamba wakati huu yanatakiwa kufanyiwa kazi hiyo, sisi tuko tayari kushirikia naye na tukaweza kuyafanyia kazi pamoja na yale ambayo yeye pale moja kwa moja hayaoni.

Na ndiyo maana juzi wakati tunamchangia Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, tukawa wawazi kuhakikisha kwamba mambo mengine yanabakia kwenye historia na yanapaswa kubakia kwenye historia na tukalazimika historia zile kuzinunua kwa gharama yoyote lakini zibakie katika kumbukumbu zetu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, lakini vile vile nimjibu suala lake juu ya mchezo wa Ng'ombe. Kwanza nataka nimhakikishe Mheshimiwa kwamba sherehe zote za mapinduzi zinazofanyika hapa, mchezo wa ng'ombe unafanywa, zote na Wizara imeweka katika kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015/2020 kuhakikisha inaibua hii michezo ya zamani yote inafanyika kama vile ilivyokuwa ikifanywa zamani.

Lakini zuri zaidi tayari tumepata maombi kupitia *ZIPA* na Wizarani kwetu kwamba kuna kikundi ambacho kinafanya kazi zake Pemba na kiko tayari kuibua michezo yote hii ikiwemo resi za ngalawa, uchezaji wa msewe, mchezo wa ng'ombe na kipole pia atakuwepo huko Mheshimiwa asiwe na wasi wasi.

Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Suleiman Sarahani Said, tunaendelea Mhe. Abdalla Maulid Diwani.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nimesimama kwa kifungu SJ010202.

Katika mchango wangu nilizungumzia Vyama vya Michezo na nilizungumzia W*eight Lifting Association Zanzibar,* kwa kudai kwamba kile chama ni chama kikongwe, kimesajiliwa katika mashirika yote ya kimataifa kutoka Afrika mpaka dunia. Lakini kina ukata wa upewaji wa ruzuku kutoka Serikalini.

Nikamuomba sana Mhe. Waziri aje kuniambia ni lini jambo hili ambalo nasubiri na hivi sasa wana deni la $4000 ambazo zinatakiwa zilipwe katika Afrika $2000 na katika dunia $2000. Je, Mhe. Waziri katika majumuisho yake hajalizungumza hili, kasema tu wamesaidia michezo hivi na hivi.

Mhe. Mwenyekiti, nataka anipe jibu ni lini wale watu watapata ruzuku yao ili waweze kulipa ile ada za kimataifa.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Abdalla Maulid Diwani lakini vile vile kwa mchango wake kupata kuwatanabahisha na wananchi wote ambao wanatusikiliza.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nakubali kwamba jitihada za Chama cha *Weight Lifting* hiki kupata uwanachama tunashukuru sana kwamba ni cha kwanza kupata uwanachama nje ya Zanzibar. Lakini hii inaungana na jitihata tulizozifanya hivi karibuni kwa Chama cha Mpira wa Miguu *ZFA* nacho kupata uwanachama kwa pale kupitia *CAF*.

Kwa pamoja tunataka kumakikishia Mhe. Abdalla Maulid Diwani tutakaa nao pamoja ili kutizama namna deni hili linavyopaswa kulipwa, kwa pale mchango unaotuhusu sisi basi tunahakikisha tutashirikiana nao ili tuweze kuhakikisha kwamba tunawasaidia mchazngo huo.

Lakini vile vile katika kuhakikisha kwamba hiki chama nacho kinakuzwa pamoja na vyama vyengine, bajeti yetu inaeleza namna gani kupitia BMTZ tumeomba ile bajeti na itakavyosaidia vyama vyote vinavyopata ushiriki wa kimataifa namna gani tunaweza tukawasaidia.

Kwa hivyo hawa kama ilikuwa hawana utaratibu huo, tunawaomba tu sasa hivi waje BMTZ, mambo huenda yakabadilika na mambo yanabadilika siku hadi siku, kwa hivyo tutashirikiana pamoja katika kuhakikisha tunaondoa kadhia hii.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, Mwalimu Rashid ni mwalimu wangu, namfahamu sana akisema ijapokukwa anasema Kiuroa kidogo.

Sasa mimi suala langu lilikuwa ni lini kwa sababu, yeye kwenda BMTZ imekuwa sasa hivi tatizo. Mashirikiano BMTZ na hivi vyama vimekuwa tatizo. Mimi ni shahidi kwa hayo kwa sababu nakumbana nayo, kila muda. Hapa utapata majibu mazuri lakini watendaji wake katika kwenye zile taasisi hawatupi majibu kama haya ambayo anayozungumza Mhe. Waziri.

Mhe. Mwnyekiti, ili nisimkamate sana Mhe. Waziri naomba awe shahidi mimi nioke na watu wa *Weight Lifting* nianze kwenye Ofisi yake, anitupe *purposely* nende katika BMTZ kulitatua hili tatizo la kupata $4000 ili tuone kwamba hatutoki katika uwanachama ule.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, natumaini kuwa milango ya Wizara wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo iko wazi. Kwa hivyo Mhe. Abdalla Maulid Diwani yeye na hiyo timu yake aje tutakaa, tutajadiliana na tuone namna gani tunaweza tukalitatua suala hili. *(Makofi)*

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi nichukue fursa hii kwanza kumshukuru Mhe. Waziri kwa juhudi kubwa ambazo anazichukua lakini mimi nilitaka katika kifungu hichi ambacho kinasema kuna, "Uendelezaji na Ukuzaji wa Shughuli za Utamaduni", na mimi ndio suala zima linalonikereketa katika moyo.

Mhe. Mwenyekiti, nilitaka kujua kwa sababu miongoni mwa mila na utamaduni wa Mzanzibari ni kivazi chenye heshima ambacho ni mara nyingi, ni muda mwingi tulikuwa tunaililia Sheria hii iletwe kwa sababu ipo lakini ni

ya muda mrefu ambayo kwa sasa ina mapungufu inataka iletwe hapa irekebishwe.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, nilitaka kujua ni lini Mhe. Waziri ataweza kushirikiana na Mwanasheria Mkuu waweze kutuletea Sheria hii tuweze kuipitisha ili utamaduni wa Mzanzibari usizidi kutoweka. .

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, nitoe pongezi za dhati kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein. (Makofi).

Ninataka nimuhakikishe Mhe. Mwakilishi wangu hapa Bi. Panya kwamba Mhe. Rais tayari kishaelekeza namna gani ya kuzipitia sheria zote ambazo tunaona zina mapungufu, na agizo hilo lipo ndani ya Wizara yetu na hiyo sheria aliyoiona nayo ina mapungufu nayo hiyo ni moja katika sheria zilizotolewa Mwananasheria Mkuu kwa kila Wizara.

Kwa hivyo mimi namuhakikishia kwamba kwa kushirikana na wanasheria wetu wa Wizara na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, zile sheria tunazifanyia kazi na tuzipeleke zile sheria ambazo zina mapungufu, zinazohitajika kufutwa za muda mrefu tutazifuta na tunazohitaji kabisa kuzifanyia marekebisho Waheshimiwa wapo tutawaletea, siwezi kuwaahidi tu kuwaambia kwamba kesho sheria itatengezwa. Kwa sababu sheria inatizama na mambo gani muhimu ambayo ya kuyadhibiti.

Mhe. Mwenyekiti, lakini utaratibu huo upo na ninamshukuru sana Mhe. Panya Ali Abdalla na ninakushukuru sana kwa mchangio wako au pengine nilikusahau pale wakati ule wa kukujibu.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mhe. Rais wetu kwa kuona mapungufu ya sheria na kwa kuwa Mhe. Waziri ameshatuahidi sheria zenye mapungufu zitaletwa ili kuweze kulinda mila na utamaduni wa nchi hii.

Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Kifungu PJ0102 Maendeleo ya Utamaduni, Utalii na Michezo
Jumla ya Kifungu 2,733,006,000

Kifungu PJ0103 Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Habari,
Utalii na Michezo 10,260,660,000
Jumla Kuu **17,807,832,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU J02 - KAMISHENI YA UTALII

Mhe. Mwenyekiti: Bado Mheshimiwa.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Ninajua ninachokifanya hivyo.

Mhe. Mwenyekiti: Hapana bado Mheshimiwa. Zima kipaza sauti chako.

Kifungu J02 - Kamisheni ya Utalii 4,000,000,000

Mhe. MohammedSaid Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nazungumza kuhusu makusanyo ya Wizara hii hapa, nimeona tuna kazi kubwa ambazo tumefanya kwenye utalii lakini bado makusanyo haya ya bilioni nne nayaona ni madogo mno. Na kwa sababu hiyo tuna sehemu nyingi ambazo tunataka kuziongezea kama kwenye maabara, nataka tuseme tu makusanyo haya ni madogo na Serikali ijue hapa tutafanya mbinu gani ya kuyaongeza ima mapato ya Shs.4,000,000,000 ni madogo sana.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa napendekeza yaongezwe angalau yafikie Shs. 5,000,000,000.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa imani yako Mhe. Mohammed Said Mohammed ya kupenda Serakali iwe na mapato mengi ili iendeleze shughuli zake za kila siku zaidi.

Lakini nataka nikuhakikishie tu dhamira nzuri ya Serikali mwaka huu ni si kuongeza kodi ya aina yoyote, sikuweza kuwakandamiza wananchi katika kulipa mapato na mimi mwenyewe nina elimu chache kidogo katika ukusanyaji wa mapato. Makasio haya yamepangwa kutokana na vianzio vyake vilivyo, *source* kubwa angalie tu kwamba kiwango kilichowekwa mwaka jana na kiwango kilichowekwa mwaka huu, vianzio ni vile vile, hakuna kulichopandishwa bei, hakuna kilichoongezeka basi nahisi kwamba kwa hayo

mapato yaliyokisiwa acha twende nayo, tujaribu kukusanya, sisi pengine imani yetu tunaweza tukayafikia, tunaweza tusiyafikie.

Mhe. Mwenyekiti, lakini suala la kuongeza natumai Serikali imekuwa makini sana katika kuangaza hili na hapa mpaka kufikia idadi hii ya makusanyo, pamoja na ustadi wangu wote huu, najua haya yanakwenda na vyanzo na Serikali imeweka kwa mujibu wa vyanzo vyake.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, nimemuelewa sana Mhe. Waziri lakini nilikuwa nataka kujua, hakuna kodi ambayo imeongezwa lakini tuna mtiririko mzima wa utalii kuongezeka, na huku mbele tutakuja kuzidisha kifungu cha kutangaza utalii wetu. Sasa nataka vile vyanzo, ni vyanzo gani vimebuniwa ili basi tuone mapato haya yameongezeka baadae tumpe yeye kutumia huku mbele.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nimpe faida ndogo tu Mhe. Mohammed Said Mohammed na kwa niaba ya Wajumbe wengine ni kwamba mtalii anapoingia analipa mapato ya aina nyingi sana. Na mapato hayo si lazima yote yakusanywe na Kamisheni ya Utalii, kuna mapato yanaweza yakakusanywa kupitia *ZRB*, kuna mapato yanaweza kukusanywa kupitia Halmashauri na kuna mapato yanaweza kukusanywa kupitia Uhamiaji, lakini vyote hivyo vinakusanywa kipitia utalii.

Mhe. Mwenyekiti, kikubwa kilichokuwepo hapa ni kwamba Kamisheni ya Utalii ina vianzio vyake vikuu viwili. Ni *permit* na leseni za mahoteli. Hakuna hoteli liloongezeka jipya lilojengwa hapa, hakuna *permit* za magari mapya yenye idadi kubwa ya kuongezwa kiasi hicho yaliyoongezeka hapa, wala yeye hatujawahi kusikia kwamba ameomba kiwanja labda ataweka *Five Stars* za kuweza kutusaidia kama mapato hayo yaongezeke.

Kwa hivyo Mhe. Mjumbe naomba sana awe mtulivu wa kujua kwamba makisio haya ni kwa ajili ya vile vianzio viliopo. Na kwa mtazamo mdogo ingependezesha labda tuseme ikakuwa nusu tu ya miradi tuliyokuwa nayo hapa ya utalii basi mapato yaliyowekwa mwaka jana yasingefikia kiasi hicho, yangekuwa bado yamo katika *level* hii ambayo tunatakiwa tuikubali.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo Mhe. Mjumbe vyanzo vyetu sisi kama Kamisheni ya Utalii na vilivyopangiwa kukusanyiwa hapa ni zile *permit* anazoziona *tour operator* zikienda zake huko, vibali vile vya watembeza

wageni wanavyovaa begi zile, na bei zake ndio hizo hizo elfu moja, elfu mbili, elfu tano. Bei kubwa zinapatikana kwenye leseni zenye mahoteli na zile leseni zenye mahoteli nazo pia zinakusanywa kutegemea na *season* zenyewe na wingi wa wageni wanaoingia mule katika mahoteli.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.(*Makofi*).

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, nimemfahamu sana Mhe. Waziri anapozunguza jambo hilo, lakini bado ni hoja yangu ya tatu sina nia ya kulikamata fungu hili, bado tunao muda mzuri sana wa kuhifadhi na kudhibiti mapato yanayotokana na utalii tukawaongezea wengine ili tukaongeza katika vifungu vyengine, tuendelee.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba nimjulishe Mhe. Mohammed Said Mohammed kwamba haya ni makadirio, ni *estimate* hazifungi tukikusanya zaidi ya hapo zinapokelewa. *(Makofi)*

Kwa hivyo haya ni makadirio), nakubaliana naye kwamba tuweke *measures* za kuongeza makusanyo na hilo litafanyika kama alivyosema Mhe. Waziri. Mwaka jana tulikuwa na bilioni mbili (2,000,000,000), mwaka huu tumeweka bilioni nne (4,000,000,000), lakini makadirio hiyo sio *ceiling.* Tunaweza tukakusanya mpaka bilioni tano (5,000,000,000) na kama uwezo huo utakuwepo mwakani tutakipandisha kima cha makusanyo kwa Kamisheni. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti: Fungu limekubalika.

Wajumbe: Ndio

FUNGU J02 - KAMISHENI YA UTALII

Kifungu PJ0201

Mhe. Mwenyekiti: Naanza na Mhe. Omar atafuatwa na Mhe. Suleiman na baadae Mhe. Miraji.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa na mimi nafasi ya kuuliza.

Wakati nilipokuwa ninachangia nilizungumzia habari ya utalii, kuna mpango wa *Islamic Tourism* ambapo kwa sasa nchi nyingi za Kiarabu zinaufurahia sana, na kwa sababu katika hotuba yao walieleza kwamba wana mpango wa kuzidi kuitangaza Zanzibar kwenye nchi za Ulaya na nchi za Kiarabu.

Sasa mimi nilitaka kujua huu mpango wa *Islamic Tourism* ambao upo kwa sasa na unawavutia watu wengi, wizara ina mpango gani wa kuutangaza mpango huu ili tukaweza kuingiza watalii wengi kutoka nchi za Kiarabu na nchi zile za Kiislamu ambazo zina ufurahia. Kwa sababu mpango huu kwenye mahoteli kuna sehemu za ibada, familia wanakwenda kule wanakaa wanapumzika ambapo sasa hivi ulimwenguni unaanza kuenea kwa kasi.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, bado niendelee kumpongeza Mhe. Mwakilishi kwa mchango wake na yeye anataka kujua tu namna gani tunaweza tukapanga mpango wa *Islamic Tourism*.

Kama tulivyosema tunajua hatari ya dini kuiweka moja kwa moja ndio kipaumbele ya jambo lilivyo. Tumeona mataifa mengi yanavyopata migogoro lakini inabidi tuwe waangalifu sana katika kufikia hatua hii ya kuwa na *Islamic Tourism.* Tunaweza tukaja tukajihisi kwamba tunataka kwenda mbele, tukaja tukatolewa kabisa kwa ulimwengu wa kuonekana tunazalisha mambo mengine ambayo yaliyokuwa sio. Kwa hivyo kutokana na sera zetu za nchi ilivyo, Zanzibar yetu kama mnavyosema haina dini, wananchi wake kila mmoja ana dini vizuri na anaabudu kwa mujibu wa uhuru aliokuwa nao.

Hivyo, mpango huo kwa sasa hivi tunahisi kwamba tuuchukue, tuufanyie kazi mpaka tuone namna gani tunaweza tukafikia katika kuungiza katika *market* ya kuweza kuutangaza. Lakini tunapokwenda kutangaza nchi za Uarabuni, ahakikishe tu kwamba Uarabuni inatembelewa na watu wengi kutoka mataifa tofauti duniani kote.

Kwa hivyo wale wananchi wanaotembea Uarabuni, vivutio vilivyowapeleka kule kwenda Uarabuni na sisi ndio tunavyovitizama kama ni vigezo vya kuwavutia kuja kwetu Zanzibar. Kwa hivyo tutaendelea kuutangaza ndani ya nchi za Uarabuni na nchi nyenginezo ili kuwafuata wale wageni zile sehemu ambazo wapo na wanapenda kufanya utalii.

Kwa hivyo kwa sasa hivi naona ingali mapema sana kabisa kuanza kuwaanzisha *Islamic Tourism*, lakini wazo lake tunalichukua.

Mhe. Omar Seif Abeid: Tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi nashukuru kwa kunipa nafasi hii.

Mhe. Mwenyekiti, katika utangazaji na uhamasishaji wa utalii ikiwemo na Makumbusho, watalii wanatoka sehemu mbali mbali wanakwenda katika makumbusho. Nilipokuwa nikichangia hapa nilisema kwamba kule Mkamandume Pemba limebakia lile jina na ile ardhi ya pale Mkamandume. Lakini ule uhalisia wa Mkamandume wa lile jengo na maeneo mengine hayapo tena yanatoweka kila siku.

Vile vile pia nikazungumzia kuhusu Makumbusho ya Mkumbuu kwenye kaburi la Mwana Mwari na nyumba iliyoko chini ya bahari Mkomani.

Je, nataka Mhe. Waziri anijibu hapa kwenye suala hili magofu ya Mkumbuu bajeti iliyopita niliyazungumzia kwamba yanachukuliwa na bahari kila leo, nikitaka kujua kwamba ana mpango gani kwenye bajeti hii kuhakikisha kwamba magofu yale anayanusuru ili yasichukuliwe na bahari kwa kuyapigia ukuta.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri kwa maelekezo tu kwamba utajibu suala moja la Mhe. Suleiman Makame Ali kwa sababu tayari kuna na mchangiaji mwengine wa tatu, unatakiwa kujibu suala moja na mwengine ambaye ameshauliza mwanzo umeshamjibu. Kwa hivyo Mhe. Suleiman kwake ni suala moja tu la kumjibu.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi suala lake kuhusu uhamasishaji wa utalii juu ya Makumbusho, lile jengine nitaliacha kama ulivyotoa maelekezo.

Lakini nataka kumwambia wazi Mhe. Suleiman kwamba hata tutapofanya matengenezo hatuwezi kwenda nayo yote yale kwa pamoja ndani ya bajeti ya mwaka huu mmoja hatutoweza kutengeneza Makumbusho yote. Hivi sasa tutizame tuna athari kubwa ya kumbusho letu la Beit-el-Ajaib na ndio kumbusho linaloingiza mapato mengi sana hapa Zanzibar. Linaingiza takriban kwa sasa kwa mwezi milioni 18 Makumbusho ya pale.

Sasa Makumbusho mengine kama haya yaliyoanguka kabisa ya Mkamandume, Mkumbuu na kwengine yanataka utaratibu, yanataka kufanyiwa utafiti, yanatakiwa kufanyiwa na mambo mengine ambayo yanajuulikana yaanze wapi na yamalizikie wapi. Kwa hivyo bado katika bajeti hii hatukulipa bajeti wala fungu hili suala la Mkamandume, lakini bado tunajua kwamba lipo na lina umuhimu na litafanyiwa kazi.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nimemfahamu vizuri Mhe. Waziri kwamba kwenye bajeti hii hawezi kufanya yote, lakini hii ni bajeti ya pili tangu tuanze Baraza hili ni bajeti ile 2016/2017 na hii 2017/2018.

Sasa nilitaka kujua tu kwamba ile bajeti iliyopita wapi walitengeneza na sasa hivi kujua hii bajeti tunayokwendea wanatengeneza wapi hilo tu ndio nilikuwa nataka kujua.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, katika jibu langu mama nafikiri nimeeleza sehemu zile ambazo tumefanyia matengenezo zikiwemo Kijichi, zikiwemo kuweka uzio, tumefahamisha sehemu zilizoko Wilaya ya Kati na sehemu nyingi nyenginezo ambazo kwa mujibu wa ile bajeti tuliyoipanga tulipotekeleza uwasilishaji wa utekelezaji wa bajeti tumeweza kueleza.

Lakini mapenda kumwambia Mhe. Suleiman Makame Ali awe mvumilivu kwamba hii ni bajeti ya kila mwaka na katika kutekeleza hii Ilani wetu ya miaka mitano. Kwa hivyo asakheri *inshaallah* tunaweza tukafika bajeti si lazima mwaka huu hata mwakani tunaweza tukatekeleza yale masuala mengine ambayo ameyapa kipaumbele.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nimeridhika na majibu ya Mhe. Waziri isipokuwa namuomba tu kwamba afanye ziara kwenye majengo haya ya Makumbushe ayaangalie hali yake ilivyo ili apate kujua zaidi,

Mhe. Mwenyekiti, tuendele.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, katika mchangio wangu kwenye eneo hasa hii la Utangazaji na Uhamasishaji wa Utalii,

programu ndogo kuitangaza Zanzibar ndani na nje ya nchi. Kuna kituo nilikichangia ambacho kiko India na nikamwambia Mhe. Waziri hata ule mkataba ambao tunakwenda nao katika uendelezaji wa kituo hiki ume-*expire* na haujapitiwa na kuna pesa tumezitenga hapa.

Sasa nilikuwa nataka Mhe. Waziri kwanza akiri anaelewa ku-*expire* kwa mkataba huo? Lakini la pili fedha hizi kama ile Bodi ya Kamisheni kupitia Makamishna hawakuridhia. Kama hawakuridhia maana yake kuendelea na kituo hiki...

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Miraji Khamis Mussa ni suala moja tu unatakiwa uulize. Kwa hivyo jipange uliza suala moja tu.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Hili ninalouliza sasa ni suala kwa sababu naulizia kuhusu pesa.

Mhe. Mwenyekiti: La pili ndio lifanye suala lako moja. Suala moja tu.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Haya Mhe. Waziri naomba kukuuliza kwa sababu umeomba tukuidhinishe pesa ya kuitangaza Zanzibar ndani na nje, na kuna kituo nilisema kimeshamaliza mkataba wake na kama Bodi haikuridhia, pesa hizi utazi-*allocate* wapi au maeneo gani mengine ambayo tukikupitishia tutaweza kuzitumia basi nilikuwa nataka ufafanuzi huo.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, mimi ningependa sana Mhe. Miraji Khamis Mussa akaridhika kwamba pesa hizi tumezipanga kwamba zitatumika kwa makusudio yaliyopangwa, na nataka nimuhakikishie kwamba alilioliuliza tunalielewa juu ya kumalizika kwa ule mkataba. Mkataba ule ni kwa ajili ya mwaka huu wa fedha unaokwisha 2016/2017 na tuna mipango ya kuhakikisha kwamba kituo kile tunaendelea nacho na bajeti hii inahitajika ili kuweza kutumia huduma zile zilizopangwa kule.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru sana Mhe. Waziri kwa maelezo yake ya kina aliyonipa na naomba tuendelee najua jitahada zitaendelea.

Kifungu PJ0201 Utangazaji na Uhamasishaji wa Utalii 425,293,000

Kifungu PJ0201	Uendeshaji na Uratibu wa Kamisheni ya Utalii	1,152,507,000
	Jumla Kuu	**1,577,800,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

(Baraza lilirudia)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa kabla ya kumuita Waziri naomba niwatambulishe wageni wetu, ni wageni wa Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo, Mhe. Rashid Ali Juma. Hawa ni wafadhili wa viwanja vya michezo kutoka Afrika ya Kusini wenye asili ya Kitanzania. Wageni wenyewe ni Bwana Shaaban Juma Haji na Bwana Haroun V. Mohamed. Karibuni sana. *(Makofi).*

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha Makadirio ya Fedha ya Wizara yangu bila ya mabadiliko, sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza liyakubali makadirio hayo.

Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe Mhe. Waziri ametoa hoja wale wanaokubaliana na hija hiyo wanyooshe mikono, wale wanaokataa, wanaokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, nichukue fursa hii kwanza kabisa kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na Naibu wake na watendaji wote wa wizara kwa kazi nzuri ambayo wameifanya katika hotuba yao, lakini pamoja na kujibu hoja za Waheshimiwa. (*Makofi*).

Ni matarajio yetu kwamba yale ambayo yote ambayo uliyoyasema utayafanya basi utayafanya na matokeo yake tutakuja kuyaona katika taarifa za utekelezaji za wizara. (*Makofi*).

Baada ya kusema hayo waheshimiwa naahirisha kikao chetu hadi saa 11:00 jioni leo hii.

(Saa 6:53 mchana Kikao kiliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2017/18 - Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto

Utaratibu

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Kanuni ya 72 inayosomeka kwamba: "Kiwango cha vikao vyote vya Baraza kutakuwa na nusu ya Wajumbe wote..", inaendelea. Wajumbe hatujatimia nusu tunahitaji muongozo wako.

Mhe. Mwenyekiti: Ulipokuwa unasoma utaratibu Serikali ipo na wajumbe wameshaongezeka kwa hivyo tunaendelea.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima naomba kutoa hoja kwa Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili liweze kupokea, kujadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya njema na uzima. Pia, napenda kumpongeza kwa dhati Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein, kwa uongozi wake mahiri, thabiti na makini katika kuleta maendeleo ya nchi na ustawi wa wananchi wake. Sote ni mashahidi

kuwa, mnamo mwezi Aprili, 2017 ametimiza ahadi yake aliyoitoa ya kuongeza mara mbili mishahara kwa watendaji wa serikali.

Kwa niaba ya watendaji wote tunamshukuru sana na tunamuomba Mwenyezi Mungu azidi kumjaalia afya njema, uadilifu, maarifa na hekima katika kuiongoza nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kumpongeza tena Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein, kwa kuanzisha Operesheni Maalum ya kupambana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji dhidi ya Wanawake na Watoto vinavyoendelea na kukithiri katika jamii yetu siku hadi siku. Naomba nitowe wito kwa jamii kutolifumbia macho tatizo hili.

Aidha, namshukuru Makamu wa Pili wa Rais, Mhe. Balozi Seif Ali Iddi kwa kushirikiana na Mhe. Rais katika kuhakikisha nchi yetu ina amani, upendo na wananchi wapo katika hali nzuri kimaisha.

Napenda pia kumshukuru Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi, Mhe Abdul-hamid Yahya Mzee kwa utendaji wake mahiri wa kulitumikia taifa hili.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile napenda kukupongeza wewe binafsi na Baraza lako kwa mashirikiano mnayotupatia katika kufanikisha shughuli za wizara. Aidha, naishukuru Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii ya Baraza la Wawakilishi chini ya Mwenyekiti wake Mahiri, Shupavu na Msikivu Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata), kwa mashirikiano mazuri, busara na michango wanayotupatia katika kufanikisha shughuli za wizara wakiwemo na wajumbe wafuatao:

Wajumbe wa Kamati ni Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma, Makamo Mwenyekiti na Mjumbe wa Viti Maalum Vijana kutoka Mkoa wa Kusini Unguja. Mhe. Hassan Khamis Hafidh, Mhe. Maryam Thani Juma, Mhe. Jaku Hashim Ayoub, Mhe Mussa Foum Mussa na Mhe. Zainab Abdalla Salum. Pia shukurani ziende kwa Ndugu Himid Haji Choko na Haji Jecha Salum makatibu wa kamati na Ndugu Amina Abeid Hemed mkalimani.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii adhimu kuwapa pole wale wote waliofikwa na maafa katika kipindi hiki cha mvua na upepo mkali, Mwenyezi Mungu atawajaalia faraja na kuwaondolea matatizo yote yanayowakabili. Pia, nawapa pole wananchi wa Arusha kwa Msiba

uliowapata wa kuondokewa na watoto wao wapendwa wa Shule ya Lucy Vincent katika ajali ya gari iliyotokea tarehe 6 Mei, 2017. Namuomba Mungu awalaze Mahala Pema Peponi na awape subirá na faraja wazazi wao. Naomba nichukue nafasi hii pia kuwapa pole wale wote waliodhalilishwa katika mazingira mbali mbali katika kipindi chote hiki cha mwaka huu tulichoanza, Mwenyezi Mungu aendelee kuwajaalia na serikali itaendelea kuhakikisha kwamba hamtadhalilishwa tena.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sasa nitoe maelezo mafupi ya mapato, matumizi na utekelezaji wa Programu za Wizara kwa mwaka wa fedha 2016/2017, pamoja na Mwelekeo, Vipaumbele, Programu na Makadirio ya Bajeti kwa mwaka wa fedha 2017/2018

MUHTASARI WA MATUMIZI NA MAPATO KWA MWAKA 2016/2017

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto kwa mwaka wa fedha 2016/2017 iliingiziwa jumla ya Shilingi Bilioni Kumi na Mbili, Milioni Mia Moja na Nne, Laki Nne na Sitini Elfu (Tsh. 12,104,460,000/=). Kati ya hizo, Shilingi Milioni Mia Tano Ishirini na Saba, Laki Tano na Elfu Arobaini (Tsh. 527,540,000/=) ni kwa ajili ya kutekeleza Programu ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi; Shilingi Milioni Mia Nne Tisini na Elfu Tisini (Tsh. 490,090,000/=) kwa ajili ya kutekeleza Programu ya Kukuza Usawa wa Kijinsia na Uendelezaji wa Wanawake; Shilingi Bilioni Tano, Milioni Mia Nne na Kumi, Laki Nne na Arobaini Elfu (Tsh.5,410,440,000/=) kwa ajili ya kutekeleza Programu ya Kuimarisha Huduma za Ustawi; Shilingi Bilioni Tano, Milioni Mia Tano Arobaini na Saba, Laki Moja Thamanini na Tisa Elfu (Tsh. 5,547,189,000/-) kwa ajili ya kutekeleza Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto na Shilingi Milioni Mia Moja, Ishirini na Tisa, Laki Mbili na Elfu Moja (Tsh. 129,201,000/=) ni kwa ajili ya utekelezaji wa Programu ya Usimamizi wa Sheria za Kazi, Ukaguzi wa Kazi na Kazi za Staha kwa wote.

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi Aprili, 2017 fedha zote zilizotolewa ni Shilingi Bilioni Tisa, Milioni Mia Saba Hamsini na Mbili, Laki Sita Ishirini na Moja Elfu, Mia Saba Tisini na Tatu (Tsh. 9,752,621,793/-), ambayo ni sawa na asilimia Sabini na Tano (75%) ya utekelezaji wa Programu zote. Kati ya hizo Shilingi Milioni Sitini na Tatu, Laki Mbili na Ishirini na Tano Elfu Mia Sita na Hamsini (Tsh. 63,225,650/-) zilitumika

kwa ajili ya kutekeleza Programu ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ambayo ni sawa na asilimia Kumi na Mbili (12%) ya fedha kwa programu hiyo.
Shilingi Milioni Mia Nne na Sabini na Tano, Laki Nane Tisini na Nne Elfu na Sitini na Sita (Tsh.475,894,066/-) zilitumika kwa kutekeleza Programu ya Kukuza Usawa wa Kijinsia na Kuwaendeleza Wanawake ambayo ni sawa na asilimia Tisini na Saba (97%) ya fedha kwa Programu hiyo.

Shilingi Bilioni Tatu, Milioni Mia Sita na Hamsini na Mbili, Laki Nne na Sabini Elfu na Mia Mbili (Tsh.3,652,470,200/-) zimetumika kwa ajili ya kutekeleza Programu ya Kuimarisha Huduma za Ustawi ambayo ni sawa na asilimia Sitini na Nane (68%). Jumla ya Shilingi Bilioni Tano, Milioni Mia Nne Sabini na Tisa, Laki Tano Sabini na Moja Elfu, Mia Nane Sabini na Saba (Tsh.5,479,571,877/-) zilitumika kwa kutekeleza Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto sawa na asilimia Thamanini na Tano (85%) ya fedha za Programu hiyo.

Jumla ya Shilingi Milioni Thamanini na Moja Laki Nne na Sitini Elfu (Tsh.81,460,000/-) zilitumika katika kutekeleza Programu ya Usimamizi wa Sheria za Kazi, Ukaguzi wa Kazi na Kazi za Staha kwa wote, sawa na asilimia Sitini na tatu (63%) ya fedha kwa programu hiyo. (Angalia Kiambatanisho namba 1).

MAPATO KWA MWAKA 2016/2017

Mhe. Mwenyekiti, wizara ilitarajiwa kukusanya kiasi cha Shilingi Milioni Mia Nne Thamanini na Saba na Laki Nne (Tsh. 487,400,000/-) kupitia Ada ya Usajili na Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika, Ada ya Ukaguzi wa Mikataba ya Ajira ya nje ya Nchi, Ada ya Ukaguzi wa Maeneo ya Kazi na Vibali vya Kazi.

Mhe. Mwenyekiti, hadi Mwezi Aprili, 2017 wizara kupitia Kamisheni ya Kazi, Idara ya Ajira, Idara ya Usalama na Afya Kazini na Idara ya Ushirika ilikusanya jumla ya Shilingi Milioni Mia Nne Ishirini na Moja, Laki Tatu Arobaini na Nne na Mia Mbili (Tsh. 421,344,200/-), kutokana na Ada za Usajili na Ada ya Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika na Vibali vya Kazi ambavyo ni sawa na asilimia Thamanini na Sita (86%) ya Makadirio ya Makusanyo (Angalia Kiambatanisho namba 2).

UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA WIZARA KWA MWAKA 2016/2017

Mhe. Mwenyekiti, wizara kwa mwaka wa fedha 2016/2017 imetekeleza Programu zifuatazo:

Programu Kuu ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

Mhe. Mwenyekiti, programu hii inalenga kuinua hali za wananchi kiuchumi kwa kuwapatia mikopo nafuu, kujenga uwezo wa ujasiriamali na kuwaunganisha na Vyama vya Ushirika.

Programu Ndogo ya Mfuko wa Uwezeshaji

Mhe. Mwenyekiti, programu hii ina lengo la kutoa mitaji na huduma nyingine za kifedha zenye masharti nafuu kwa wananchi wenye kipato kidogo kutoka maeneo yote ya Unguja na Pemba, ili waweze kujiajiri na kupunguza umaskini. Wizara kwa kupitia programu hii kwa mwaka wa fedha 2016/2017 imefanikiwa kutekeleza yafuatayo:

- Imetoa mikopo 341 (Unguja 232 na Pemba 109) yenye thamani ya Shilingi Milioni Mia Sita (Tshs. 600,000,000/=). Mikopo hiyo iliwanufaisha wananchi 3,486 (wanawake 1,944 na wanaume 1,542) katika Shehia 143 za Unguja na Pemba. Asilimia 65 ya walionufaika ni vijana wenye umri kati ya miaka 18 - 35 na asilimia saba (7%) ya walionufaika ni makundi maalum ikiwemo watu wenye ulemavu 40 na vikundi 2 vya ushirika. (Angalia Kiambatanisho namba 3).

- Asilimia thalathini na tatu (33%) ya walionufaika na mikopo hiyo ni wakulima wa mboga mboga na matunda, asilimia thalathini (30%) ni wafanya biashara wa maduka ya vyakula ya jumla na rejareja, maduka ya nguo, viatu na mikoba, maduka ya vipodozi na wafanyabiashara wanaosafiri nje ya nchi kuleta bidhaa za aina mbali mbali hapa Zanzibar. Asilimia thalathini na saba (37%) ya wanufaikaji ni wafugaji na wenye viwanda vidogo vidogo.

- Imetoa mafunzo kwa wakopaji wapya 739 kuhusiana na usimamizi mzuri wa fedha na kufanya maamuzi sahihi ya fedha, mbinu za kubuni miradi mipya, utayarishaji wa mpango biashara, taratibu za kurudisha mikopo, utumaji na upokeaji wa fedha kwa njia za mitandao na kuweka

kumbukumbu za mahesabu ya biashara zao. Mafunzo haya yamepelekea kuongezeka kwa kiwango cha urejeshaji wa mikopo.

Hadi kufikia mwezi Aprili, 2017 jumla ya Shilingi Milioni Mia Tatu na Sabini, Laki Tatu na Elfu Ishirini na Tano (Tsh. 370,325,000/=) zimerejeshwa Unguja na Pemba. Kiwango hiki cha urejeshaji wa mikopo kimeongezeka kwa Shilingi Milioni Kumi na Moja, Laki Saba, Ishirini na Moja Elfu (Tsh. 11,721,000/=) ukilinganisha na kiwango kilichokusanywa mwaka jana cha Shilingi Miloni Mia Tatu Hamsini na Nane, Laki Sita Elfu Nne (Tsh.358,604,000), kwa kipindi cha (Julai 2015 hadi April 2016).

Kati ya marejesho hayo, Unguja zilikusanywa Shilingi Milioni Mia Mbili na Tisini na Tatu na Elfu Sabini na Nane (TSh. 293,078,000/=) na Pemba zilikusanywa Shilingi Milioni Sabini na Saba, Laki Mbili na Elfu Arubaini na Saba (TSh. Shs 77,247,000/=). Matarajio kwa mwaka ilikuwa tukusanye Shilingi Milioni Mia Tatu na Tisini (Tsh.390,000,0000/-). (Angalia Kiambatanisho namba 4)

- Imetunisha Mfuko kwa kuwekeza sehemu ya fedha Shilingi Milioni Mia Nane (Tsh.800,000,000/-) katika Benki ya Watu wa Zanzibar na ukusanyaji wa ada ambazo wananchi wanaokopa hutakiwa kuzilipa. Pia, imekusanya mapato ya Shilingi Milioni Mia Moja na Nne (Tsh.104,000,000/=) kwa kuwekeza sehemu ya fedha na ada kutoka kwa waombaji wa mikopo.

Mhe. Mwenyekiti, mapato haya na marejesho yaliyokusanywa yamewezesha kutoa mikopo ya Shilingi Milioni Mia Sita (Tsh.600,000,000/=) kama ilivyopangwa.

- Inawashajiisha wananchi kujiwekea akiba kwa kile wanachokipata. Jumla ya wateja 146 wamefungua akaunti katika Benki za Biashara na wateja wetu kwa ujumla wamemudu kujiwekea akiba katika vikundi vyao na katika akaunti za mtu mmoja mmoja.

Hadi kufikia mwezi Machi, 2017 jumla ya Shilingi Milioni Sabini na Tisa na Laki Mbili (TShs.79,200,000/=) zimehifadhiwa katika akaunti za wateja wa Mfuko. Pia imesaidia kuwapatia mikopo wateja 54 wa mradi wa huduma za fedha Unguja na Pemba (17 Wanawake na 37 Wanaume).

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, wizara kupitia Programu ya Mfuko wa Uwezeshaji imepanga kutoa mikopo 600 yenye

thamani ya Shilingi Milioni Mia Sita (Tsh.600,000,000/=) kwa vikundi na mjasiriamali mmoja mmoja; Itasimamia mikopo inayotolewa na kuhakikisha inatumiwa ipasavyo na inarudishwa kwa wakati kwa asilimia tisini na tano; Itaimarisha uwekaji wa kumbukumbu za wateja na kuendelea na juhudi mbali mbali za kutunisha Mfuko.

Mhe. Mwenyekiti, ili wizara iweze kutekeleza programu hii kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2017/2018, naliomba Baraza lako liidhinishe jumla ya Shilingi Milioni Mia Mbili na Thalathini na Mbili, Laki Nne Thamanini na Sita Elfu, (Tsh.232,486,000/=**)**.

Programu ndogo ya Usimamizi na Uimarishaji wa Vyama vya Ushirika

Mhe. Mwenyekiti, programu hii ina lengo la kuimarisha mageuzi ya Vyama vya Ushirika ili viweze kuchangia katika kukuza ajira na kipato kwa wananchi na kuviimarisha Vyama vya Ushirika viwe endelevu, vyenye ubunifu na vinavyokidhi mahitaji ya wanachama wake kijamii na kiuchumi. Wizara kwa kupitia programu hii kwa mwaka wa fedha 2016/2017 imefanikiwa kutekeleza yafuatayo:

- Imehamasisha na kusajili Vyama vya Ushirika 259 (Unguja 204 na Pemba 55). Kati ya hivyo 3 ni *SACCOS*, na 256 ni vyama vya uzalishaji na utoaji wa huduma. Hadi kufikia Aprili,2017 vyama 3,071 vimesajiliwa.

- Imeimarisha uwezo wa kiutendaji wa vyama vya ushirika 511 (Unguja 444 na Pemba 67) kwa kuvipatia mafunzo ya mageuzi ya uendeshaji wa vyama hivyo. Mafunzo haya yameimarisha umiliki na ushiriki katika vyama vyao. Pia, imetoa mafunzo ya mbinu bora ya kilimo cha mboga mboga na usarifu wa mazao na kuwaunganisha na huduma za mikopo ya pembejeo. Jumla ya vyama 7 vimepatiwa huduma hiyo.

- Imeunda Vyama vikubwa vinane (8) (4 Unguja na 4 Pemba) vya uzalishaji mazao ya kilimo kupitia mnyororo wa thamani.

- Imefanya ukaguzi wa kumbukumbu kwa vyama vya ushirika 962 (518 Unguja, Pemba 364). Kati ya vyama hivyo, Chama cha Ushirika (*ZYMC*) kinachotoa huduma za ukaguzi kimekagua hesabu za vyama 80. Matokeo ya ripoti za ukaguzi yanaonesha vyama vinaimarika. (Angalia Kiambatanisho namba 5).

- Imefanya ukaguguzi kwa *SACCOS* 230 (Unguja 138 na Pemba 92) na kuziwekea madaraja ili kuweza kutoa huduma stahiki na kwa ufanisi. Matokeo ya zoezi hili yameonesha *SACCOS* hizi zimepanda madaraja.

- Imesimamia ukuaji wa mitaji ya *SACCOS* kutoka Shilingi Bilioni Sita nukta Sita (Tzs: Bilioni 6.6) Mwezi Disemba 2015 hadi kufikia Shilingi Bilioni Kumi na Moja nukta Mbili (Tzs. Bilioni 11.2) mwezi Machi 2017. Kiwango hiki cha ukuaji wa mitaji ni asilimia 58. (Angalia Kiambatanisho namba 6 na 7).

- Imeadhimisha Siku ya Ushirika Duniani tarehe 02 Julai 2016 ambapo Kauli mbiu ilikuwa ni "USHIRIKA NI NGUVU YA PAMOJA KATIKA KULETA MAENDELEO ENDELEVU" Wanaushirika na wadau wa ushirika walishiriki shughuli mbali mbali za kijamii zikiwemo kufanya usafi wa mazingira nyumba za Wazee, nyumba ya kulelea Watoto Mayatima Mazizini, Hospitali za wilaya na kutoa misaada kwa Wazee,Wagonjwa na Watoto.

- Imesaidia uandishi wa miradi mitatu (3) ya usarifu wa Mazao Vyama 3 vya Ushirika pamoja na kuwaombea ruzuku kutoka Programu ya *MIVARF*. Pia, Programu imesaidia vyama hivyo kupatiwa mkopo kwa ajili ya mchango wa asilimia 25 zilizohitajika na *MIVARF* kama dhamana. (Angalia Kiambatanisho namba 8). Hatua za kutafuta wazabuni wa kununua mashine za usarifu wa mazao zinaendelea.

- Imekusanya jumla ya Shilingi Milioni Ishirini na Mbili Laki Nane na Sabini Elfu (Tsh.22,870,000/=) kutokana na Ada ya Usajili na Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika sawa na Asilimia Sabini na Moja (71%) ya lengo.

Mhe. Mwenyekiti, Kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara kupitia Programu ya Usimamizi na Uimarishaji wa Vyama vya Ushirika imepanga kuhamasisha na Kusajili Vyama vya Ushirika 150 (Unguja 80 na Pemba 70); kusimamia uundwaji wa Vyama vikuu vitatu (3) vya kisekta; kujenga uwezo wa kiutendaji kwa Viongozi 700 na Wanachama 2,110 wa Vyama vya Ushirika; kusimamia utekelezaji wa Sheria kwa kufanya Ukaguzi wa Kawaida wa Vyama 1,000 (Unguja 650 na Pemba 350); na Ukaguzi wa Hesabu kwa Vyama 200 (Unguja 120 na Pemba 80).

Mhe. Mwenyekiti, ili Wizara iweze kutekeleza Programu hii kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2017/2018, naliomba Baraza lako liidhinishe jumla ya Shilingi Milioni Mia Tatu Thamanini, Thamanini na Mbili Elfu (Tsh.380,082,000/=).

Program ndogo ya Uratibu na Uendelezaji wa Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

Mhe. Mwenyekiti, Program hii ina lengo la kupanua na kukuza Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ili kukuza kipato cha wananchi na kuongeza ajira. Wizara kwa kupitia Programu hii kwa mwaka wa fedha 2016/2017 imefanikiwa kutekeleza yafuatayo:

Imewajengea uwezo wajasiriamali 50 (27 wanawake na 23 wanaume) wenye viwanda vidogo vidogo Unguja na Pemba juu ya ujuzi wa biashara na masoko. Wajasiriamali hao walishiriki katika maonesho ya Afrika Mashariki ya Jua Kali na Kongamano la Wajasiriamali wakiwa na bidhaa zilizo bora na zinazokubalika katika soko.

Imewapatia mafunzo ya awali ya ujasiriamali vijana 100 Unguja na Pemba waliomaliza masomo katika Vyuo Vikuu vya Zanzibar kama vile *SUZA*, ZU , *IPA* na vijana ambao bado hawajaajiriwa. Vijana kutoka Mabaraza ya vijana ya Wilaya ya Kati, Kaskazini na Mjini nao pia wameshiriki. Baadhi ya vijana hao tayari wameanzisha biashara za kilimo cha mboga mboga na matunda, ufugaji, kazi za mikono, biashara za maduka na usarifu wa mazao ya kilimo.

Imefanya Kongamano la wajasiriamali tarehe 3 na 4 Disemba, 2016 ambapo vijana 325 wameshiriki wakiwemo wajasiriamali mmoja mmoja, vikundi na makampuni ya ujasiriamali. Kongamano hilo limewaunganisha wajasiriamali na taasisi mbali mbali za kifedha na kitaaluma.

Imewasaidia Wajasiriamali wadogo wadogo 26 Unguja na Pemba kushiriki katika Maonesho ya JUAKALI yaliyofanyika nchini Uganda. Kutokana na ushiriki huo, Wajasiriamali wa Zanzibar waliendelea kujifunza mbinu mbali mbali za kuimarisha bidhaa zao na kupata uzoefu juu ya upatikanaji wa soko kutoka kwa washiriki wa nchi nyengine.

Imefanikiwa kutoa mafunzo ya nadharia na vitendo juu ya ukuzaji wa biashara, kwa wajasiriamali 124, (wanawake 93 na wanaume 31) kupitia Kituo cha Kulea na Kukuza Wajasiriamali *Incubation Center*. Kwa mwaka

wa fedha 2016/2017 kituo kiliwapatia mikopo Makampuni sita yaliyoanzishwa kituoni hapo.

Kiasi cha Shillingi Milioni Ishirini na Saba na Laki Tano (Tsh.27,500,000/=) zilitolewa kwa ajili ya ununuzi wa vitendea kazi mashine. Fedha hizo zilitokana na Mfuko Maalum unaowasaidia wajasiriamali wanaomaliza kituoni hapo uliochangiwa na *Zanzibar Milele Foundation*.

Pia, Wizara imesaidia Kampuni tatu kupata Shillingi Milioni Kumi na Mbili, Laki Sita, Hamsini Elfu (Tsh.12,650,000/-) kutoka *COSTECH* kwa ajili ya kukuza na kuimarisha biashara zao. Kampuni hizo zilinunua vifaa ikiwemo vifungashio kwa ajili ya bidhaa wanazozizalisha pamoja na vifaa vya teknolojia ya mawasiliano. Kampuni zote hizo zinaendelea na uzalishaji na utoaji wa huduma baada ya kuhitimu kituoni.

Imeeneza huduma za Uwezeshaji kwa Wananchi 53 waliojiunga na Kituo kutoka sehemu mbali mbali wakiwemo wakulima wa mbogamboga kutoka kijiji cha Mtule ambao tayari wameweza kusarifu na kuongeza thamani ya matunda na mboga mboga kutoka katika mashamba yao.

Pia, walezi wa familia kutoka *SOS*, walipatiwa mashine mbili za kutengeneza sabuni na taasisi hiyo baada ya kuhitimu mafunzo katika Kituo cha Kulea Wajasiriamali.

Imeendelea na taratibu za uanzishaji wa Kituo cha Kulelea Wajasiriamali Pemba ambapo kituo hiki kitaanzishwa katika eneo la Mbuzini Pemba.

Imeendelea kukiimarisha Kituo cha Kutengeneza Vifaa Vinavyotumia Umeme wa Jua *Barefoot Collage* kilichopo Kibokwa Kaskazini Uguja. Jumla ya kinamama 9 walipewa mafunzo hayo katika mwaka huu wa fedha 2016/2017. Kina mama hao walitengeneza taa 798 zikiwemo za mikononi *Lanten* 64 na kufunga taa za majumbani *Home Lighting System* 734, katika nyumba 300. Taa hizo zimefungwa katika vijiji vya Mbuyu tende, Bumbwini Kiongwe.

Mhe. Mwenyekiti, Kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara kupitia Programu ya Uratibu na Uendelezaji wa Wananchi kiuchumi itaendelea kutoa mafunzo ya ujasiriamali;

Itatekeleza miradi ya “kuwawezesha Wabunifu ili kutoa huduma na bidhaa zenye ubora kwa wajasiriamali na Uwezeshaji Vijana kupitia usarifu wa taka za plastiki;

Itafanya ziara za kujifunza kwa wajasiriamali wabunifu 15 wa kutengeneza mashine Unguja na Pemba;

Itafanya mafunzo ya utumiaji wa mashine zitakazotengenezwa kwa wajasiriamali wadogo 35 Unguja na Pemba;

Itagharamia ununuzi wa mashine zinazotengenzwa kwa ajili ya wajasiriamali wadogo;

Itaratibu uendeshaji wa Kituo cha Kutengeneza Vifaa vya Umeme wa Jua *Barefoot*;

Itawawezesha wajasiriamali 24 kushiriki katika maonyesho ya Afrika Mashariki JUA KALI nchini Burundi na itaimarisha kitengo cha Technolojia ya Habari na Mawasiliano *ICT Hub*;

Itaendelea kutoa mafunzo katika kituo cha kulea wajasiriamali na itaratibu shughuli za Uwezeshaji wa Wananchi kiuchumi.

Mhe. Mwenyekiti, Ili Wizara iweze kutekeleza Programu hii kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Naliomba Baraza lako liidhinishe jumla ya Shilingi Milioni Mia Sita, Laki Moja na Elfu Tatu (Tsh.600,103,000/=**)**.

Programu Kuu ya Kukuza Usawa wa Kijinsia na Uendelezaji Wanawake.

Mhe. Mwenyekiti, Programu inalenga kukuza Usawa wa Kijinsia, kuimarisha uwezo wa Wanawake kiuchumi, kuongeza ushiriki wa wanawake katika uongozi na vyombo vya kutoa maamuzi pamoja na kuratibu mapambano dhidi ya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto. Programu hii ina programu mbili ndogo zifuatazo:

Programu ndogo ya Uratibu wa Masuala ya Usawa wa Kijinsia na Uendelezaji Wanawake

Mhe. Mwenyekiti, Programu ndogo ya Uratibu wa Masuala ya Jinsia ina lengo la kuleta usawa na uwiano wa kijinsia katika maendeleo pamoja na

kumwezesha mwanamke kiuchumi, kisiasa na kijamii. Kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara kupitia Programu hii imetekeleza yafuatayo:

Imehamasisha wanawake kuimarisha vikundi vya ujasiriamali na jumla ya vikundi 173 (115 Unguja na 58 Pemba) vilifanyiwa ufuatiliaji na tathmini kati ya hivyo vikundi 16 vimeunganishwa na fursa za ujasiriamali, vitano ushirika na viwili mikopo na kuvipatia ushauri na maelekezo katika kuviendeleza vikundi vyao.

Imeadhimisha Siku ya Wanawake Duniani tarehe 8/03/2017 katika Mkoa wa Kusini Unguja na Kusini Pemba. Ujumbe wa mwaka huu ulikuwa ni "Imarisha Fursa za Ajira kwa Kumwezesha Mwanamke Kiuchumi".

Maadhimisho hayo yalijumuisha kuelimisha jamii kupitia vyombo vya habari, utoaji wa zawadi kwa mwanamke jasiri, mkulima na mwanafunzi bora pamoja na usafi wa mazingira.

Imeratibu uanzishwaji wa Mtandao wa Wajasiriamali Wanawake Unguja na Pemba wenye lengo la kuwaunganisha pamoja kwa ajili ya kunufaika na fursa mbali mbali za kuendeleza biashara zao.

Jumla ya Wajasiriamali 388 Unguja na Pemba tayari wameshajiunga na Mtandao huo na kupatiwa mafunzo ya ujasiriamali ya nadharia na vitendo kwa wajasiriamali wanawake 70 (35 Unguja na 35 Pemba) ambayo yalihusu taratibu za uchukuaji na urejeshaji wa mikopo, taratibu za viwango na uongezaji wa thamani kwa bidhaa za matunda. Pia, Wajasiriamali hawa walishiriki katika Maonesho mbali mbali ya Wajasiriamali nchini.

Imewapeleka wajasiriamali wanawake kumi (10) katika ziara ya kimafunzo mjini Dar es Salaam katika kiwanda cha *SIDO* ambapo wamepata fursa ya kujifunza usindikaji wa maziwa na utenegenezaji wa bidhaa za maziwa ikiwemo mtindi na ufugaji wa ng'ombe wa kisasa.

Mhe. Mwenyekiti, Kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara kupitia Programu ya Uratibu wa Masuala ya Kijinisa na Uendelezaji wa Wanawake inatarajia kufanya ufuatiliaji wa vikundi vya wanawake na kuviunganisha na fursa zilizopo na itaelimisha jamii juu ya haki za wanawake na watoto.

Mhe. Mwenyekiti, Ili Wizara iweze kutekeleza Programu hii kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Naliomba Baraza lako liidhinishe jumla

ya Shilingi Milioni Mia Mbili na Arobaini na Saba, Laki Sita na Elfu Mbili (Tsh.247,602,000/=).

Programu ndogo ya Mapambano dhidi ya Udhalilishaji wa Wanawake na Watoto

Mhe. Mwenyekiti, Programu hii ina lengo la kukuza mwitiko na kuratibu mapambano dhidi ya vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto nchini. Kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara kupitia Programu hii imetekeleza yafuatayo:

Imepokea, kuyasikiliza na kuyafanyia kazi jumla ya malalamiko 173 (128 Unguja na 45 Pemba) juu ya changamoto mbali mbali zinazowakabili wanawake ikiwemo kutelekezwa, migogoro ya ndoa na familia, kupigwa na kudhulumiwa mali.

Kati ya hayo malalamiko 102 (28 Pemba na 74 Unguja) yalifanyiwa kazi ikwemo kusuluhisha wanandoa na kuwataka Mababa watoe huduma za matunzo kwa watoto na wake zao na malalamiko 67 yamefikishwa Mahakamani kwa kupatiwa ufumbuzi unaofaa. (Angalia Kiambatanisho namba 9).

Imepokea jumla ya simu 574 za waathirika wa vitendo vya udhalilishaji kati ya hizo simu 31 ndiyo rasmi ambazo zimesikilizwa na kupatiwa ushauri nasaha pamoja na maelekezo. Malalamiko haya yaliunganishwa na taasisi zinazotoa huduma za kisheria.

Imeadhimisha siku 16 za wanaharakati za kupinga vitendo vya Ukatili na Udhalilishaji dhidi ya Wanawake na Watoto kwa kufanya mikutano ya uhamasishaji jamii na kuwakutanisha watoa huduma na waathirika wa vitendo hivyo ili kujadili changamoto zinazokabili kesi hizo na kufanyiwa kazi.

Imetoa mafunzo kwa watoto wa Mabaraza 21 ya Watoto ya Wilaya ya Kusini Unguja, Skuli 17 na Madrasa 8 za Qur-an kutambua haki na wajibu wao. Mafunzo hayo yamewajengea uwezo na uthubutu wa kuripoti matukio ya ukatili na udhalilishaji.

Imetengeneza Muongozo wa Mabaraza ya watoto ambao umesambazwa kwa mabaraza yote ya Shehia na Wilaya. Kupitia muongozo huo jumla ya Mabaraza 45 ya Shehia, 11 ya Wilaya na Bodi ya Ushauri ya Watoto imeundwa kwa lengo la kukuza ushiriki na ushirikishwaji wa watoto.

Imeratibu mikutano 2 ya Kamati ya Mawaziri ya Kupambana na Vitendo vya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia. Kupitia mikutano hiyo Kamati hiyo imetoa msukumo katika kushughulikia matukio ya vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia.

Imetoa mafunzo kwa Viongozi wa dini 64 wa Unguja na Pemba katika kupambana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia. Viongozi hao huitumia taaluma hiyo katika kuelimisha na kuhamasisha jamii katika kupambana na kudhibiti ongezeko la vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia katika sehemu zao.

Imetengeneza jumla ya sehemu 40 za Mchezo wa redio wa Mshike Mshike ambao umerushwa katika vyombo vya habari Unguja na Pemba. Kupitia Mchezo huo jamii inakuza uelewa na muamko wa kupambana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto.

Mhe. Mwenyekiti, Kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara kupitia Programu ya Mapambano dhidi ya Udhalilishaji wa Wanawake na Watoto itaendelea kuwajengea uwezo wadau katika kupinga vitendo vya ukatili na udhalilishaji dhidi ya wanawake na watoto, pamoja na kuratibu utekelezaji wa Mpango wa Miaka Mitano wa Kupambana na Vitendo vya Ukatili na Udhalilishaji dhidi ya Wanawake na Watoto 2017 – 2022.

Mhe. Mwenyekiti, Ili Wizara iweze kutekeleza Programu hii kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Naliomba Baraza lako liidhinishe jumla ya Shilingi Milioni Hamsini na Tano na Laki Moja Tsh.55,100,000/=.

Programu Kuu ya Kuimarisha Huduma za Ustawi

Mhe. Mwenyekiti, Programu hii ina lengo la kuimarisha Mifumo ya Hifadhi ya Jamii ikiwemo Hifadhi ya Mtoto, huduma za Wananchi Wanaoishi katika Mazingira Magumu zaidi na kuimarisha Ustawi na Maendeleo ya Vijana. Programu hii ina Programu ndogo zifuatazo:

Programu Ndogo ya Uratibu wa Huduma za Uhifadhi wa Jamii

Mhe. Mwenyekiti, Programu hii ina lengo la kutoa huduma za kiustawi kwa makundi yanayoishi katika mazingira magumu. Kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara kupitia Programu hii imetekeleza yafuatayo:

Imepokea na kutathmini maombi mapya ya fidia kwa Wafanyakazi 19 (13 Unguja na 6 Pemba) walioumia wakiwa kazini na kulipa fidia ya maombi 22 ya

zamani yenye thamani ya Shilingi Milioni Kumi na Nane, Laki Sita Hamsini Elfu na Hamsini na Saba (Tsh.18,650,057/=) (6 Unguja yenye thamani ya Shilingi Milioni Nane, Laki Sita Tisini na Nane Elfu, Mia Tisa na Kumi (Tsh. 8,698,910/=) na 16 Pemba yenye thamani ya Shilingi Milioni Tisa, Laki Tisa Hamsini na Moja Elfu, Mia Moja Arobaini na Saba (Tsh**.** 9,951,147/-).

Aidha, hadi kufikia mwezi Mei mwaka 2017 kuna deni la fidia la wafanyakazi 15 lenye thamani ya Milioni Thalathini, Laki Sita na Saba, Mia Nane na Thalathini (Tshs. 30,607,830/=); (6 kwa Unguja lenye thamani ya Shilingi Milioni Kumi na Tatu, Laki Sita na Nane, Mia Mbili Arobaini na Nane (Tsh. 13,608,248/-) na 9 Pemba lenye thamani ya Shilingi Milioni Kumi na Sita, Laki Tisa Tisini na tisa, Mia Tano Thamanini na Mbili (Tsh. 16,999,582/=).

- Inaendelea kuwahudumia Wazee 73 (Unguja 64 na Pemba 9) wa Welezo, Sebleni na Limbani kwa kuwapatia malazi, chakula, nguo na posho.

Vilevile, imewapatia mahitaji ya msingi watoto 33 wanaolelewa katika nyumba ya kulelea watoto Mazizini (Wanaume 17 na Wanawake 16) na kuwapatia waathirika wa ukoma 55 (wanaume 28 na wanawake 27) posho ya Tsh. 25,000/- kila mmoja kwa mwezi. Katika kipindi hichi jumla ya watoto 24 wamehifadhiwa kwa muda katika Nyumba ya Watoto Mazizini; 17 kati yao walirejeshwa katika familia zao baada ya matatizo yao kumalizika, 5 wanaendelea kuhifadhiwa na wawili (2) wapo katika hatua za mwisho za kurejeshwa katika familia zao.

- Imewapatia posho ya Tsh. 20,000/- kila mmoja kila mwezi jumla ya familia 154 (Unguja 95 na Pemba 59) zinazoishi katika mazingira magumu. Familia 11 (Unguja 4 na Pemba 7) zenye watoto mapacha zaidi ya wawili zimepatiwa msaada wa posho la maziwa. Vile vile, maiti kumi na tano (15) zisizokuwa na wenyewe zimezikwa.

- Imepokea na kushughulikia matukio 266; (Unguja 173 na Pemba 93) ya ukatili na udhalilishaji dhidi ya watoto. Aidha, Wizara imekuwa ikihakikisha watoto wanaokabiliwa na mivutano ya malezi wanawekwa kwenye mazingira salama kwa kuzingatia maslahi bora ya watoto. Malalamiko yanayoshindikana kupatiwa ufumbuzi kwa kutokubaliana baina ya wazazi/ walezi wa pande mbili, malalamiko hayo hufanyiwa rufaa kwenye mahakama ya watoto. (Angalia Kiambatanisho namba 10a na 10b)

- Imefuatilia Kesi za Madai 41 za watoto kwenye Mahakama za Mikoa na Mahakama ya Watoto Vuga. Kati ya hizo; kesi 29 ni za madai yanayohusu

malezi na 12 ni za matunzo. Aidha, Jumla ya kesi 34 za Watoto Wanaokinzana na Sheria zimefuatiliwa katika Mahakama za Watoto Unguja na Pemba. Kati ya hizo kesi 8 zimeshatolewa hukumu, 24 zinaendelea na 2 zimefutwa.

Imepokea matukio 571 (Unguja 537 na Pemba 34) ya Udhalilishaji wa Watoto kutoka vituo vya Mkono kwa Mkono Unguja na Pemba; Matukio hayo yalihusisha Kubakwa 273 kati ya hayo Pemba 8, kukashifiwa 211 kati ya hayo Pemba 9, kulawitiwa 27; kati ya hayo Pemba 7 na Ujauzito 60; kati ya hayo Pemba 10. Pia, iliendelea kuimarisha Ulinzi wa Mtoto kwa kufanya matengenezo ya Kitengo cha Hifadhi ya Mtoto Wilaya ya Kaskazini A, Mkoani na Wete.

- Imefanya utambuzi wa Watoto 991 (wanaume 467 na wanawake 524) wenye Mazingira Magumu na kusajiliwa upya katika Shehia 6 za Mjini, Unguja na Shehia 10 za Chake Chake, Pemba. (Angalia Kiambatanisho namba 11).

- Imeendelea kusimamia uendeshaji wa Vituo vya Kulea Watoto Yatima 9 (7 Unguja na 2 Pemba). Hadi kufikia mwezi Mei 2017, jumla ya watoto 481 (wanaume 393 na wanawake 88) wanalelewa katika vituo hivyo. Vilevile, ilikifungia kuendelea kutoa huduma ya matunzo ya watoto Kituo cha Omar bin Khatwaab kilichokuwepo Fumba kutokana na kukosa viwango. Watoto wote 32 wa kituo hicho walipatiwa Makaazi katika Kituo cha Kulea Watoto cha *S.O.S*.

- Inaendelea kutekeleza mradi wa Marekebisho ya Tabia kwa Watoto Wanaokinzana na Sheria na walio katika hatari ya kukinzana na Sheria ambapo jumla ya watoto 31 (wanaume 28 na wanawake 3) walipokelewa katika kituo. Kati ya hao, watoto 10 walikuwa katika hatari ya kuingia katika makosa na kukinzana na Sheria. Mabadiliko ya tabia ya watoto hao yalikuwa ni mazuri sana, ambapo ufuatiliaji unaonesha kuwa kati ya watoto 38 waliomaliza watoto 37 wanaendelea vizuri na 1 ameonekana kurejea tabia zake za awali.

- Imeratibu mikutano ya kila robo mwaka na wadau wa Hifadhi ya Jamii Unguja na Pemba kwa lengo la kutoa fursa ya kutathmini shughuli za wadau wa Hifadhi ya Jamii na kuangalia aina na viwango vya huduma zinazotolewa, walengwa wanaofikiwa pamoja na fursa zilizopo na changamoto zinazowakabili wadau katika utekelezaji wa utoaji wa huduma.

- Imefanikisha maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Wazee tarehe 1 Oktoba 2016 yaliyofanyika katika Kiwanja cha Gombani mpya Pemba. Mgeni

rasmi katika maadhimisho hayo alikuwa ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein.

- Maadhimisho hayo yaliambatana na shughuli za wazee zikiwemo kuwakagua wagonjwa, kuwapatia matibabu na kuwatembeza katika Fukwe. Ujumbe wa mwaka huu katika maadhimisho hayo ulikuwa ni "Chukua Hatua Zuia Unyanyasaji dhidi ya Wazee."

- Inaendelea kuratibu, kusimamia na kutekeleza Mpango wa Pensheni Jamii kwa Wazee wenye umri wa miaka 70 na kuendelea ambapo kwa mwaka huu Wazee wameongezeka kutoka 24,178 hadi 27,097. Aidha, Wazee 1,422 wamefariki. Mwitiko wa Wazee kwenda kupokea Mafao yao umeongezeka kutoka Mwezi wa Julai mwaka 2016 kwa asilimia 86% hadi kufikia Aprili 2017 kwa asilimia 94%. Changamoto kubwa ni kutokamilika kwa Mfumo madhubuti wa kuhifadhi kumbukumbu za Wazee.

Mhe. Mwenyekiti, Kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara kupitia Programu ya Uratibu wa Huduma za Uhifadhi wa Jamii itaimarisha hifadhi ya Mtoto, itaendeleza utoaji wa misaada ya kijamii kwa wanaoishi katika mazingira magumu zaidi, itaimarisha Hifadhi ya Wazee, itakamilisha uandaaji wa Mfumo wa kuhifadhi kumbukumbu za taarifa za Pensheni ya Jamii na itafanya ukarabati wa nyumba za Wazee.

Mhe. Mwenyekiti, Ili Wizara iweze kutekeleza Programu hii kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Naliomba Baraza lako liidhinishe jumla ya Shilingi Bilioni Nane, Milioni Mia Tano Kumi na Nne, Laki Tisa Tisini na Saba Elfu (Tshs.8,514,997,000/=**)**.

Programu Ndogo ya Maendeleo ya Vijana

Mhe. Mwenyekiti, Programu hii ina lengo la kuratibu shughuli za Maendeleo ya Vijana ikiwemo kuimarisha ushiriki wao, kuwajengea uwezo na kuwaunganisha kwenye fursa katika masuala ya kiuchumi na kijamii. Kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara kupitia Programu hii imetekeleza yafuatayo:

- Imeendelea kutoa Mafunzo ya Stadi za Maisha kwa Vijana walio nje ya skuli kwa kutumia Mwongozo ulioandaliwa na Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Idadi ya Watu Duniani (*UNFPA*). Vijana 60 kutoka Wilaya zote za Zanzibar walipewa mafunzo ya Ukufunzi. Kwa kushirikiana na Taasisi ya *Africa Muslim Agency* imewapatia mafunzo ya Stadi za Maisha Vijana 461

Unguja na Pemba. Pia, imeelimisha jamii kupitia vyombo vya habari juu ya umuhimu wa Stadi za Maisha kwa Vijana**.**

- Imefanya ufuatiliaji kwa vikundi 62 vya Vijana wanaojishughulisha na shughuli za kiuchumi na kimaendeleo kwa Mikoa yote ya Zanzibar kwa lengo la kufahamu mafanikio, fursa na changamoto zinazowakabili Vijana katika shughuli zao za kila siku ili kuimarisha shughuli hizo. Miongoni mwa changamoto iliobainika ni kukosekana kwa vyanzo vya kudumu vya maji kwa matumizi ya umwagiliaji wa mazao yao. Wizara imeanza hatua za kuwachimbia visima vikundi 9 vya vijana vilivyoonesha bidii katika shughuli za kilimo cha Kisasa Unguja na Pemba. Vikundi vinne (4) (2 Unguja na 2 Pemba) vitawekewa umeme wa jua katika visima vyao.

- Kwa kushirikiana na Program ya Fursa Kijani, Wizara imeshajihisha vijana 396 (190 Unguja na 206 Pemba) kuendeleza kilimo endelevu na cha kisasa. Kati ya hao, Vijana 60 (wanawake 30 na wanaume 30) waliunganishwa na Programu hiyo. Baada ya mafunzo hayo Vijana 18, (wanawake 6 na wanaume 12) waliajiriwa na Mradi wa Maendeleo ya Mji wa Fumba. Aidha, chini ya Programu hii, Wizara imewagharamia Vijana 10 (wanaume 6 na wanawake 4) ili kupata mafunzo hayo. Pia, Wizara imesaidia vijana 14 kutoka Pemba (wanaume 8 na wanawake 6) kujiunga na Tasisi ya kujitolea ya Vijana (*VSO*).

- Kwa kushirikiana na Shirika la Idadi ya Watu na Maendeleo iliadhimisha siku ya Vijana Duniani kuanzia tarehe 06 - 12 /08/2016 kwa kufanya programu mbali mbali zinazohusu Vijana. Ujumbe kwa mwaka 2016 ni**:** “Kuelekea 2030: Tokomeza Umasikini kwa Uzalishaji Endelevu na Matumizi yenye Tija.”

- Imeratibu Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2016 ikiwa ni pamoja na Usaili, Uzinduzi, Kilele na Wiki ya Vijana. Kilele kilifanyika Mkoa wa Simiyu; Mgeni Rasmi alikua Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein. Aidha, kwa mwaka 2017; Uzinduzi ulifanyika Mkoa wa Katavi ambapo Mgeni Rasmi alikuwa Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar Mhe. Balozi Seif Ali Iddi**.** Ujumbe kwa mwaka 2017 ni **“**Shiriki Kukuza Uchumi wa Viwanda kwa Maendeleo ya Nchi yetu” Aidha, Kilele cha Mbio hizo pamoja na wiki ya Vijana Kitaifa, zinatarajiwa kufanyika Mkoa wa Mjini Magharibi Oktoba 14, 2017. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, Kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara kupitia Programu ya Maendeleo ya Vijana itaendelea kutoa mafunzo ya Stadi za Maisha kwa

Vijana 330, itahamasisha na kuimarisha Vikundi vya Uchumi vya Vijana 24 na itaratibu Mbio za Mwenge wa Uhuru.

Baraza la Vijana

Mhe. Mwenyekiti, Kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Baraza la Vijana Zanzibar limefanikiwa kutekeleza yafuatayo:-

- Imekamilisha uundwaji wa Mabaraza ya Vijana kwa ngazi ya Shehia, Wilaya na Taifa ambapo Mabaraza ya Vijana 52 ya Shehia yameundwa, 11 ya Wilaya na Baraza la Vijana Taifa.

- Imefanya uzinduzi wa Mabaraza ya Vijana kwa Wilaya zote za Unguja na Pemba.

- Imetoa mafunzo kwa Viongozi 53 (wanawake 21 na wanaume 32) wa Mabaraza ya Vijana kwa Wilaya tatu za Unguja na Taifa. Mafunzo hayo yalihusisha masuala ya uongozi, uzalendo, demokrasia, Sheria ya kuanzisha Baraza la Vijana Zanzibar na muhimu wa uutunzaji wa amani kwa vijana.

Mhe. Mwenyekiti, Baraza la Vijana kupitia Programu ya Maendeleo ya Vijana katika mwaka wa fedha 2017/2018 italijengea uwezo Baraza la Vijana kwa kuipatia Sekretarieti vifaa kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli na majukumu ya Baraza; itayaunganisha Mabaraza ya Vijana na fursa za kiuchumi, kijamii na kiutamaduni katika taasisi mbali mbali pamoja na kuendelea kuratibu uendeshaji wa Baraza ya Vijana Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, Ili Wizara iweze kutekeleza Programu ya Maendeleo ya Vijana kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Naliomba Baraza lako liidhinishe jumla ya Shilingi Milioni Mia Nne Ishirini na Saba, Laki Tatu Sitini na Tatu Elfu (Tsh.427,363,000/=**)** ikiwa ni pamoja na ruzuku ya Baraza la Vijana.

Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto

Mhe. Mwenyekiti, Programu hii ina jukumu la kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Mipango, Sera, Tafiti, Maslahi ya wafanyakazi na kuimarisha mazingira bora ya utendaji kazi. Programu hii ina programu ndogo zifuatazo:-

Programu ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara

Mhe. Mwenyekiti, Programu hii ina jukumu la kuratibu na kusimamia utayarishaji na utekelezaji wa Sera, Mipango, Tafiti, Programu na Miradi ya Maendeleo ya Wizara, pamoja na kufanya ufuatiliaji na tathmini ya shughuli za Wizara. Pia, Inaimarisha mashirikiano ya kisekta, kitaifa, kikanda na kimataifa pamoja na kuratibu na kusimamia utekelezaji wa masuala mtambuka ikiwemo jinsia. Kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara kupitia Programu hii imetekeleza yafuatayo:

- Imekamilisha uandaaji wa Sera ya Jinsia ya mwaka 2016 na Sera ya Usalama na Afya Kazini ya mwaka 2016 pamoja na kuchapisha nakala 231 za Sera ya Jinsia na nakala 1200 za Sera ya Usalama na Afya Kazini. Aidha, imekamilisha uandaaji wa Mpango wa utekelezaji wa rasimu ya Sera ya Uwezeshaji na Sera ya Hifadhi ya Jamii 2014.

- Imefanya mapitio ya Sera ya Mtoto ya mwaka 2001 ambapo rasimu ya Sera mpya imeshapitiwa na wadau na Viongozi mbali mbali kwa ajili ya kuiimarisha. Wizara inakamilisha uandaaji wa Mpango wa Utekelezaji wa Sera hiyo ambapo Rasimu ya mwanzo imeshapitiwa na wadau.

- Imeratibu uandaaji wa Mpango wa Miaka Mitano wa Kupambana na Vitendo vya Ukatili na Udhalilishaji dhidi ya Wanawake na Watoto (2017 - 2022).

- Imeratibu uandaaji wa taarifa ya utekelezaji wa Mkutano wa 61 wa Hadhi na Haki ya Wanawake ambayo ilijumuishwa na ya Tanzania Bara na kuwasilishwa katika Tume ya Kusimamia na Kuratibu utekelezaji wa haki na Hadhi ya Wanawake nchini Marekani. Ujumbe ni ‘Kumwezesha Mwanamke Kiuchumi katika Ulimwengu wa Kazi’.

- Imewajengea uwezo Maofisa 20 wa Wizara katika masuala ya Ufuatiliaji na Tathmini ya *MKUZA*, Malengo Endelevu ya Maendeleo na kuandaa viashiria vitakavyopima utekelezaji wa Sera ya Jinsia.

Pia, imefanya ufuatiliaji wa shughuli za kawaida za Wizara Unguja na Pemba. Changamoto zilizobainika zilifanyiwa kazi ikiwemo kuratibu upatikanaji wa mafunzo kwa vitendo kwa vikundi vya ujasiriamali kupitia *Incubation, Barefoot, Permaculture* na *SIDO* Dar es Salaam ambapo

walijifunza namna ya kusarifu maziwa na kurekebisha kasoro mbali mbali za kiutendaji zilizojitokeza.

- Imeandaa andiko la nadharia juu ya utafiti wa kuzitambua fursa za ajira zilizopo kwa vijana katika Sekta ya utalii, uvuvi wa bahari kuu na kilimo. Andiko la mradi wa kusarifu taka ngumu pamoja na uanzishaji wa kiwanda cha vifungashio kwa bidhaa mbali mbali za Wajasiriamali. Aidha, programu imeandaa andiko la nadharia kwa ajili ya kuimarisha kitengo na Mfumo wa takwimu wa Wizara.

Mhe. Mwenyekiti, Kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara kupitia Programu ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara itamalizia hatua za uandaaji wa Sera ya Mafunzo ya Wanagenzi, Sera ya Uwezeshaji na Sera ya Mtoto;

Itaandaa Sheria ya Hifadhi ya Jamii; itaratibu ufanyaji wa Utafiti wa kuzitambua fursa za ajira zilizopo kwa vijana katika Sekta ya utalii, uvuvi wa bahari kuu na kilimo;

Itaimarisha mashirikiano, itandaa Mpango Mkakati wa Wizara, itaandaa Mfumo wa Ufuatiliaji na tathmini wa Wizara;

Itafanya ziara za ufuatiliaji na tathmini ya Shughuli za Wizara;

Itaimarisha kitengo cha takwimu cha Wizara na itaratibu utekelezaji wa Programu na miradi ya Wizara.

Mhe. Mwenyekiti, Ili Wizara iweze kutekeleza Programu hii kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Naliomba Baraza lako liidhinishe jumla ya Shilingi Milioni Mia Nne na Ishrini na Saba, Laki Nane Thalathini na Nane Elfu (Tsh.427,838,000/=).

Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji

Mhe. Mwenyekiti, Programu hii ina lengo la kujenga mazingira mazuri ya Kazi kwa kuhakikisha upatikanaji wa maslahi ya wafanyakazi, vifaa na huduma muhimu. Kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara kupitia Programu hii imetekeleza yafuatayo:

- Imeanza ujenzi wa ghorofa ya kwanza ya Jengo la Makao Makuu ya Wizara Mwanakwerekwe kwa lengo la kuimarisha mazingira safi na salama kwa wafanyakazi ili waweze kuwahudumia wananchi ipasavyo.

- Imefanya matengenezo ya Makaazi ya Wazee Limbani Wete, Pemba na kuyazungushia uzio ili kuimarisha usalama wa Wazee wanaotunzwa katika maakazi hayo.

- Imenunua vitendea kazi ikiwemo "*Overhead Projector*" kwa ajili ya Ukumbi wa Mkutano wa Wizara, Kompyuta kumi (10), Printa sita (6), Fotokopi Mashine moja (1) na kuyafanyia matengenezo ya kawaida Magari manane (8) ya Viongozi na ya huduma nyenginezo. Vile vile, imenunua seti tatu (3) za samani pamoja na kufanya matengenezo ya mashine za fotokopi tatu (3).

- Imewasaidia wafanyakazi ishirini na saba (27) kupata mafunzo katika fani mbalimbali Ndani na Nje ya Nchi wakiwemo 21 muda mfupi na 6 muda mrefu.

- Imefanya mafunzo kwa Watumishi sitini (60) (wanaume 30 na wanawake 30) wa kada za Uhudumu, Ulinzi, Udereva na Utarishi kwa lengo la kuwapa uelewa juu ya Sheria za Utumishi wa Umma na Kanuni zake.

Kupitia kitengo cha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano *TEHAMA*, Wizara imetoa mafunzo ya matumizi ya Serikali Mtandao *e-government* kwa watendaji wa ngazi mbalimbali na viongozi. Pia, imeweka mitambo ya *CCTV* ili kuimarisha usalama wa jengo na vifaa vya Wizara.

Imeajiri wafanyakazi saba (7) (wanaume 3 na wanawake 4) kwenye Kitengo cha Hifadhi ya Mtoto. Kati ya hao wanne (4) wanafanya kazi Pemba na watatu (3) Unguja. Pia, imepokea watumishi wawili (2) kwa njia ya uhamisho.

Imeelimisha jamii kupitia vyombo vya habari kuhusu shughuli zinazotekelezwa na Wizara na ilielimisha jamii kupitia vipeperushi, mabango na stika.

Imewawezesha Watendaji Wakuu wa Wizara kufanya ziara za kikazi nchini India, Qatar, Ethiopia, Burundi na New York.

Imefanya malipo ya posho la likizo kwa wafanyakazi mia na kumi (110) Unguja 80 na Pemba 30, malipo ya saa za ziada *overtime* kwa wafanyakazi thalathini na mbili (32) Unguja 18 na Pemba 14 na kusimamia upatikanaji wa

malipo ya kiinua mgongo kwa watumishi wanne (4) Unguja 2 na Pemba 2 waliostaafu kazi kisheria.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara kupitia Programu ya Utawala na Uendeshaji itakamilisha ghorofa moja ya jengo la Makao Makuu ya Wizara;

Itafanya uchambuzi yakinifu kwa watumishi wote wa Wizara na kuandaa Mpango Mkakati wa Rasilimali Watu;

Itawasaidia wafanyakazi tisa (9) ambao wanakamilisha mafunzo yao na sita (6) wapya watakao jiunga na vyuo Unguja na Pemba,

Taimarisha kitengo cha *TEHAMA* kwa kukipatia zana bora na za kisasa ili kiweze kufanya kazi zake kwa ubora zaidi pamoja na Kuimarisha mfumo wa Serikali mtandao;

Itaielimisha jamii kuhusu huduma zitolewazo na Wizara yetu;

Itasimamia utekelezaji wa Mkataba wa Huduma;

Italipa posho za likizo kwa wafanyakazi Mia Moja Sitini (160) kwa Unguja na Hamsini (50) Pemba;

Itahakikisha uwepo wa uhakika wa vitendea kazi kwa ajili ya kazi za kila siku za Wizara vikiwemo vifaa vya kuandikia, *Photocopy*, Kompyuta, na vyombo vya usafiri.

Mhe. Mwenyekiti, Ili Wizara iweze kutekeleza Programu hii kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Naliomba Baraza lako liidhinishe jumla ya Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Sita Thamanini na Tano, Laki Tano Hamsini na Moja Elfu Tsh.1,685,551,000/=.

Programu Ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba

Mhe. Mwenyekiti**,** Programu ya Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba inasimamiwa na Ofisi kuu Pemba na inaratibu utekelezaji wa Programu zote za Wizara kwa upande wa Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, ili Programu ya Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha

2017/2018, naliomba Baraza lako liidhinishe jumla ya Shilingi Milioni Mia Nane Ishirini na Tisa, Laki Tisa na Elfu Nane Tsh.829,908,000/= kwa ajili ya matumizi ya Programu na Mishahara kwa Pemba.

Programu Kuu ya Usimamizi wa Sheria za Kazi, Ukaguzi Kazi na Kazi za Staha kwa Wote

Programu hii ina lengo la kupunguza tatizo la ukosefu wa Ajira hasa kwa Vijana na kuzingatia Sheria na Miongozo ya kazi ikiwemo Usalama na Afya Kazini. Programu Kuu hii ina Programu ndogo zifuatazo:

Programu ndogo ya Uratibu wa Upatikanaji wa Ajira za Staha

Mhe. Mwenyekiti**,** Programu hii ina lengo la kukuza na kuongeza upatikanaji wa ajira za staha ili kupunguza tatizo la ukosefu wa ajira hasa kwa Vijana. Kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara kupitia Programu hii imetekeleza yafuatayo:

Imetoa mafunzo ya kuwawezesha kujiajiri na kuajirika Vijana 184 kwa Unguja na Pemba Wanaume 86 na Wanawake 98. Mafunzo hayo yalilenga kuwajengea uwezo wa kujiamini katika usaili *Speed dating* na uandikaji wa maelezo binafsi *CV*.

Kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani *ILO*, Taasisi ya Utalii ya Chuo Kikuu cha Taifa *SUZA* na Sekta Binafsi,

Wizara imeanzisha Programu maalum ya Mafunzo Kazi kwa Wanagenzi *Apprenticeship Program* katika fani ya Utalii ambayo itatekelezwa kwa muda wa miezi 18 kuanzia Machi 2017. Vijana 65 waliotoka katika Wilaya za Zanzibar wanashiriki. Inategemewa mafunzo haya yatabadili hali ya ajira kwa Vijana hawa katika sekta ya Utalii.

Imeelimisha jamii kupitia vyombo mbalimbali vya habari vya hapa Zanzibar kuhusu fursa za ajira. Hatua hiyo imewasaidia vijana kubadilika na kuwa na ari ya kufanyakazi katika sekta binafsi za ndani na nje ya nchi.

Kwa kushirikiana na Wakala Binafsi wa Ajira, Wizara imewaunganisha na waajiri vijana 791 Wanaume 245 na Wanawake 546 kwenda kufanyakazi nchini Qatar, Oman na Jumuia ya nchi za Falme za Kiarabu *U.A.E*. Vijana hao wameajiriwa kwenye fani za Udereva, Hoteli, Maduka, Mafuta, Uhasibu, IT, Upishi, Kazi za viwandani na kazi za nyumbani. Kwa kipindi

cha Julai 2016 hadi Machi, 2017 Vijana Elfu Saba, Mia Nane na Kumi na Moja 7,811 wameajiriwa ndani ya nchi katika taasisi mbali mbali za binafsi.

Imefanikiwa kupata fursa 100 za ajira ya udereva kwa Vijana nchini Qatar ambapo taratibu zinazohitajika za kuwapata Vijana hao kwa mujibu wa makubaliano yaliyofikiwa zinaendelea.

Mhe. Mwenyekiti, Kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara kupitia Programu ya Uratibu wa Upatikanaji wa Ajira za Staha itawezesha Jamii Kupata Fursa za Ajira za Staha kwa kutangaza nafasi za ajira kupitia Mfumo wa Taarifa za Soko la Ajira, itaimarisha mashirikiano na wadau katika ukuzaji wa Ajira, itatoa mafunzo kwa watafuta kazi hasa Vijana juu ya kujiajiri na kuajirika na itaelimisha jamii kuhusu masuala ya Ajira.

Mhe. Mwenyekiti, Ili Wizara iweze kutekeleza Programu hii kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Naliomba Baraza lako liidhinishe jumla ya Shilingi Milioni Mia Mbili Kumi na Tatu, Laki Nne, Thamanini na Nne Elfu Tsh.213,484,000/=.

Programu Ndogo ya Usimamizi wa Usalama na Afya Kazini

Mhe. Mwenyekiti, Programu hii inasimamia utekelezaji wa Sheria Namba 8 ya mwaka 2005 ya Usalama na Afya Kazini.

Kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara kupitia Programu hii imetekeleza yafuatayo:

Imefanya ukaguzi kwenye sehemu za kazi 139 Unguja 89, Pemba 50 na kutoa miongozo kwa Waajiri na Waajiriwa juu ya umuhimu wa kuweka mazingira bora ya Usalama na Afya Kazini ili kujikinga na matukio ya ajali na maradhi katika maeneo ya kazi.

Imefanya uchunguzi wa matukio ya ajali na maradhi yaliyoripotiwa kutoka sehemu nane (8) za kazi *Karafuu Beach Resort and SPA, Dream Zanzibar Hotel, Blue Bay Beach Resort and SPA, Melia Hotel, Estim Construction Company LTD, Tera Firma Construction Company, Marmaid Beach Resort na Hideaway Hotel.*

Imefanya usajili wa Sehemu za Kazi 78 Unguja 48, Pemba 30 kwa lengo la kuzitambua shughuli zao za kazi ili ziweze kufikiwa kwa Ukaguzi wa

Usalama na Afya Kazini.

Imeandaa kanuni mbili (2) za Usalama na Afya Kazini kwa ukaguzi wa ujenzi na majengo na Ukaguzi wa Usalama wa umeme.

Imewajengea uwezo Wawakilishi wa Usalama na Afya Kazini 90 Unguja 60, Pemba 30 kutoka taasisi za umma na taasisi za binafsi ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

Mhe. Mwenyekiti**,** Kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara kupitia Programu ya Usimamizi wa Usalama na Afya Kazini itasimamia ukaguzi wa Usalama na Afya Kazini wa Sehemu za Kazi 180 na Usajili wa Sehemu 120;

Itaimarisha Mfumo wa Ukaguzi wa hali ya Usalama na Afya Kazini kwa kuijengea uwezo Idara;

Itatoa elimu juu ya hatari zinazoweza kutokea katika Sehemu za Kazi na namna ya kuzikabili na itaimarisha uratibu na mashirikiano na wahusika wa Usalama na Afya Kazini.

Mhe. Mwenyekiti, Ili Wizara iweze kutekeleza Programu hii kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Naliomba Baraza lako liidhinishe jumla ya Shilingi Milioni Mia Mbili na Thalathini na Tatu, Laki Tano Thalathini Elfu Tsh.233,530,000/=.

Programu Ndogo ya Usimamizi wa Viwango vya Kazi vya Kimataifa na Majadiliano ya Pamoja Kazini

Mhe. Mwenyekiti**,** Programu hii ina lengo la kuhakikisha kunakuwepo utekelezaji mzuri wa Sheria za Kazi kama ilivyoelekezwa katika Sheria ya Ajira Namba 11 ya mwaka 2005 na Sheria ya Mahusiano Kazini Namba 1 ya mwaka 2005. Kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara kupitia Programu hii imetekeleza yafuatayo:

1) Imefanya ukaguzi kazi kwa Taasisi 240 Unguja 156 na 84 Pemba. Pia, Taasisi ishirini (20) zilipewa notisi na muda maalumu wa kurekebisha kasoro zilizobainika.

2) Imethibitisha Mikataba ya Kazi Elfu Mbili Mia Tatu na Moja 2,301 kwa Wafanyakazi wazalendo Unguja 1,939 na Pemba 362 kwa mujibu wa

Sheria za Kazi. Pia, vibali vya kazi Elfu Moja na Ishirini na tisa (1,029) kwa wafanyakazi wa kigeni vimetolewa.

3) Imezipatia elimu kazi kwa njia ya ana kwa ana taasisi 12 Unguja (8) na Pemba (4) juu ya Sheria za Kazi. Pia, vipindi 18 vya redio na 11 vya TV vilirushwa hewani kwa lengo la kuwapatia elimu waajiri, waajiriwa na jamii.

4) Imekagua vyama vitatu (3) vya Jumuiya ya wafanyakazi kwa mujibu wa Sheria ya Mahusiano Kazini Namba 1 ya mwaka 2005.

5) Imesuluhisha Migogoro ya Kazi 78 kati ya migogoro 90 iliyowasilishwa na iliyobakia inaendelea kushugulikiwa. Idadi kubwa ya migogoro hiyo ilihusu kuachishwa kazi.

6) Imefanya ufuatiliaji wa watoto waliotolewa katika Ajira na walio katika hatari ya kuingia katika Ajira za Watoto ambao wamerejeshwa Skuli na kuendelea na masomo katika Mkoa wa Kusini Unguja 966 wanawake 428 na wanaume 538 na Kaskazini Pemba 449 wanawake 211 na wanaume 238. Ufuatiliaji huo umeonesha watoto hao wanaendelea na masomo yao vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, Kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara kupitia Programu ya Usimamizi wa Viwango vya Kazi vya Kimataifa na Majadiliano ya Pamoja Kazini itafanya Ukaguzi Kazi kwa Taasisi 520; itathibitisha Mikataba ya Kazi 4000; itakagua Vyama vya Waajiri na Wafanyakazi 14; itasuluhisha migogoro ya kazi 145; itawatoa watoto 400 katika Ajira za Watoto na itasimamia utoaji wa Vibali vya Kazi 800 kwa wageni.

Mhe. Mwenyekiti, Ili Wizara iweze kutekeleza Programu hii kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Naliomba Baraza lako liidhinishe Shilingi Milioni Mia Sita na Nane, Laki Tano Tisini na Sita Elfu Tsh.608,596,000/=.

VIPAUMBELE VYA WIZARA KWA MWAKA 2017/18

Mhe. Mwenyekiti, Wizara kupitia Programu zake Kuu Tano (5) kwa mwaka wa fedha 2017/2018 imejipangia kutekeleza vipaumbele vifuatavyo:

1) Kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Ajira kwa Vijana na Kusimamia Sheria za Kazi;

2) Kupanua Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi pamoja na kuimarisha mfumo wa Ushirika.

3) Kuimarisha uratibu wa Programu za Hifadhi na Maendeleo ya Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto.

4) Kusimamia uendeshaji wa Baraza la Vijana; na

5) Kukuza Usawa wa Kijinsia pamoja na Kuratibu utekelezaji wa Mpango wa miaka mitano wa Kupambana na Vitendo vya Udhalilishaji wa Wanawake na Watoto 2017 – 2022.

MAOMBI YA FEDHA KWA PROGRAMU ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

Mhe. Mwenyekiti, Ili Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto iweze kutekeleza Programu zake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2017/2018, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi Bilioni Kumi na Nne, Milioni Mia Nne na Hamsini na Sita, Laki Sita Arobaini Elfu Tsh. 14,456,640,000.

Kati ya hizo, Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Mbili Kumi na Mbili, Laki Sita Sabini na Moja Elfu Tsh.1,212,671,000/- ni kwa ajili ya kutekeleza Programu ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.

Shilingi Milioni Mia Tatu na Mbili, Laki Saba na Elfu Mbili Tsh.302,702,000/- kwa ajili ya kutekeleza Programu ya Kukuza Usawa wa Jinsia na Uendelezaji wa Wanawake.

Shilingi Bilioni Nane, Milioni Mia Tisa Arubaini na Mbili, Laki Tatu na Sitini elfu Tsh. 8,942,360,000/- kwa ajili ya kutekeleza Programu ya Kuimarisha Huduma za Ustawi;

Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Tisa Arubaini na Tatu, Laki Mbili Tisini na Saba Elfu Tsh. 2,943,297,000/- kwa ajili ya kutekeleza Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto na

Shilingi Bilioni Moja, Milioni Hamsini na Tano, Laki Sita na Elfu Kumi Tsh. 1,055,610,000/- ni kwa ajili ya utekelezaji wa Programu ya Usimamizi wa Sheria za Kazi, Ukaguzi Kazi na Kazi za Staha kwa wote (Angalia Kiambatanisho namba 12).

Mhe. Mwenyekiti, Wizara katika kipindi cha mwaka wa fedha 2017/2018 inatarajiwa kukusanya mapato ya jumla ya Shilingi Milioni Mia Nane Tisini na Moja, Sabini na Nane Elfu Tsh. 891,078,000/- kutokana Ada za Usajili na Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika;

Ada ya Ukaguzi wa Mikataba ya Ajira Nje ya Nchi.

Ada ya Ukaguzi wa Maeneo ya Kazi na Vibali vya Kazi (Angalia Kiambatanisho namba 2).

HITIMISHO

Mhe. Mwenyekiti, Shughuli zote tulizozitaja hapo juu zimefanywa kwa mashirikiano na wadau mbali mbali wakiwemo taasisi za Serikali, taasisi za kiraia, Jumuiya za Dini na madhehebu mbali mbali ya dini, Washirika wa Maendeleo wakiwemo *UNFPA, UNICEF, UN WOMEN, UNDP, UNIDO, ILO, SAVE THE CHILDREN, FIH, MIVARF, HELP AGE INTERNATIONAL, CSEMA, Measure Evaluation, VSO, REPSSI, Shell, Milele Foundation, COSTECH*, Tunajali Program, Benki ya Maendeleo ya Afrika pamoja na Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mhe. Mwenyekiti, Napenda kuzishukuru Taasisi za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mashirikiano wanayotupa katika kutekeleza majukumu yetu. Taasisi hizo ni pamoja na Wizara ya Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu ya Mhe. Jenistar Muhagama, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Wazee, Wanawake na Watoto ya Mhe. Ummi Mwalimu, pamoja na Wizara ya Mambo ya Nje ya Nchi na Ushirikiano wa Kimataifa na Afrika Mashariki, na Wizara ya Mambo ya Nje ya Mhe. Migulu Nchemba, Naibu Waziri Mhe. Hamad Yussuf Masauni Mbunge wa Jimbo la Kikwajuni Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, Nawashukuru Mabalozi wote walioshirikiana na sisi katika kufanikisha shughuli za Wizara kwa maendeleo ya Wanawake, Watoto, Wazee, Vijana na Watoto. Balozi hizo ni pamoja na Oman, India, Qatar na Jamhuri ya Watu wa China na Msumbiji.

Mhe. Mwenyekiti, Taasisi za Kiraia ni pamoja na *ZAFELA, ZAWCO, ZAMWASO, ZLSC, COWPZ, PIRO, UVIKIUTA, UWAWAZA, UWT, ACTION AID, TAMWA, CUZA, ZYMC, ZAPROCO, Madrasa Resource Centre, JUMAZA, Male Network, ZIADA, SUA, Pathfinder na Ikhlas.* Pia, nazishukuru taasisi zote za kifedha, ikiwemo *PBZ , CRDB* na *NBC* kwa mashirikiano yao mazuri kwa Wizara. Nawaheshimu wote wa Mheshimiwa wetu Dkt. Ali Mohammed Shein kuhusu Wizara hasa Mhe. Zainab Omar Mohammed Waziri Mstaafu wa Wizara ya Wanawake na Watoto.

Mhe. Mwenyekiti, Navishukuru kwa dhati ya moyo wangu vyombo vyote vya habari vilivyoshirikiana na taasisi yangu katika kuelimisha jamii juu ya shughuli mbali mbali zinazotekelezwa na Wizara. Vyombo hivyo ni pamoja na *ZBC Redio* na televisheni, Gazeti la Zanzibar Leo, *Cable Television, TBC* na *Zenj FM, Channel Ten, BBC.* Sitaweza kuvitaja vyote lakini nawashukuru watendaji na viongozi wote wa vyombo vya habari walioshirikiana nasi.

Mhe. Mwenyekiti, Mwisho kabisa napenda kuwashukuru watendaji wote wa Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto kuanzia Naibu Waziri Mhe. Shadya Mohammed Suleiman; Katibu Mkuu Ndugu Fatma Gharib Bilal; Manaibu Makatibu Wakuu Ndugu Maua Makame Rajab na Ndugu Hassan Khatib Hassan; Kamishna, Katibu Mtendaji Baraza la Vijana; Ofisa Mdhamini Pemba Khadija Khamis Rajab; Wakurugenzi na Watendaji wa ngazi zote kwa mashirikiano makubwa wanayonipa katika kutekeleza majukumu yetu ya kila siku. *(Makofi)*

Nawaomba wazidishe mashirikiano na upendo baina yetu ili tuwatumikie wananchi kwa ari zote na kuleta maendeleo na kutekeleza majukumu yetu kwa ufanisi mkubwa.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja na Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

(Hoja ilitolea iamuliwe)

Kiambatanisho 1
MCHANGANUO WA FEDHA ZA MATUMIZI KWA MUJIBU WA PROGRAMU KUU NA PROGRAMU NDOGO KWA KIPINDI CHA JULAI 2016 HADI APRIL 2017

IDARA/PROGRAMU NDOGO	MAKADIRIO 2016/2017	UPATIKANAJI WA FEDHA JULY -APRIL 2017	ASILIMIA YA UPATIKANAJI WA FEDHA
Q0101: Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi	**527,540,485**	**63,225,650**	**12**
Q010101: Mfuko wa Uwezeshaji	41,230,000	19,628,250	48
Q010102: Usimamizi na Uimarishaji wa Vyama vya Ushirika	25,400,000	13,387,400	53
Q010103: Uratibu na Uendelezaji wa programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi	460,910,485	30,210,000	7
Q0102: Kukuza Usawa wa Kijinsia na Uendelezaji wa Wanawake	**490,090,000**	**475,894,066**	**97**
Q010201:Uratibu wa Masuala ya Usawa wa Kijinsia na Uendelezaji wa Wanawake	28,990,000	24,886,766	86
Q010201:Mapambano dhidi ya Udhalilishaji wa Wanawake na Watoto	461,100,000	451,007,300	98
Q0103: Kuimarisha Huduma za Ustawi	**5,410,440,000**	**3,652,470,200**	**68**
Q010301: Uratibu wa Huduma za Uhifadhi wa Jamii	5,072,960,000	3,316,992,800	65
Q010302: Maendeleo ya Vijana	337,480,000	335,477,400	99

Q0104: Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto	**6,410,898,465**	**5,479,571,877**	**85**
Q010401: Uratibu wa Mipango, Sera na tafiti za Wizara	75,000,000	18,190,000	24
Q010402: Utawala na Uendeshaji	3,013,009,650	2,476,971,677	82
Q010403:Uratinu na Utekelezaji wa Shughuli za Wizara Pemba	3,322,888,815	2,984,410,200	90
Q0104: Usimamizi wa Sheria za Kazi, Ukaguzi Kazi na Kazi za Staha kwa wote	**129,200,700**	**81,460,000**	**63**
Q010501:Uratibu na Upatikanaji wa Ajira za Staha	29,511,700	16,000,000	54
Q010501: Usimamizi wa Usalama na Afya Kazini	37,339,000	17,260,000	46
Q010503: Usimamizi wa Viwango vya Kazi vya Kimataifa na Majadiliano ya Pamoja Kazini	62,350,000	48,200,000	77
Jumla	**12,968,169,650**	**9,752,621,793**	**75**

Kiambatanisho 2

TAARIFA YA UKUSANYAJI MAPATO KWA MWEZI WA JULAI-APRIL 2016/ 2017 NA MAKADIRIO YA MAPATO KWA MWAKA 2017/2018

IDARA	KASMA NAMBA	CHANZO CHA MAPATO	MAKADIRIO YA MWAKA 2016/2017	UKUSANYAJI HALISI	ASILIMIA YA UTEKELEZAJI	MAKADIRIO 2017/2018
Kituo Cha Kukuza Wajasiri amali	1422088	Ada ya Mafunzo	11,975,000	-	-	20,000,000
Idara ya Vyama Vya Ushirika	1422036	Ada ya Uandikishaji Vyama Vya Ushirika	14,370,000	10,095,000	70	50,000,000
Idara ya Vyama Vya Ushirika	1422037	Ada ya Ukaguzi wa Vyama na Huduma	17,963,000	12,775,000	71	70,000,000
Idara ya Wazee na Ustawi wa Jamii	1422078	Ada ya Ukodishaji wa Ukumbi	9,580,000	6,360,000	66	30,000,000
Idara ya Ajira	1422071	Ukaguzi wa Maeneo ya kazi	47,901,000	29,625,000	62	65,901,000
Idara ya Usalama na Afya Kazini	1422012	Ada ya malipo ya ukaguzi katika Sehemu za Kazi	20,358,000	12,456,650	61	43,264,000
Kamisheni ya Kazi	1422075	Ada ya Ukaguzi wa Mikataba ya Ajira Nje ya Nchi	41,913,000	30,000,000	72	61,913,000
Kamisheni ya Kazi	1422011	Ada ya Vibali Vya Kazi kwa Wataalam wageni (Work Permit)	323,340,000	320,032,550	99	550,000,000
JUMLA			**487,400,000**	**421,344,200**	**86**	**891,078,000**

Kiambatanisho 3

UTOAJI WA MIKOPO, MFUKO WA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI KUANZIA JULAI,2016 HADI APRIL,2017

NA	WILAYA	IDADI YA MIKOPO	MIKOPO YA VIKUNDI	MIKOPO BINAFSI	SHEHIA	IDADI YA FEDHA ZILIZOTOLEWA	WALIONUFAIKA	JUMLA YA WANUFAIKA
							W'KE	W'ME
1	CHAKE CHAKE	25	13	12	9	32,500,000.00	157	101
2	MKOANI	31	8	23	5	25,742,000.00	101	87
3	WETE	27	7	20	6	28,900,000.00	63	82
4	MICHEWENI	26	4	22	6	26,700,000.00	81	65
	JUMLA NDOGO	**109**	**32**	77	**26**	**113,842,000.00**	**402**	**335**
5	MJINI	45	12	33	25	79,750,000.00	162	125
6	MAGHARIBI A	32	8	24	16	71,845,000.00	162	109
7	MAGHARIBI B	44	9	35	25	107,626,000.00	183	134
8	KASKAZINI "A"	29	6	23	12	50,100,000.00	97	76
9	KASKAZINI "B"	21	4	17	10	33,530,000.00	76	59
10	KATI	36	13	23	18	83,835,000.00	367	337
11	KUSINI	25	14	11	11	59,472,000.00	495	367

	JUMLA NDOGO	**232**	**66**	**166**	**117**	**486,158, 000.00**	**1542**	**1207**	**2 7 4 9**
	JUMLA KUU	**341**	**98**	**243**	**143**	**600,000, 000**	**1,944**	**1,542**	**3 , 4 8 6**

Kiambatanisho 4

UREJESHAJI WA MIKOPO MFUKO WA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI JULAI,2016 HADI

WILAYA	JULAI,2016	AGOSTI,.2016	SEPT,2016	OKT,2016	NOVE,2016	DESE,2016
CHAKE	1,085,500.00	3,684,000.00	3,363,000.00	1,935,000	1,778,000	**1,788,000**
MKOANI	1,557,000.00	1,931,000.00	1,975,000.00	1,509,500	1,354,000	**1,746,500**
WETE	2,413,500.00	2,478,000.00	2,102,000.00	1,620,500	1,546,000	**1,410,000**
M/WENI	1,054,000.00	1,919,000.00	1,622,500.00	2,459,000	1,757,000	**1,910,000**
J. NDOGO	**6,110,000.00**	**10,012,000.00**	**9,062,500.00**	**7,524,000**	**6,435,000**	**6,854,500**
MJINI	4,225,500.00	7,799,500.00	4,690,000	6,171,500	7,374,000	4,513,000
MAGH A	3,117,500.00	3,378,300.00	2,722,000.00	3,045,000	2,002,500	2,355,000
MAGH.B	4,648,000.00	8,282,000.00	5,839,000.00	7,407,000	4,445,000	5,138,000
KASK"A"	3,702,500.00	4,126,500.00	3,439,500.00	3,059,500	4,134,500	3,530,000
KASK "B"	2,064,000.00	3,987,000.00	3,090,000.00	2,867,500	2,835,000	3,028,000
KATI	3,325,000.00	4,399,000.00	3,967,000.00	5,096,000	3,759,000	3,893,000

KUSINI	4,007,000.00	4,059,000.00	3,777,000.00	3,648,000	3,065,000	7,888,000
J.NDOGO	**25,089,500.00**	**36,031,300.00**	**27,524,500.00**	**31,294,500**	**27,615,000**	**30,345,000**
J.KUU	**31,199,500.00**	**46,043,300.00**	**36,587,000.00**	**38,818,500**	**34,050,000.00**	**37,199,500.**

Kiambatanisho 5

UKAGUZI WA KUMBUKUMBU ZA HESABU 2016/2017

UNGUJA	PEMBA	ZYMC	JUMLA
518	364	80	962

Kiambatanisho 6

UNGUJA.

SACCOS POTFOLIO HADI MACHI, 2017

S/N.	Wilaya	Saccos	Hisa	Akiba	Amana	Jumla Mtaji
1	**Urban District**	36	1,076,762,903	4,166,271,336	181,118,207	5,424,
2	**West "A"**	10	44,019,628	291,211,985	68,932,031	404,16
3	**West "B"**	18	242,398,431	1,868,363,115	350,300,330	2,461,
4	**North "A"**	29	100,325,000	65,045,920	8,107,000	173,47
5	**North "B"**	13	39,564,701	147,793,569	32,856,900	220,21
6	**Central**	23	60,551,690	198,070,230	20,436,300	279,05
7	**South**	9	36,389,200	53,272,888	20,838,000	110,50
	JUMLA	**138**	**1,600,011,553**	**6,790,029,043**	**682,588,768**	**9,072,**

Kiambatanisho 7
SACCOS POTFOLIO HADI MACHI, 2017
PEMBA

S/N.	Wilaya	Saccos	Hisa	Akiba	Amaan	Jumla ya Mtaji	Mko
							Iliyo
1	Wete	25	74,972,500	456,469,752	10,778,500	542,220,752	772,5
2	Micheweni	12	28,105,000	120,126,600	6,122,000	154,353,600	166,8
3	Mkoani	19	32,474,000	313,911,931	4,632,100	351,018,031	376,5
4	Chake chake	36	89,647,750	1,044,258,944	4,560,000	1,138,466,694	1,660
	TOTAL	**92**	**225,199,250**	**1,934,767,227**	**26,092,600**	**2,186,059,077**	**2,976**
JUMLA KUU		**230**	**1,825,210,803**	**8,724,796,270**	**708,681,368**	**11,258,688,441**	**24,**

Kiambatanisho 8
VYAMA VIKUU VILIVYOSAIDIWA NA PROGRAMU YA MIVARF

	JINA LA USHIRIKA	GHARAMA MRADI	75%	25%	
				WALICHOLIPA	TOFAUTI
	MTULE AMCOS	100,000,000/-	75,000,000/-	9,000,000/-	16,000,000/-
	UWAMIJICHWA	31,000,000/-	23,250,000/-	800,000/-	6,950,000/-
	TUSIYUMBISHANE	31,000,000/-	23,250,000/-	3,500,000/-	4,250,000/-
	JUMLA	**162,000,000/-**	**121,500,000/-**	**13,300,000/-**	**27,200,000/-**

Kiambatanisho 9
ORODHA YA MALALAMIKO YA WANAWAKE YALIYORIPOTIWA UNGUJA NA PEMBA.

WILAYA	Kutelekezwa na mume	Migogoro ya ndoa	kupigwa	Madai ya mali baada ya kuachana	Kupewa ujauzito	Madai ya mahari	Migogoro ya familia	Madai ya shamba na nyumba.	Kukatishwa masomo.	Kubakwa.	Madai ya fedha.	Shambulio la matusi.	Msaada wa makaazi.	Shambulio la mwili.	Kutoroshwa.
MJINI	3		2		2			1	1	2					
MAGHARIBI“A”		3	2	1		2	3			1		2	1	1	
MAGHARIBI “B”	7	4	1		1			1		1		1		1	1
KATI				1	1	1									
KUSINI	5		5		2					2					
KASKAZINI “A”	30		6												
KASKAZINI “B”	5									3				2	4
CHAKECHAKE	4	7	7												
MKOANI	2	1	1												2
WETE		4	2			2	1								
MICHEWENI	2		2			2	2								
JUMLA															

Kiambatanisho 10a
MATUKIO YA UDHALILISHAJI YALIYORIPOTIWA KATIKA KITENGO CHA HIFADHI YA MTOTO, UNGUJA NA PEMBA MWEZI WA JULAI 2016-MACHI 2017

MWEZI	KESI ZA MATUNZO	KESI ZA MVUTANO WA MALEZI	JUMLA
JULAI	4	4	8
AGOSTI	8	6	14
SEPTEMBA	7	9	16
OKTOBA	5	10	15
NOVEMBA	6	12	18
DISEMBA	14	4	18
JANUARI	16	18	34
FEBUARI	9	9	18
MACHI	18	14	32
JUMLA	**87**	**86**	**173**

Kiambatanisho 10b
MATUKIO YA UDHALILISHAJI YALIYORIPOTIWA KATIKA KITENGO CHA HIFADHI YA MTOTO, PEMBA
MWEZI WA JULAI 2016-APRILI 2017.

MWEZI	KESI ZA MATUNZO	KESI ZA MVUTANO WA MALEZI	JUMLA	MAELEZO/HATUA
JULAI	2	5		Katika matukio hayo, matukio 53 yamepatiwa ufumbuzi kwa wazazi kukubaliana kutunza watoto wao 1 yamefanyiwa rufaa Mahakama ya Kadhi, 10 hawakurudi tena na kukubaliana kifamilia na 29 hatua zinaendelea
AGOSTI	2	7	9	
SEPTEMBA	4	2	6	
OKTOBA	1	1	2	
NOVEMBA	8	5	13	
DISEMBA	1	5	6	
JANUARI	13	7	20	
FEBUARI	9	9	18	
MACHI	15	4	19	
APRILI	5	1	6	
JUMLA	**51**	**42**	**93**	

Kiambatanisho 11

WATOTO WANAOISHI KATIKA MAZINGIRA MAGUMU ZAIDI WALIOTAMBULIWA NA KUSAJILIWA 2017

SHEHIA	WANAUME	WANAWAKE	JUMLA
UNGUJA			
KWA WAZEE	26	19	45
JANG'OMBE	28	28	56
MWEMBE MAKUMBI	14	8	22
MAGOMENI	36	29	65
NYERERE	28	36	64
KIDONGO CHEKUNDU	8	13	21
JUMLA	**140**	**133**	**273**
PEMBA			
PUJINI	44	44	88
WAWI	0	20	20
TIBIRINZI	60	64	124
CHANJAANI	39	60	99
WARA	29	44	73
KICHUNGWANI	16	22	38
MSINGINI	39	45	84
ZIWANI	57	50	107
CHACHANI	9	10	19
MJINI OLE	34	32	66
JUMLA	**327**	**391**	**718**
JUMLA KUU	**467**	**524**	**991**

Kiambatanisho 12

MUHTASARI WA MAKADIRIO YA FEDHA KWA PROGRAMU KUU NA
NDOGO KWA MWAKA 2017/2018

IDARA/PROGRAMU NDOGO	MAKADIRIO 2017/2018
Q0101: Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi	**1,212,671,000**
Q010101: Mfuko wa Uwezeshaji	232,486,000
Q010102: Usimamizi na Uimarishaji wa Vyama vya Ushirika	380,082,000
Q010103: Uratibu na Uendelezaji wa Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi	600,103,000
Q0102: Kukuza Usawa wa Kijinsia na Uendelezaji wa Wanawake	**302,702,000**
Q010201:Uratibu wa Masuala ya Usawa wa Kijinsia na Uendelezaji Wanawake	247,602,000
Q010201:Mapambano dhidi ya Udhalilishaji wa Wanawake na Watoto	55,100,000
Q0103: Kuimarisha Huduma za Ustawi	**8,942,360,000**
Q010301: Uratibu wa Huduma za Uhifadhi wa Jamii	8,514,997,000
Q010302: Maendeleo ya Vijana	427,363,000
Q0104: Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto	**2,943,297,000**
Q010401: Uratibu wa Mipango, Sera na tafiti za Wizara	427,838,000
Q010402: Utawala na Uendeshaji	1,685,551,000
Q010403:Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Wizara Pemba	829,908,000
Q0104: Usimamizi wa Sheria za Kazi, Ukaguzi Kazi na Kazi za Staha kwa wote	**1,055,610,000**
Q010501:Uratibu wa upatikanaji wa Ajira za Staha	213,484,000

Q010501: Usimamizi wa Usalama na Afya Kazini	233,530,000
Q010503: Usimamizi wa Viwango vya Kazi vya Kimataifa na Majadiliano ya Pamoja Kazini	608,596,000
Jumla	**14,456,640,000**

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Waziri kwa uwasilishaji wa hotuba yako. Waheshimiwa Wajumbe sasa nitamwita Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo, Wanawake, Habari na Utalii. *(Makofi)*

Mhe. Maryam Thani Juma: (Kny. Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo, Wanawake, Habari na Utalii): Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii naomba kusoma Hotuba ya maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii kuhusiana na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto kwa mwaka wa fedha 2017/2018. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, Mwingi wa Rehma, kwa kutujaalia uzima na afya njema tukaweza kukutana tena katika Baraza hili la Tisa kwa ajili ya kuendelea kuwatumikia wananchi wetu. Aidha, namshukuru Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Baraza kwa kuliongoza Baraza hili tukufu, ninaamini kwamba mtaliongoza Baraza hili kwa uadilifu wa hali ya juu na kuimarisha Demokrasia katika chombo hiki muhimu cha wananchi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru na kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein, kwa kutimiza ahadi yake ya kuongeza mishahara kwa watendaji wote wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kama alivyoahidi katika kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Zanzibar uliopita. Napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza Wawakilishi wote waliomo katika Baraza lako tukufu ni wazi kwamba wananchi wamejenga imani kubwa kwetu, nasi ahadi yetu kwao ni kwamba tutawatumikia kwa dhati kama ambavyo walivyotuamini kutuleta katika chombo hiki kwa lengo la kutetea maslahi yao. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, sina budi pia kumshukuru Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto na Naibu wake pamoja na watendaji wote wakiongozwa na Katibu Mkuu pamoja na watendaji wa Wizara ya Fedha

na Mipango kwa mashirikiano waliyotupa wakati wa kupitia makadirio ya Bajeti ya Wizara hii, lakini pia nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati yetu kwa umoja wao na kazi nzuri waliyoifanya kiasi cha kunirahisishia kazi ya kuongoza kikao kuwa nyepesi zaidi, kwa hakika ni wajumbe Mahiri, wameweza kuijadili ipasavyo na kuhoji mambo mbali mbali kwa lengo la kuhakikisha kwamba fedha wanazoidhinishwa kwa Wizara hii zinatumiwa kwa matumizi yaliyokusudiwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima ya hali ya juu napenda kuwatambua Wajumbe hao kwa majina kama hivi ifuatavyo:

1.	Mheshimiwa Ali Suleiman Ali (Shihata)	Mwenyekiti
2.	Mheshimiwa Salha Mohammed Mwinjuma	Makamu Mwenyekiti
3.	Mheshimiwa Hassan Khamis Hafidh	Mjumbe
4.	Mheshimiwa Maryam Thani Juma	Mjumbe
5.	Mheshimiwa Zaina Abdalla Salum	Mjumbe
6.	Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub	Mjumbe
7.	Mheshimiwa Mussa Foum Mussa	Mjumbe
8.	Ndugu Himid Haji Choko	Katibu
9.	Ndugu Haji Jecha Salum	Katibu
10.	Ndugu Amina Abeid	Mkalimani

Mhe. Mwenyekiti, ikumbukwe kwamba miongoni mwa majukumu ya msingi ya Kamati yetu ni kuchambua mapendekezo ya Serikali kuhusu makadirio ya Wizara husika ya mapato na matumizi ya kazi za kawaida na kazi za maendeleo kwa mwaka, hivyo katika kutekeleza jukumu hilo lililoelezwa katika kanuni ya 106(a), Kamati yangu ilikaa na kujadili na hatimae kupitisha Makadirio ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto tarehe 05/05/2017 na leo hii kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Kamati nawasilisha maoni ya Kamati yangu kuhusiana na Bajeti hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo mfupi sasa naomba nichukue fursa hii adhimu kutekeleza jukumu lililonileta hapa mbele ya Baraza lako tukufu moja kwa moja.

MFUMO WA BAJETI WA PBB

Mhe. Mwenyekiti, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuanzia mwaka wa fedha 2015/2016 ilianzisha mfumo wa bajeti unaozingatia programu yaani *Program Based Budget (PBB)* ambapo bajeti hii imetumia mfumo huo huo. Hata hivyo, licha ya kuwa mfumo huu ulikwishaanza kutekelezwa katika mwaka wa fedha

uliopita, bado unaonekana kuwa mgumu kufahamika miongoni mwa Wajumbe na imekuwa ni changamoto kwao na kupelekea ugumu kidogo kuweza kumudu kufanya uchanganuzi wa vitabu vya Bajeti vilivyoletwa katika Kamati zako, hata hivyo wamejitahidi kadiri ya uwezo wao kuweza kuchambua bajeti hiyo kwa msaada wa watendaji wetu na Wizara ya Fedha na Mipango ambao kwa kweli tunawashukuru sana.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ina fungu moja (1) ambalo ni Q01 na imepanga kutekeleza Programu kuu tano (5) zenye Programu ndogo kumi na tatu (13) ambapo kwa ujumla Fedha iliyoombwa kwa Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto ni Tshs. 14,456,640,000 (Bilioni kumi na nne, Mia nne hamsini na sita milioni na laki sita na arobaini).

Zifuatazo ni Programu kuu:

1. Programu ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.
2. Programu ya Kukuza Usawa wa Kijinsia na Uendelezaji Wanawake.
3. Programu ya Kuimarisha Huduma za Ustawi.
4. Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya KUWVWW.
5. Programu ya Usimamizi wa Sheria za Kazi, Ukaguzi Kazi na kazi za Staha kwa wote.

Mhe. Mwenyekiti, katika hotuba hii, nitazungumzia mambo ya msingi yafuatayo ambayo Wizara inatarajia kuyatekeleza katika bajeti ya mwaka wa fedha 2017/2018:

PROGRAMU KUU YA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu imeridhika na makadirio yaliyopangwa katika programu kuu ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na ilipendekeza mambo mbali mbali, ambayo yatakapozingatiwa yataboresha kwa kiasi kikubwa. Miongoni mwa mambo hayo ni:

(a) Serikali kuzipa kipaumbele bidhaa zinazozalishwa na wajasiriamali pale yanapofanyika manunuzi katika taasisi au shughuli za kiserikali.

(b) Wizara iandae Sera maalumu itakayowataka wawekezaji hususani wa mahoteli kununua na kutumia bidhaa zinazozalishwa na wajasiriamali wa Zanzibar ili kukuza soko la bidhaa zao.

(c) Wizara, mbali ya kuwawezesha kifedha, iwasaidie kutafuta vitendea kazi kama vile mashine pamoja na kuwapa utaalamu utakaowawezesha kuboresha shughuli zao.

Mhe. Mwenyekiti, aidha, Kamati inatoa msisitizo kwa Wizara ihakikishe kuwa inaongeza juhudi zake, katika kuwasaidia wananchi inaowawezesha kwa kuwatafutia masoko ya bidhaa wanazozalisha na kulitafutia ufumbuzi tatizo la vifungashio na usindikaji *(packaging)* wa bidhaa wanazozalisha, ili ziweze kukidhi viwango vya kitaifa na kimataifa hali itakayopelekea kupata soko la uhakika na vilevile, kurudisha fedha walizokopeshwa kwa wakati. Kamati inaishauri Wizara kuongeza bidii ya kufuatilia mikopo iliyotoa kwa ajili ya kuboresha marejesho hali itakayoweza kuwanufaisha watu wengine.

Mhe. Mwenyekiti, Programu kuu ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi imetengewa jumla ya Tshs. 1,212,671,000 (Bilioni moja, Milioni mia mbili na kumi na mbili, Laki sita na sabini na moja elfu) kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Kamati yangu inaliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha matumizi ya fedha hizo ili Wizara iweze kutekeleza yale inayokusudia kuyatekeleza katika mwaka wa fedha 2017/2018.

PROGRAMU NDOGO YA MAPAMBANO DHIDI YA UDHALILISHAJI WA WANAWAKE NA WATOTO

Mhe. Mwenyekiti, wizara katika kipindi cha utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2016/2017 ilijitahidi sana pamoja na mambo mengine kupunguza vitendo vya udhalilishaji wanawake na watoto. Kwa kuwa, bado vitendo hivyo vinaendelea katika jamii yetu, hivyo, Kamati inaliomba Baraza hili tukufu kuikubali na kuidhinisha bajeti ambayo Wizara imeiwasilisha mbele yetu ili waendelee na juhudi zao za kutokomeza kabisa vitendo hivyo na kuirudishia heshima nchi yetu kama ilivyokuwa hapo awali.

Mhe. Mwenyekiti, Programu ndogo ya Mapambano dhidi ya Udhalilishaji wa Wanawake na Watoto imetengewa jumla ya Tshs. 55,100,000 (Milioni hamsini na tano na Laki moja) katika mwaka wa fedha 2017/2018. Hata hivyo, Kamati inadhani kwamba kiwango hicho cha fedha ni kidogo kulingana na uwepo wa vitendo hivyo pamoja na mapambano yanayohitajika katika kutokomeza kabisa vitendo hivyo nchini. *(Makofi)*

PROGRAMU KUU YA KUIMARISHA HUDUMA ZA USTAWI

Mhe. Mwenyekiti, Kamati inatoa pongezi za dhati kwa Wizara kwa namna ilivyoweza kutekeleza majukumu yake juu ya ustawi wa jamii. Hata hivyo, Kamati inaishauri Wizara kuhakikisha kuwa inalipa deni linalohusiana na fidia kwa wale wote wanaodai. Aidha, Wizara ihakikishe kuwa inaweka utaratibu wa kulipa madeni kwa wakati ili kuepuka malimbikizo ya madeni ambayo Wizara hushindwa kulipa kwa wakati na kusababisha usumbufu kwa waathirika. Vilevile, Kamati inaishauri Wizara kuhakikisha kuwa inaweka utaratibu mzuri wa malipo na uhifadhi wa fedha za pencheni jamii ili kuepuka matumizi mabaya ya fedha hizo na kuodosha dhana ya ubadhirifu wa fedha hizo ambayo imejengeka miongoni mwa jamii yetu.

Mhe. Mwenyekiti, Programu kuu ya Kuimarisha Huduma za Ustawi imetengewa Tshs. 8,942,360,000 (Bilioni nane, Milioni mia tisa na arobaini na mbili, Laki tatu na sitini elfu) kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha fedha hizo ili Wizara iweze kutekeleza yale iliyojipangia.

PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA KAZI, UWEZESHAJI, WAZEE, VIJANA, WANAWAKE NA WATOTO

Mhe. Mwenyekiti, katika nyakati tofauti, Kamati yangu ilibaini changamoto zifuatazo katika baadhi ya ofisi za Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto Unguja na Pemba:

(a) Upungufu wa watendaji/wataalamu katika Idara ya Ajira na Idara ya Usalama na Afya Kazini.
(b) Ufinyu wa ofisi za kufanyia kazi.
(c) Uhaba wa vitendea kazi.

Hivyo, Kamati inaishauri Wizara ichukue hatua za haraka kukabiliana na changamoto hizo ili Idara hizo ziweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo katika kuleta maendeleo nchini.

Mhe. Mwenyekiti, Program kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto imetengewa jumla ya Tshs. 2,943,297,000 (Bilioni mbili, Milioni mia tisa na arobaini na tatu, Laki mbili na tisini na saba elfu) katika mwaka wa fedha 2017/2018. Kamati yangu inaliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha matumizi ya fedha hizo ili Wizara

iweze kutekeleza yale inayokusudia kuyatekeleza katika mwaka wa fedha 2017/2018.

PROGRAMU NDOGO YA URATIBU WA UPATIKANAJI WA AJIRA ZA STAHA KWA WOTE

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu imeridhika na makadirio yaliopangwa katika programu hii kwa vile suala la upatikanaji wa ajira ni muhimu sana katika nchi yetu kutokana na uwepo wa idadi ya watu na vyanzo kidogo vya ajira. Kimsingi, uwezo wa Serikali wa kutoa ajira kwa wananchi wote ni mdogo. Hivyo, katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara ilitafuta na kuratibu ajira kutoka nchi za nje kama vile Oman na Qatar. Hata hivyo, Kamati inaishauri Wizara kuongeza bidii katika kufanikisha upatikanaji wa vijana wenye sifa zinazohitajika kwa ajili ya nafasi 100 za ajira zilizotolewa na Qatar ili Zanzibar isipoteze fursa hiyo adhimu na kujenga uaminifu nje ya nchi.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati inachukua fursa hii kuliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya Tshs. 213,484,000 (Milioni mia mbili na kumi na tatu, Laki nne na themanini na nne elfu) kwa ajili ya utekelezaji wa Programu hii ndogo na kuiwezesha Wizara kufikia malengo waliyojipangia ikiwemo kutafuta, kufuatilia na kuratibu ajira zaidi.

PROGRAMU NDOGO YA USIMAMIZI WA USALAMA NA AFYA KAZINI

Mhe. Mwenyekiti, licha ya mambo mbalimbali yaliyotekelezwa na Wizara katika mwaka wa fedha 2016/2017, Kamati yangu inaishauri Wizara kuandaa mipango madhubuti itakayowezesha waajiri kutekeleza kwa ukamilifu Sheria ya Usalama na Afya Kazini, nambari 8 ya mwaka 2005. Kama Sheria hiyo ina mapungufu au inahitaji kutungiwa Kanuni ni vyema Wizara ikaweza kuyabaini hayo na kuifanyia marekebisho ili waajiri wote waweze kutekeleza ipasavyo.

Aidha, Kamati inashauri Wizara iangalie uwezekano wa kuzitaka taasisi za umma au binafsi hususani zenye mazingira hatarishi ya kufanyia kazi ziwawekee bima ya afya wafanyakazi wao.

Mhe. Mwenyekiti, programu ndogo ya Usimamizi wa Usalama na Afya Kazini imepangiwa jumla ya Tshs. 233,530,000 (Milioni mia mbili na thelathini na tatu, Laki tano na thelathini elfu) kwa mwaka wa fedha *2017/2018*. Kamati yangu inaliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha matumizi ya fedha hizo ili

Wizara iweze kutekeleza yale inayokusudia kuyatekeleza katika mwaka wa fedha 2017/2018.

PROGRAMU NDOGO YA USIMAMIZI WA VIWANGO VYA KAZI VYA KIMATAIFA NA MAJADILIANO YA PAMOJA KAZINI

Mhe. Mwenyekiti, programu ndogo hii ina lengo kuu la kuhakikisha kwamba kunakuwepo utekelezaji mzuri wa sheria za kazi nchini.

Mhe. Mwenyekiti, kamati inaipongeza sana Wizara kwa kusimamia utekelezaji wa Sheria za kazi pamoja na hatua ilizozichukua dhidi ya kukomesha ajira mbaya kwa watoto nchini. Hata hivyo, Kamati yangu bado inaiomba Wizara ihakikishe kwamba inaendelea na juhudi zake za kutokomeza kabisa ajira mbaya kwa watoto nchini hususani katika maeneo ya ubanjaji kokoto na uchimbaji matofali huko Micheweni, Pemba ili watoto hao wapate haki zao za msingi ikiwemo elimu. Katika mzunguko wa Kamati uliopita wa kufuatilia utekelezaji wa shughuli zinazotekelezwa na Wizara, ilishuhudia watoto wakiwa katika ajira mbaya ambao ni dhahiri wanakosa haki zao za msingi kama vile elimu, afya na wengine kuathirika na ndoa za utotoni.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2017/2018, program ndogo hii imepangiwa kiwango cha Tshs. 608,596,000 (Milioni mia sita na nane, laki tano na tisini na sita elfu). Hivyo, Kamati yangu inaliomba Baraza lako tukufu kujadili na kuidhinisha fedha hizo ili Wizara iweze kutekeleza majukumu yake ili kuweka hatma njema ya watoto wetu.

Mhe. Mwenyekiti, Mwisho, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru tena kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maoni ya Kamati yangu kwa niaba ya Kamati pamoja na kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa kunisikiliza. Sasa niwaombe Wajumbe wa Baraza lako tukufu waijadili na hatimaye waiunge mkono bajeti hii ili wamuwezeshe Mhe. Waziri kufanikisha na kutekeleza yale waliojipangia katika mwaka huu wa fedha 2017/2018.

Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba yangu na kwa niaba ya Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii naunga mkono hoja hii, na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mheshimiwa kwa hotuba yako nzuri na uwasilishaji mzuri. Sasa Waheshimiwa tunaendelea kuanza kuchangia hotuba ya bajeti hii kwa kuanza na Mhe. Suleiman Sarahan Said na baadaye atafuatia na Mhe. Omar Seif Abeid na akifuatiwa na Mhe. Hassan Khamis Hafidh.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kunipatia fursa hii adhimu kwa ajili ya kuchangia hotuba ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee Vijana Wanawake na Watoto.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa kazi yake nzuri anayoifanya katika juhudi zake za kuhakikisha kwamba tunalisukuma gurudumu hili likiwa salama usalimini.

Mhe. Mwenyekiti, mimi namuomba Mhe. Waziri atakapokuja katika kifungu cha 45 na 46 ukurasa wa 34 kifungu kinachosema "Programu Ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba". Nimeiona humu kuna uratibu wa Shughuli ya Wizara ya Pemba ili kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka 2017/18 anaomba milioni 829,908 kwa ajili ya matumizi ya program na mishahara Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, ningemuomba Mheshimiwa atakapokuja anipe ufafanuzi mishahara yao itakuwa ni kiasi gani ili hili fungu libakishwe katika uendeshaji. Wakati tunakwenda pale kuangalia angalia utasikia wanasema kwamba bajeti ndogo, mambo yanakuwa hivi. Sasa hatuwezi kuelewa hapa sijaona kwamba hasa mishahara yao inakuwa kiasi gani ili lile fungu lililobakia liweze kutekelezeka. Bado hali ya masuala ya unyanyasaji Pemba yanahitaji ufatiliaji sana. Ikiwa Wizara itakuwa haina bajeti nzuri ya ufatiliaji itakuwa kama itakuwa ndio tunapalilia hii hali itaendelea. Maana yake muhusika atakapokuwa anashindwa kwenda kufatilia mambo yake basi hali inaweza ikawa ya ziada ikiwa itakuwa mtu anaanza kuchoka kwa kufatilia.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka niingie hapo hapo katika suala hili la unyanyasaji. Mimi nafikiri sijui niseme hii ni laana au sijui tumekutwa na jambo gani. Masuala haya kadiri tunavyoyapigia mbio, kadiri tunavyokuwa tunayatolea elimu, lakini sijui kwa nini bado kasi yake haijapungua zaidi ya kuendelea.

Mhe. Mwenyekiti, katika utafiti wako Waziri sijui umegundua ni tatizo gani ambalo anaweza akatushauri au akatwambia tumefikwa na nini katika utafiti wako. Haiwezekani kwa sababu kama sasa hivi miundombinu ya wanawake ilivyo, lakini bado utamkuta mtu anachukua mtoto wa miaka miwili, mwaka mmoja, sijui anakwenda kutafuta nini zaidi ya laana hii inayotufika. Itakuwa wewe Mhe. Waziri umeshakaa na timu yako kuangalia ni tatizo gani hasa linalotufika mpaka kadhia hii bado ikawa haijatuwacha.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi kila mtu anaogopa ile heshima ya zamani iliyokuwa ukimkuta mzazi wa mwenzako unampokea mkoba, badala kukwita umpelekee mkoba nyumbani kwake umpokee wewe unamkimbia. Mheshimiwa tumefika mahali pabaya, unaweza ukamuona mtu anamwita kijana ampelekee mkoba akaenda mbio, anaogopa kwa sababu ameshatahadharishwa. Heshima yetu pia imeondoka ile ya Uzanzibari ya kupokeana mikoba na kumpelekea mtu nyumbani kwake. Naomba sana kwamba Waziri atakapokuja pengine anaweza akatufafanulia.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nimueleze Mhe. Waziri kwamba kuna matatizo mengi ambayo sasa hivi yanatukuta sana na kigezo ni umri. Utakapokuja Mhe. Waziri naomba utuletee ufafanuzi wa umri, mtoto mchanga anaanzia siku ngapi mpaka muda gani, mtoto mwengine anaanzia muda gani mpaka muda gani, nataka utufafanulie kuanzia mtoto wa siku moja mpaka mzee wa miaka mia tunamwitaje katika hoja hii. Tena utuletee ufafanuzi kiserikali au kimataifa kwamba miaka huyu ni hii haki yake ni hii. Maana mpaka sasa hivi unamuona mtu anabaleghe kwa miaka 15, lakini sheria inamchukulia mpaka afike miaka 18 ndio aonekane mtu mzima. Sijui mnatupelekaje hapa, mtu mzima miaka 15, 18, 21, 40 hebu tufafanulie utakapokuja, kidogo kwa sababu hizi sheria zinatupa tabu.

Mhe. Mwenyekiti, unamkuta mtu anafanya vitendo lakini anashabihia umri kwamba ndiyo unaomlinda. Utakapokuja naomba kidogo utufafanulie umri wa kisheria ambao mtoto mdogo, mtoto wa siku moja, mtoto mkubwa, mtu mzima, baleghe wote hawa wanakwenda na miaka mingapi ambayo tunakwenda nayo. Halafu vilevile uweze kutufafanulia kwamba hawa watu wazima mpaka miaka mingapi wanapotea akili. Maana kuna watu wengine wanafika miaka 70 ukimkamata unaambiwa akili zimeshaondoka. Sasa huyo ana akili zimeshaondoka kwa muda gani? Ningeomba hapo utufafanulie hilo.

Mhe. Mwenyekiti, katika ukurasa wa 26, Programu hii ambayo ni Programu ya Mapambano Dhidi ya Udhalilishaji wa Wanawake na Watoto. Programu hii ina lengo la kukuza muitikio na kuratibu mapambano dhidi ya vitendo vya ukatili na udhalilishaji wanawake na watoto nchini kwa mwaka 2016/17 Wizara kupitia programu hii.

Mhe. Mwenyekiti, huku kuna mambo mengi sina haja ya kupoteza muda, ila utakapokuja mimi nataka utuangalie mikataba yetu ambayo tumeitengeneza kwa ajili ya ndoa. Wakati wa kufunga ndoa ni wepesi sana na ni wazuri sana wa kupeleka mikataba ya kwenda kufunga ndoa. Lakini mkataba wa kuvunja ndoa haupo, mtu anamwambia tu toka na watoto wako anakwenda zake.

Mhe. Mwenyekiti, tusiwe tunacheza ngoma ikawa kama ngoma ya kasa, juu humuoni kumbe ndani tunacheza wenyewe. Itakuwa nyama ya kasa tutakuja kucheza mpaka ndani ya sufuria, maisha tutakuwa hatujui matatizo yanayotukabili. Mhe. Waziri utakapokuja hapa hebu tuletee sheria ya kutubana utwambie ukweli kwamba mtu wakati wa kuoa, sherehe, vifijo na washauri wanakuwa wengi na mazogo mengi. Wakati wa ndoa kuvunjika hapana ushauri tena, mama kuondoka na watoto wake.

Mhe. Mwenyekiti, kadhia hii unaweza ukawakuta Wakurugenzi wamo humo, Wawakilishi wamo humo, halafu wanawatelekeza watoto, kwa nini mshahara wake usikamatwe. Huu uwe ni mkataba wa kweli, siyo anakwenda pale unamwita baada ya mwezi mmoja, miezi miwili haonekani tena mshahara unachukuliwa na anakwambia niite popote mimi siogopi. Hii itakuwa bado watoto hawa ndio watoto wa mitaani na hawa ndio wanaozidisha balaa kila siku na matatizo ya kila siku. Lakini kama tunawaachia ndio tunawatengeneza halafu tukisema watoto wanafanyaje wakati tunatengeneza sisi na sababu ni wanaume. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, hajalazimishwa mtu kwenda kuowa wake wanne wala sita, sheria ya kiislamu inasema mmoja kama unaona bado uongeze wapili, kama unaona bado watatu, lakini kwa kujiweza, siyo kwamba uwende ukaoe tu. Mimi ninachotaka kukwambia kwamba ufatiliaji wa wajane pamoja na watoto. Baba akishakujenga nyumba yake na kumaliza siku ya pili ana mtoto mama yule anakwenda kuweka ngoma mpya tena anajisifu hasa naweka ngoma mpya. Sasa naomba kama ngoma mpya kwanza nusu ibakie kwa yule mama mkongwe halafu ngoma mpya nyengine achukuwe yeye.

Mhe. Mwenyekiti, hapa naomba tupatizame sana vyenginevyo itakuwa kila siku tunapiga kelele hatufiki mwisho. Mama huyu hana uwezo wa kuwalisha watoto, hana uwezo wa kuwasomesha watoto hana uwezo wa kuwalinda watoto. Sasa ningekuomba tuangalie mikataba yetu ya mwanzo. Mimi nataka niseme kitu kimoja, wewe unakwenda kumchukua mtu kigori kwao, mtoto mdogo kabisa, unafika pale wewe huna kitu, unamwambia tuandae maisha Mungu atatujaalia unampiga blaa blaa, unampiga muhogo mtupu, unampiga sembe tupu, yeye anastahamili tujenge nyumba, tununue na gari tumalize.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya miaka mitano mpaka miaka kumi yule mtoto keshakuwa kibibi kizee mpaka meno hana kwa kustahamilia wewe. Leo anaachwa baba yule keshapata nyumba, keshapata gari, keshapata kila kitu. Kwa nini huyu hagaiwi mali zake na yeye akapewa. Huyu unamuacha ndio kibogoyo, unamrudisha kwao na makofi juu. Serikali haiwezekani, lazima

Mhe. Waziri tuhakikishe hili suala yule mtoto uliyemchukua kwao haki yake iko wapi? Ile miaka yote aliyekuja akakustahamilia miaka yote amekaa na wewe miaka 15 miaka 20 kila kitu kila unaloona amekustahamilia halafu haki yake yote uliyompotezea muda wake iko wapi. Uislamu gani unaosema hivyo, hakuna. Huyu Mheshimiwa aandikiwe mali zake alizonazo wakimalizana wagawe mbao kila mmoja fungu lake mmoja gari, mmoja nyumba, atajua mwenyewe kama ataanza tena na kigori mpya sawa lakini zile wagawane. Mhe. Waziri ningekuomba sana uwatafutie nafasi hapa wanawake wapate fungu lao.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika suala moja, mimi nakushauri sijui itakuwaje lakini Mheshimiwa tuna wanawake akina mama kwa bahati mbaya hufanya makosa kwa bahati mbaya wanakwenda jela. Kule anakaa jela pengine na ujauzito mpaka anajifungua. Akishakujifungua akitoka tu siku ile aliyefungwa ni mama yule mtoto hafungwi jela yule si mfungwa lakini kwa imani ya yule mama kutupatia mtoto, kwa imani ya kumjengea yule mtoto tusimjengee mazingira ya jela, kwa nini serikali hapa haimfutii kesi yake akenda nyumbani kwenda kumlea mtoto yule. Tunawasamehe wangapi kwa nini huyu asisamehewe.

Mhe. Mwenyekiti, ningemuomba Mhe. Waziri huyu mtoto hana makosa ni kiumbe cha Mungu, Malaika ameletwa lakini tukimuendeleza mama akae jela akiwa kafungwa tunamjengea mazingira ya jela kuanzia siku ya kwanza mpaka siku ile. Kwa hivyo ningekuomba sana Mhe. Waziri tukalitizama fungu hili tukalileta kuweza kulisaidia kwamba mama akishakujifungua, ni kama vile mafungu mengine katika Uislamu tuna eda, tuna mambo ya kufiliwa na mume. Lakini ninavyofikiria, wenzetu hapa wenye elimu kubwa ya ufafanuzi wa dini, kwamba siku mama anayojifungua hata kama mumewe kafa jana ina maana ile eda imekwisha au kama aliachwa bado siku 5 au 10, hana tena, anajisafisha anakuwa yule mama ni msafi ni mweupe.

Ningeomba na hili kwa wale wenye kufanya makosa, kwa sababu nataka niseme kwamba sehemu yetu ya Zanzibar hatuiti jela tunaita ni Chuo cha Mafunzo. Marehemu Mzee Abeid Karume ameileta kwa maana yake kwamba mtu anapokwenda jela asiende kwamba yule ni msugu, asende kama ana matatizo. Yule atakuwa ameshindwa na uwelewa kwa hivyo amekwenda kule apatiwe uwelewa ili akirudi huku asirudie makosa yale. Mimi siamini kama mjamzito akishakujifungua akajua faida yake na matatizo yake na ameshapata mtoto sifikirii kama atarudia kosa lile, lakini tumtizame na yule mtoto kwamba apate mazingira mazuri. Kwa hivyo ningeomba Mheshiiwa hebu tutitizame hili utatusaidiaje katika masuala kama haya ambapo inaonekana.

Mhe. Mwenyekiti, kuna jengine ambalo linakuwa sijui kwa serikali yetu lakini kwa serikali za wenzetu, mzazi anapopata hidaya ya watoto kuanzia wawili, watatu, wanne watano mpaka 10 kwa mimba moja. Sijui Wizara yako imeshajipanga vipi kwamba tunamsaidiaje mzazi huyu mwenye watoto watu aliyezaa kwa mimba moja au watoto wanne au watoto watano, Mwenyezi Mungu hajaribiki. Kwa sababu kwa wenzetu tumeshaona watoto mpaka 7 mpaka wanane anazaliwa na mama mmoja. Kwetu sisi unasikia *Alhamdulillahi*, wawili au watatu Mwenyezi Mungu atuwekee, lakini mtoto mmoja basi wewe na mumeo mnafanya mashauri ya kusaidiana ulezi, watoto wawili hali kadhalika inakuwa ngumu lakini watoto watatu na wengine inakuwa ngumu.

Je, serikali imeshaliona hili, imejipangaje au ndiyo serikali tayari sheria imeshawekwa kwamba wakizaliwa watoto zaidi ya wangapi serikali itachukua jukumu la kusaidia au mpaka tuje tuombe. Mimi ningeomba tujipange kwa sababu tuangalie tu kwamba wale watoto hawaji kusubiri huduma wakizaliwa tu wanataka huduma. Ningeomba kwa sababu yule baba haombi kama apate watoto kumi, wala yule mama haombi lakini ndio rizki imeshakuja. Ningeomba sana ili tuweze kuiangalia hali halisi ambayo itajitokeza kwa wale watoto na yule mama tunamsaidiaje kifedha, tunamsaidiaje kuwahudumia tunampaje muda wa likizo kama ni mfanyakazi, ningeshauri tukaweza kuitizama ili ikatusaidia.

Lakini Mheshimiwa nimeangalia humu kwenye ukurasa wa 36 kwenye kifungu cha 36 ukurasa wa 27 ni kwamba ina maneno mengi kuanzia ukurasa wa 36 kuhusu Mabaraza ya Vijana na Maendeleo yake, Mheshimiwa inasema itajenga uwezo wa vijana kupitia sekreteriati, vifaa vya ajili ya uendeshaji na shughuli za majukumu ya baraza litaunganisha Mabaraza ya Vijana, fursa za kiuchumi, kijamii, kiutamaduni, taasisi mbali mbali pamoja na kuendelea kuratibu pamoja na hiyo.

Lakini Wizara iweze kutekeleza majukumu mimi Mheshimiwa ningeomba kwamba kuna milioni 427,363,000 ambazo ni pesa ambazo naweza kusema kwamba ni pesa za Mabaraza na ruzuku sasa utakapokuja mimi naona ungetufafanulia kidogo uweze kutueleza hasa kwamba ruzuku ya hawa vijana watapata kiasi gani sioni ambayo hata kiambatanisho sikioni kwamba kipo lakini wewe mwenyewe najua ni mtaalamu zaidi.

Kwa hivyo ningeomba kwamba ruzuku zitakuwa ngapi na za uendeshaji zitakuwa kiasi gani ili tuweze kuangalia kwamba ruzuku zinatosha au hazitoshi na hii ruzuku kwa muda huu miye nataka kuangalia kwamba itakuwa ni lile Baraza la Kitaifa au mpaka huku Wilayani chini ni ruzuku hizohizo sasa nataka

uje utufafanulie kwamba hiyo ruzuku zinaanza wapi kwasababu tujue kwamba huku chini ndiyo kwenye kazi, sasa lakini ruzuku zenyewe hatujajuwa watapewa kiasi gani. Kwa hivyo ningeomba utakapo tufafanulia basi tuweze kujua kwamba masuala ni hayo.

Lakini miye nikija tena nije kwenye *pension* ya wazee Mheshimiwa mimi ningeomba sana kwamba tumpongeze Rais wetu Dk. Ali Mohammed Shein kwa kazi kubwa ambayo anaifanya lakini pia kuwaona wazee wanaofika miaka sabini...

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa mjumbe una dakika tatu.

Mhe. Suleiman Sarhan Said:: Nashukuru Mheshimiwa sawa wanaofika miaka sabini kwamba wazee hawa hakutaka idadi, wazee hawa hakufanya *limit* ya nini wale wanaofanyakazi wasiofanyakazi anayefika sabini apate *pension* ya Shs. 20,000/= ni pesa nyingi sana, ni pesa nyingi nyingi sana kwa sababu ya idadi ya watu hawa.

Lakini Mheshimiwa mimi nilikuwa nataka nikwambie kwamba nia safi ipo kazi mnaifanya lakini bado mimi nataka nikwambie kwamba hapa hapajafikiwa malengo, kuna mambo kama manne ambayo hapa yametendeka. Kuna moja ni kwamba idadi ya watu sio kamili ambayo bado ipo kwasababu nataka kukwambia Mheshimiwa sheria ndio msumeno hapa kuna watu wanapata hii pesa hawakupata pesa hii kwa ajili ya kwamba washafika muda, wamepata pesa kwa ajili ya sheria kwasababu wamejiandikisha ana miaka sabini na hapahapa kuna watu washazidi miaka sabini na tano mpaka thamanini watu hawa hawapati hii pesa kwasababu ya sheria. Maana najua kwamba kitambulisho chako ndiyo sheria lakini sasa tutizame dhana kamili nini ambacho tulikusudia hapa hasa Dk. Shein alikusudia mtu anayevuka miaka sabini. Lakini mimie nataka nimuombe tena Dk. Ali Mohamed Shein pamoja na mambo ambayo Mhe. Waziri nataka uyavalie njuga kuna watu wanaokufa bado utaratibu wao wa kurudisha masuala haya bado unafichwa. Kwa hivyo ningekuomba sana una kazi kubwa sana ya kuweza kupungua pungua mpaka ukajua idadi ya watu hawa kila siku maana yake hawa hawasimami wengine wanaingia wengine wanakufa, una kazi kubwa sana lakini pia nimuomba Dk. Ali Mohamed Shein apunguze miaka, miaka sabini hawafiki wengi muda ushakuwa mzito sana hata miaka sitini, sitini na tano basi ananisikia huko atupunguzie miaka....

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa mjumbe muda wako umemaliza

Mhe. nashukuru sana Mheshimiwa naunga mkono hoja asilimia mia moja nakushukuru sana Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Anayefuatiwa ni Mhe. Omar Seif Abeid naona hayupo nafasi yake itachukulia na Mhe. Jaku Hashim Ayoub.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti na mimi nikushukuru na niombe ku-*declare interest* Mhe. Mwenyekiti mimi ni Mjumbe wa Kamati hii iliyopo mbele yetu hapa tunapojadili na niendelee kumshukuru Dk. Ali Mohamed Shein kwa umakini wake na kuendelea kupiga vita dhidi ya watoto kuhusu unyanyaswaji na ubakaji.

Mhe. Mwenyekiti nachukua fursa hii kukmpongeza Waziri, Naibu wake pamoja na watendaji wake japokuwa sio wote lakini panapo ukweli tuzungumze ukweli.

Mhe. Mwenyekiti, mchango wangu utakuja kuanzia kwenye nyumba ya kulelea watoto Mhe. Waziri kilio hiki bado kipo na kinaendelea mabadiliko mliyoyafanya pale bado hayajazaa matunda, mmempeleka mtu lakini bado sijui kama mmepeleka au mmekwenda kusikiliza kuna nini kule au mmepeleka tu lakini bado kuna malalamiko. Mashirikiano na wafanyakazi hayapo tofauti na yule alikuwepo mwanzo kwa hilo Mheshimiwa hilo mlifikirie bado kuna matatizo pale.

Mheshimiwa mimi machango nafikiri utagawika katika sehemu mbili naomba ufafanuzi ukurasa wa 25 fungu Q01 fungu la programu hii la usawa wa kijinsia uendeshaji wanawake kwa kasma ya kujufunza, ukurasa wa 44 kiambatanisho namba moja kuhusu mchango wa fedha za matumizi kuanzia Julai 2016, Aprili 2017 zinaonyesha fedha zilizotengwa kwa kutumia kwenye mapambano dhidi ya udhalilishaji wanawake na watoto, fedha zilizotengwa ni Shs. 461 na zilizopatikana karibu asilimia 98.

Mhe. waziri, hizi pesa mlizopewa nyingi lakini bado utendaji wenu umekuwa na mitihani au misukosuko, Dk. Shein amejitahidi kukupeni pesa kwa asilimia 98 nimpongeze sana Mhe. Rais lakini bado watoto wanaendelea kunyanyaswa na kubakwa. Kwa maana hizi pesa mmepewa nyingi lakini bado kesi hizi hamzisimamii ipasavyo, nasema tena kwa mara ya pili wanabakwa ndani ya mikono ya Serikali na nilikueleza humu ndani asilimia 98 Dk. Ali Mohamed Shein amejitahidi sana kuweka pesa karibu milioni 451,000,000 ni jambo la kumshukuru sana Mhe. Rais.

Lakini bado usimamzi wenu una changamoto kubwa pamoja na kelele tunazopiga waheshimiwa wawakilishi watu wako ndani sio kidogo hivi sasa lakini kuna wengine hizi kesi wanasukumiwa tu kwa maonevu. Hawa mahakimu ninawaombe sana wawe makini kuhusu suala hili. Mfano Mhe. Jazira sio kabaka tuchukulie kama mfano mimi mwanamke kanitaka huyu, mimi sikumtaka atanitafutia sababu kuja kuniletea hata mtoto mdogo kuja kunisingizia, hiyo kesi nishaikuta mimi. Kwa hivyo kidogo muwe makini haya maneno mkipewa muyafatiliye, bado kuna watu wanasukumiwa hizi kesi kuna nyengine za ukweli nyengine si za ukweli lakini hizi pesa mlizopewa ni nyingi lakini utendaji wenu bado unasuasua, kwa hivyo mchukuwe tahadhari hizo.

Jengine Mhe. Waziri ukitazama pesa zenyewe hazendi na matokeo yenyewe na jengine naomba kupata ufafanuzi mchango wa matumizi ya fedha hizi ukoje kwani wizara imepewa hizo asilimia 98 bado, bado, wanashindwa.

Nije katika hoja ya pili kiambatanisho namba 2 ukurasa wa 45 kuhusu Taarifa za Ukusanyaji wa Mapato ya Julai-Aprili 2016 vyama vya Ushirika Mheshimiwa, mmepata karibu milioni 120,000,000 ukaguzi na milioni karibu 50,000,000 na 70,000,000 hiyo ni 120,000,000 hoja yangu kuhusu usimamizi wa vikundi vya ushirika sawa vinasajiliwa kulipa ada lakini vinapokwenda benki vinarudishwa, vikundi hivi sijui tatizo nini.

Hoja yangu nyengine Mhe. Mwenyekiti, katika kitabu hichi *volume* 2 kwenye Q01 Programu ya Kukuza Usawa Kijinsia Uendeshaji wa Wanawake kasma ya kijifungu HQ 01020106 kudhinisha Siku ya Wanawake duniani pesa milizochukua ni nyingi milioni 112,000,000 za kazi gani sherehe gani hiyo, milioni 112,000,000 kifungu hichi siyo maneno yangu yamo kwenye kitabu hichi, za kazi gani milioni 112,000,000 sherehe gani hiyo mnataka kufanya? Kuna harusi ya aina gani hizi pesa wananchi wetu wanakosa maji hasa Michamvi hapa itabidi nipate ufafanuzi si maneno yangu yamo kwenye kitabu hiki milioni 112,000,000 sijui sherehe za aina gani wizara haina vipaumbele vyengine kwa pesa hizi kwani fedha hizi zisipunguzwe zikatusaidia angalau wananchi wa Michamvi na Ramadhani inakuja huko.

Mheshimiwa nafikiri baada ya kupangua fungu zima nitahitaji maelezo jengine ukurasa wa 25 Programu za Kuimarisha Huduma za Ustawi wa Kijifungu HQ01030104 Kuratibu Uendeshaji wa Vituo vya Kulelea Watoto Yatima hapa pana bilioni saba laki tisa lakini kuna vifungu vile vile.

Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa skuli kuna hesabu ina *simultaneous equation* ina *two methods* njia mbili za ku- *solve, elimination method* na *substitute*

method jawabu yake ni ile ile moja hasa hizi bilioni saba (7,000,000,000) zimekatwa huyu kapewa huyu lakini lengo ni lile lile moja na hapa nitahitaji meelezo bilioni saba (7,000,000,000) lakini kuna milioni tatu laki moja (3,100,000) lakini njia ndio ile ile ya kupita hapa, imepindua hivi ikawekwa hivi lakini hapa nitahitaji maelezo, ndio nilosema kuna hesabu unaweza ku-*solve* kwa njia mbili na jawabu yake ni ile ile moja.

Mheshimiwa kuhusu Maendeleo ya Vijana milioni mia tatu na hamsini (3,050,000) na hizi nitahitaji maelezo zinahudumia kazi kwani kijifungu zaidi ya kimoja kimepangwa ile mfano wa bilioni saba (7,000,000,000) nilizosema za mwanzo ndio njia ile ile maana yake na hii natahitaji maelezo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo mimi nitakuwa sina makubwa sana hii ni Wizara yangu na nitahitaji maelezo baada ya vifungu nitakuwa sijaifanyia haki kama sikuhoji vifungu, ukizingatia fungu hilo Mheshimiwa la Udhalilishaji limewekewa pesa kidogo nalo. Lakini ndio yale niliyosema mwanzo huku wamepewa nyingi lakini wala si nyingi hizi vile vile zipunguzwe hizi pesa, utendaji bado umekuwa ni mdogo.

Mheshimiwa baada ya maelezo hayo, akishakunielimisha maana yake nimesema tena elimu yangu mime ni ndogo siku zote ndio hutaka kuelimishwa, akisha kunielimisha sina matatizo naye mimi.

Mhe. Mwenyekiti, sitounga hoja mkono mpaka nitakapopata maelezo. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Jaku sasa anafuatia Mhe. Abdalla Diwani anachukua nafasi na baadaye atafuatia Mhe. Nadir

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mwenyekiti kwa kunipa fursa kuchangia hotuba ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana na Wanawake na Watoto na mengineyo awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu sana kwa kunijalia uzima sasa hivi nikasimama mbele ya Baraza lako tukufu.

Pili nampongeza sana Waziri kwa uwasilishaji wake wa bajeti alivyoisoma kimadaha na mbwembwe na kitabu kizuri.

Tatu napenda kuwapongeza watendaji wote wa Wizara hii kuanzia Waziri, Naibu Waziri, Katibu Wakuu na Wakurugenzi wake wote pamoja na Maofisa nikienda moja kwa moja kwenye mchango wangu napenda kutoa makosa

katika kitabu hiki, kwa sababu tushazowea kitabu chochote kinachokuja kinatakiwa kiwe na *contents*, yaliyomo ili iwe rahisi kuangalia wapi unapotaka. Lakini hiki kitabu kimefunguliwa tu kikawekwa utangulizi hapa basi hamna ile yaliyomo. Kwa sababu ukitaka kuangalia Baraza la Vijana ilikuwa iweko hapa ikuongoze kwenye ukurasa wa ngapi hilo moja.

Pili nakwenda katika suala la Ustawi wa Jamii napenda kumpongeza sana Waziri natumai ule usikivu wa maelezo ya Kamati ya Habari na Ustawi wa Jamii imefanya kazi natamka mbele ya Baraza lako Tukufu nimewahi kutembelea nyumba ya kuhifadhi wazee pale Sebleni na nikafanya ushawishi nikazungumza na mabibi wa pale na mama kwa kweli wanasifu mabadiliko yalofanyika pale. *(Makofi)*

Sasa hivi angalau zile nyuso zao zinaanza kukunjuka kwa sababu unajuwa kama wale watu wanashiba zile milioni saba (7,000,000) na milioni sita (6,000,000) zilizoandikwa zinatumika kweli. Sasa hivi angalau mama anakwambia nashukuru sasa hivi nakula matunda, nakula samaki, nakula chipsi kuku, hongera sana Mhe. Waziri. Lakini hongera hizo nisikupe wewe tu, nimpe yule msimamizi wa pale aliyekuwepo simjui nani lakini ukweli usiofichika kwamba kafanya kazi ya maana kajitoleya. Kama ingekuwa hawatimizii yale lazima wangesema lugha mbaya, lakini kwa sababu anawajali na anawathamini wale wazee wetu pale ndio maana wakamsifu walinipa sifa mpaka wengine wanataka kulia kwa sifa za yule mdhamini wa pale hongera sana Mhe. Waziri katika kulifanya hilo. *(Makofi)*

Lakini katika maelezo yangu yale nikaongea nao sana tu pale kuna changamto ile TV yao pale watengenezeeni maana yake wale watu wazima kikubwa wanataka taarifa habari pale, TV yao ile na wao angalau wasijilikie kama wanalelewa katika nyumba ya Kuhifadhia Wazee pale Sebleni angalau wapate taarifa za habari namna gani.

Si hilo tu hata katika maelezo yake hizi pongezi zisingekuja bure kama sikumpongeza Mkurugenzi wa Ustawi wa Jamii anaitwa bibi mmoja naomba nimtaje Bi Wahida Maabadi hongera sana huyu mama mimi simjui, anafanya kazi nzuri na anasifika kumbe watendaji wa kazi tunao lakini tunawabania hatuwapi nafasi, kweli nakushukuru sana e wanawake kumbe mnaweza hongereni sana kwa hilo. *(Makofi)*

Lakini nikiendelea mbele pamoja na vyakula vizuri, mambo mazuri bado kuna changamoto pale jengo lile pale kuna wazee wetu wengi watu wazima, ningeomba Waziri sana kwa huruma kabisa angalau pale uwapatie nessi ili

panapotokeza tatizo lolote usiku iwe rahisi kupata matibabu hawana nesi pale na pale hutokezea *time* pale kuumwa inakuwa shida na sio tu hata usafiri wale hawana. Pana wazee pale hawapungui thalathini na moja, ningeomba sana Mheshimiwa japo ukatafute japo kijigari pale kikae angalau ikitokezea tatizo kidogo kiweze kuwasaidia kuwahisha hospitali na shughuli nyengine kwa sababu wale ni binadamu, huwezi kujua saa ngapi maradhi yatakuja. Ukiwawekea kigari cha milioni milioni nne, milioni tano, milioni sita utakuwa ushawasaidia jambo la maana na wale wenyewe watakuwa washaona raha.

Nikitoka hapo pamoja na pongezi zote hizo bado kuna changamoto ndogo tu ambayo niloulizia ulizia pale nikaambiwa kwamba pale pana mzabuni ambaye analisha pale. Kulisha kwake yule mzabuni na *procurement* wao kidogo pana matatizo naomba sana Mhe. Waziri aliangalie juu ya matumizi wanayofanyia pale. Pale *maximum* matumizi hayavuki milioni sita (6,000,000) lakini inafika *time*, huyu mzabuni anapeleka mpaka milioni nane, milioni tisa kwa chakula kile kile kwa kweli hilo kidogo tuangalie wanatupiga changa la macho. Tunawapenda wazee na tunawahifadhi wazee lakini hawa wazabuni hawa sijui sheria za *procurement* zinasemaje kama kweli kuwalisha wale wazee mpaka tenda ya milioni sita (6,000,000), milioni saba (7,000,000) kwa mwezi na ikiwa basi ikiwa hakuna sheria inayowabana basi iweke pale *cash flow* wale wazee wale vizuri zaidi kwa sababu hata sehemu nyengine mfano Welezo, Pemba, hakuna mzabuni na wanaishi vizuri.

Jengine nakwenda katika ukurasa wa 20, Programu Ndogo ya Uratibu wa Huduma za Uhifadhi wa Jamii. Napata wasiwasi na Mhe. Waziri atapokuja naomba anisaidie majibu, naomba ninukuu, "Inaendelea kuwahudumia Wazee 73 (Unguja 64 na Pemba 9) wa Welezo, Sebleni na Limbani. Lakini napata wasiwasi umesema kuna waathirika wa ukoma, hawa waathirika wa ukoma si wale waliokuweko kule Welezo? Imewekwa 55. Kwa sababu pale Sebleni mpaka jana pana Wazee 30 kama umefanya kazi zake vizuri umekwenda kufuatilia pana wazee 30, mmoja pale kaondoka siku tatu nyuma nimeambiwa hayupo.

Sasa ningeomba sana hapa uangalie, pengine hilo changa la macho la mzabuni linakuja hapa kuwalisha wazee 64. Je, 64 hawa wametoka wapi, kwa sababu imeandikwa 64 Unguja kwa kufanya hesabu ambayo imesemwa tisa (9) Pemba, Unguja hii pengine wa Welezo na Sebleni. Lakini ikasemwa huku kuna waathirika wa ukoma 55 ambao najua waathirika wa ukoma mji huu wanawekwa Welezo na wako 34. Naomba sana Mheshimiwa utapokuja hili uniwekee sawa ili tupitishe bajeti yake kwa vizuri na starehe huku tukicheka.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea mbele katika kitabu hiki nakwenda kuchangia ukurasa wa 27 Baraza la Vijana. Najua Baraza la Vijana limeanzishwa kwa sheria Nam. 13 ya mwaka 2016. Nimpongeze sana Mhe. Rais kuleta hii sheria kuona vijana wamepata kimbilio lakini liko tofauti yake, tumeanzisha Mabaraza kwa kishindo hapa lakini sasa hivi nafikiri Mabaraza yote sifahamu sijui niseme kama yako regerege au yamekufa au vipi, ilikuwa kila pahala tunashikwa tuzindue Mabaraza tumezindua lakini leo hii huyasikii hata yanafanya *activity* gani, yanafanya *activity* gani kwa sababu ya matatizo ya fedha, fedha hakuna.

Vile vile katika hiki kitabu chake pia kinanipa mashaka, naomba ninukuu: "Imekamilishwa uundwaji wa Mabaraza ya Vijana ngazi ya Shehia, Wilaya na Taifa, ambapo Mabaraza ya Vijana 52 ya shehia yameundwa", sio kweli. Sijui kama amekwenda nje ya muda huu, najua sasa hivi Unguja na Pemba kuna Mabaraza hayapungui 384 sisi si watendaji wa Ustawi wa Jamii, Wanawake na Watoto, lakini hesabu ndio hiyo. Sasa humu katika kitabu imeandikwa mpaka sasa hivi leo hii yameshaundwa Mabaraza haya basi hamfanyi hiyo kazi ati, kwa sababu wametuletea hesabu hizi sizo, niseme lugha gani itayokuwa nzuri isiyochokoza akasema ah, niseme hesabu hizi za uongo. Mabaraza 11 hayana shaka tunajua saba wilaya za Unguja nne wilaya za Pemba hapo umepatia, lakini katika shehia naomba sana aniambie atapokuja katika suala hili la Baraza.

Mhe. Mwenyekiti, lakini isitoshe hapo tu, amesema hapa itajenga uwezo wa Baraza la Vijana kupitia sekretarieti vifaa kwa ajili ya uendeshaji shughuli za majukumu ya Mabaraza, itashughulikia Mabaraza ya Vijana, fursa za kiuchumi, kijamii, kiutamaduni katika taasisi. Ni kweli nakushukuru sana kwa kuandika kitabu hiki vizuri sana lakini kiutendaji ndio ninaposikitika. Ningeomba sana haya yaliyoandikwa hapa yaende sawa sawa na vitendo vyake na akifanya hivyo basi *Wallahi-laadhim* vijana watamuombea dua gani sijui Mhe. Waziri atakuwa waziri mwenye sifa kubwa sana. Lakini napata wasiwasi huku tumezungumza Baraza la Vijana tunakwenda mbele tunakuta wizara inaweza kutekeleza programu ya maendeleo ya vijana, tayari imeshakwenda kwenye idara yake, Idara ya Vijana. Tumetoka kwenye Baraza la Vijana tumeiandikia katika Idara ya Vijana akasema kwamba amewatengea shilingi 427,363,000. Je, hizi pesa ni kwa ajili ya Baraza la Vijana au Idara ya Vijana aliyokuwanayo pale ofisini kwake?

Kama ni Baraza la Vijana anaigawa pamoja fungu hili basi atuainishie Baraza la Vijana wanapata ngapi na Idara yake ya Vijana wanapata ngapi ili tusipate shida kuichambua bajeti hii. Hapa ametupiga changa la macho, kwa sababu

hata hilo Baraza la Vijana hakuna kasma yao iliyowekwa katika kitabu hiki. Ningemuomba sana Mhe. Waziri katika suala hili la vijana aliangalie kwa sababu nina imani na mimi bado niko katika kundi lile lile la vijana nataka vijana wetu nao wasisikitike sana. *(Makofi)*

Sio hivyo tu, hata sasa hivi kwa jitihada zao wale vijana wanahangaika angalau wawezeshwe, kuna wale jamaa wa *UNFA* wamefikia wapi katika suala zima la kuwawezesha wale vijana juu ya suala la kuwajenga uwezo. Kwa sababu walikuwa wanahangaika hapa nyuma sijui hatua gani waliofikia. Ningeomba kama waziri najua unajua ana watendaji wake wengi sana pale watamueleza ili nipate kuwa shahidi katika suala hilo.

Mhe. Mwenyekiti, vijana hawa hawa tunawaambia sasa hivi kwamba tunawajengea uwezo ukiangalia *majority* vijana hawa chini ya asilimia 60 wote elimu zao ndogo ni *Form IV* kushuka chini. Sasa ningeomba sana lazima kufanywe jitihada ya dhati kabisa kuona wanasaidiwa vijana ili waondokane na malalamiko kuona kwamba wameundiwa Mabaraza lakini hawana hata kimoja wanachokijua katika Mabaraza yale. Ni shahidi katika Baraza hili juzi iliulizwa hata ofisi ya Baraza Taifa haipo, kwa sababu alama ya ofisi ni kuwa na bango nje ikatambulika kuwa hii ofisi ya pahali fulani hakuna kitu kama hicho. Unguja nzima ukitembea hukuti Ofisi ya Baraza la Vijana Taifa ambayo imewekewa bango hata mgeni akija anaweza kuona. Ningemuomba Mhe. Waziri awatafutie ofisi wakishapata ofisi itakuwa afadhali pa kukimbilia.

Mhe. Mwenyekiti, sio ofisi tu hata mamlaka wanakosa mamlaka kutokana na hili Baraza ni taasisi ambayo yenye kujitegemea na ndio maana likawa na sheria yake, mkurugenzi wake, lakini haiwezekani leo kila kitu aje aripoti kwa Katibu Mkuu, kwa Mkurugenzi wa Ustawi wa Jamii au Wanawake na Watoto. Je, suala langu hii ni taasisi au idara katika serikali yake au ni Baraza likiwa *independent* linajitegemea kama Baraza la Vijana? Kama Baraza la Vijana wana mamlaka yao kamili muwatengee kasma yao hii hapa Baraza la Vijana muendeshe shughuli zenu, lakini kwa kutuzonga hivi tu tunachezeshwa mpira hatujui nini mustakabali wa hilo Baraza la Vijana.

Nikienda mbele nakwenda moja kwa moja kiambatanisho Nam. 12, naingia katika Q010201 Mapambano dhidi ya Udhalilishaji watoto. Nimeona hapa imetengewa shilingi 55 milioni *we are serious?* Tuko kwelini katika hicho? Kwa mwaka mzima utuwekewe kifungu hiki cha shilingi 55 milioni aseme ni mapambano dhidi ya udhalilishaji wanawake na watoto wa Zanzibar tutakwenda vipi pesa hizi, fungu dogo sana hili kutokana na vita tulivyokuwanavyo sasa hivi ambavyo vinahitaji jitihada ya dhati kabisa, tena

nasema kwa msisitizo hizi pesa ndogo sana Mhe. Waziri hazitoshi, lazima tuongeze fedha hapa.

Ukienda mbele nakuta Q010402 Utawala na Uendeshaji kuna 1.4 Bilioni, lakini huku katika vita ziko hivi. Ningeomba hiki kifungu tukipunguze tukipe nguvu kifungu cha udhalilishaji. kwa sababu ndio tuko kwenye vita na naomba wajumbe mnisaidie katika hilo, lazima hiki kifungu tukinenepeshe, kifungu cha shilingi 55 milioni kwa mwaka mmoja ni pesa ndogo, nitawaomba wajumbe wenzangu sana katika hili, tusimamie tuone hiki kifungu kinaongezwa kwa sababu ndio vita kila siku ukicha hivi vita vipo vinaendelea lakini hizi pesa za kuratibia vita vile ni pesa ndogo. Lakini katika mambo mengine ya anasa yameongezwa fedha, sikubaliani na hicho nitakuomba sana Mhe. Waziri katika hili aliangalie akae, nafikiri hata Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti yupo anisaidie kukamata kifungu hiki, lazima hiki kifungu kiongezwe fedha ili kiendane sambamba na harakati tulizokuwa nazo na kupunguza fedha katika suala la utawala na uendeshaji.

Mhe. Mwenyekiti, tunajua au tunapambana na siku zote ukimuonea haya mke ndugu watu wanasema huzai naye, msemo wa Kiswahili huo sio wangu mimi. Mhe. Waziri najua anapambana sana panapo majanga upo, anasema sana, lakini bado katika watendaji wako katika suala zima la kusaidia vikundi vyetu liko tafauti. Kuna malalamiko mengi sana katika suala la vikundi vyetu.

Humu katika vikundi niliona viko vikundi vingi vimesaidiwa lakini uhalisia haikutani nao. Mimi mwenyewe ni shahidi nimeshahangaika sana na baadhi ya vikundi, anaye Mkurugenzi wake mmoja anaitwa Simba nimeshahangaika naye sana juu ya kuviangalia mustakabali atatusaidiaje katika vikundi vyangu, mpaka leo Mhe. Waziri sijafikia mwisho, sijui nimekwama wapi, sijui kuna tatizo gani, wala sijui nifanye nini ili niweze kufanikiwa. Najua pengine Bwana Simba yupo ananisikia juu lakini hiyo ni kesi ya kwake ningeomba sana katika hicho anisaidie na mimi kama waziri, ili na mimi jimbo langu la Jang'ombe lifaidike na huu Mfuko wa Uwezeshaji ili watu na wao waende mbele.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa sina mengi ya kueleza ni hayo lakini siungi mkono hoja mpaka pale waziri atakapokuja kuniridhisha na masuala yangu niliyoeleza baadae ndio nitaunga mkono. Kwa hivyo, nashukuru sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante, pamoja na kwamba hujaunga mkono lakini waziri atakutosheleza, nafasi iliyobaki nampa Mhe. Nadir Abdul-latif.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: *Bismillah Rahmani Rahiim.* Mhe. Mwenyekiti, mimi kabla sijaanza nitaipongeza sana kamati na nawapongeza kwa sababu wamezungumza vitu ambavyo vina maana sana ndani ya maelezo yao, lakini pia nampongeza Mhe. Mjumbe ambaye amepita hivi punde Mhe. Abdalla Maulid Diwani kwa kueleza kitu makini kabisa ambacho tunahisi kwamba hakijafikiriwa.

Mhe. Mwenyekiti, nikija kwenye wizara sijui nimpongeze nani watanisamehe kwa sasa hivi mpaka baadae nitakumbuka nani naweza kumpongeza.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitaanza na suala moja ambalo zuri sana walilolianza wenzangu kamati pamoja na Mhe. Abdalla Maulid Diwani la programu ya udhalilishaji. Kwa kweli serikali kwa ujumla na wizara husika inapiga kelele sana kwenye suala la udhalilishaji, lakini ukiangalia fungu halisi la shilingi 55,100,000 sio fedha ambayo itaweza kufanya kazi kwa mujibu wa malengo wanayoyataka. Sasa cha msingi kama tuko *serious*, kama serikali inataka hili suala liende vizuri bila ya vikwazo ambavyo vitakwamisha wizara husika, kama wanahitaji hili suala lifanikishwe, liende vizuri watu wasikwame kwenye kazi zao basi kwenye kifungu hiki walichokieleza baadhi ya wenzangu cha Utawala na Uendeshaji, Q010402 kilichoingiziwa 1.6 bilioni, (1,685,551,000) hapa angalau basi Waheshimiwa Wajumbe wenzangu tumege shilingi milioni mia tano kwenye fungu hili ili likaingie huko kwenye shilingi 55,100,000. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, hili suala ni muhimu sana na ni suala ambalo linataka kusaidia wananchi wote ambao wanafanyiwa udhalilishaji katika nchi yetu. Ningeomba sana Wawakilishi wenzangu watapokuja hapa tulifikirie hili suala na hapa kwenye suala la utawala basi angalau tutoe hizo fedha shilingi 500 milioni ziende huku au ukosefu kwenye shilingi 250 milioni nusu yake.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitaendelea kwengine kidogo kidogo kwenye suala la wazee. Suala la wazee ni muhimu sana katika nchi yetu. Kwanza nimpongeze sana Mhe. Rais. Dkt. Ali Mohammed Shein na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuwawezesha wazee hawa na kuweka mfano katika nchi nyingi sana duniani, basi ni moja ya nchi ambayo inataka mfano kwa kupitia uongozi wake kuweka shilingi 20,000 kuwajaalia wazee pamoja na mambo mengine ya kuwajali wazee.

Tukiangalia leo tunasikia fedha za wazee watu wanazila na ukweli uliokuwepo ni kwamba zimeliwa, fedha hizi Mhe. Waziri akija aje atujibu ni kiasi gani cha ubadhirifu umefanyika walichodhulumiwa wazee hawa. Watu wa namna hii

katika wizara yake kama wanakula fedha hizi za wazee wanyonge ambao wamesha-*over* miaka 60 halafu watu wanakuja wanazichukua wanabakishiwa nini kwenye wizara. Kwa sababu watu kama hawa wanaweza hata wakauwa baadae, ukiona mtu anaweza kumdhulumu mzee shilingi 20,00 ya kutumia chakula mzee mgonjwa ujue hao watu hatari kufanya nao kazi na hii inamuangusha Mhe. Rais katika ahadi zake na malalamiko mengi. Tungeomba sana wizara itapokuja hapa ije itueleze sawa sawa ni watu wangapi ambao wamekamatwa ambao wamefanya ubadhirifu wa pesa hizo za wazee na nini kinaendelea mpaka sasa hivi au adhabu gani wamechukuliwa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi mchango wangu mwengine pia kwenye wazee. Ningeomba sana wizara husika iangalie kwenye kila mikoa basi ikajenga nyumba za wazee wakapata wale wazee wa Kaskazini wakawa wanahifadhiwa Kaskazini, wa Mjini Magharibi wahifadhiwe Mjini Magharibi, wa Pemba Kusini wakahifadhiwe Pemba Kusini; lakini leo nyumba za wazee ziko mjini Zanzibar tu labda na huko Pemba. Mimi ningeomba wizara yake ijitahidi ijenge maeneo ya wazee kila mkoa ili wale wazee wa mkoa waliokuwa hawajiwezi wahifadhiwe kwenye mkoa wao wasiletwe mjini, wazee wapo ambao wanataka kusaidia katika mikoa mengine lakini bado hawajaweza kuwaona. Sasa leo mtapokuja kujenga nyumba nzuri, maeneo mazuri, makaazi mazuri ya kuwahifadhi wataweza kujipeleka pale wakenda kustirika kuliko wanavyoumia sasa hivi.

Mhe. Mwenyekiti, niendelee kwenye suala la Wizara ya Kazi. Kwa kweli ukiangalia kwenye kitabu hiki wameeleza kwamba kuna vijana wengi au wananchi wengi wamewapatia ajira katika nchi za Kiarabu karibu tano zimetajwa hapa ikiwa Oman, Dubai nafikiri na Qatar na nchi nyengine kama tano hivi. Lakini mimi ningeuliza ni sababu zipi ambazo wame-*target* kuwatafutia ajira kwenye nchi za Kiarabu kwa nini nchi nyengine hawakuzitaja wakati wako watu wa nchi nyengine wanaweza wakapata ajira wananchi wa Zanzibar. Kama walivyosema kwamba wameweza kuwasaidia kupata ajira Dubai, Oman na nchi nyengine za Kiarabu kwa nini hawajatafutiwa ajira Canada, Marekani, United Kingdom, South Africa na sehemu nyenginezo na watu wanahitaji wafanyakazi. Sasa Mhe. Waziri atapokuja aje atujibu ni utaratibu gani ambao wameufanya kwamba wame-*focus* kwenye nchi za Kiarabu tu na hawaja-*focus* kwenye nchi nyengine za kuwasaidia Wazanzibari wakafanye kazi kwa njia nzuri.

Vile vile mimi ningependekeza hawa watu ambao wanaondosha wafanyakazi basi wangechaguliwa watu wachache ambao wanaaminiwa wametimiza vigezo, wanahisi hawa waaminifu wakaweza kuondosha wale wananchi kwa

kushirikiana na wizara husika kwenda kuwapeleka kwenye maeneo ya kazi. Lakini leo unaweza kuja kukuta pengine nje kuna watu ambao si wazuri wanaondosha wafanyakazi, lakini kuna watu ambao wanaweza wakawa hawana ofisi lakini ni watu wazuri ambao wanafanya vizuri, wangekaa nao wakashirikiaa nao kwa pamoja ili wananchi wakaweza kupata kazi na ajira kwa wepesi zaidi kwa kushirikiana na wizara na mtu binafsi.

Mhe. Mwenyekiti, jengine nitakwenda kwenye ajira. Zanzibar bado vijana wengi ajira hawana, vijana wa kike, wa kiume ajira hawana. Hii ukiangalia ukienda kwenye mahoteli na Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo yupo hoteli asilimia 99 wafanyakazi sio Wazanzibari. Mimi ningeomba sana ingewekwa sheria maalum mtu yeyote anayefanya *investment* ndani ya Zanzibar ikiwa kiwanda, ikiwa biashara yoyote, ikiwa hoteli iwekwe asilimia basi kama anataka wafanyakazi mia yawekwe masharti maalumu kwamba wafanyakazi 50 achukue Wazanzibari. Kwa sababu kwenye hoteli na viwanda wafanyakazi wachache tu ambao wakubwa kwenye *department* kubwa ndio wanaotakikana, kwenye hoteli wafanyakazi kuanzia *manager* labda wengine *front office manager*, ma-*accountant* hawazidi 20 kwenye mahoteli makubwa.

Mfano mdogo umetaja hoteli humu ndani ya kitabu Melia Kiwengwa, wana wafanyakazi karibu 360 miaka ya nyuma lakini cha kusikitisha ukienda pale wafanyakazi wa Kizanzibari wazalendo hawafiki hata 35. Mimi ninachotaka kusema sio kweli kwamba Wazanzibari hawawezi kazi hii ni kwamba wizara haijafanya kazi ya kuwa-*push* hawa ma-*investors* na ambapo watu waliokuja ku-*invest* kuwashikilia kuwaajiri wafanyakazi wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, leo tunaona ikiwa ndugu zetu wa upande wa pili Tanzaia Bara sio tatizo kupata ajira, lakini kuna Wakenya, kuna watu kutoka India, kuna watu kutoka nje ambapo kuna kazi nyengine wanaweza kufanya Wazanzibari ndugu zetu Wazanzibari wamesoma, leo nchi hii ajira ngumu huku watoto ndio maana wanaingia kwenye madawa ya kulevya, wanaingia kwenye masuala ambayo hayana maana. Mimi naomba sana wizara mbili hizi husika pamoja na Wizara ya Katiba na Sheria washirikiane kuwapa masharti ma-*investors* wote ndani ya nchi hii waweke asilimia maalum ya kuajiri Wazanzibari. Naomba sana kwa sababu sasa hivi ukiangalia hata ukienda Tanzania Bara kukuta Mzanzibari katika mahoteli ni kitu adimu sana, lakini huku Wakenya makabila mengine wengi, kwa nini wizara wanaachilia hivi vitu wamefanya utafiti na kwenye ripoti yao hawajaleta utafiti huo kwenye mahoteli; wamepita wakaangalia Wazanzibari kama wamepata *opportunity* gani. Mimi nitaomba Mhe. Waziri atapokuja aje anijibu ndani ya Zanzibar hii

mahoteli na sehemu nyengine zote zinazomuhusu kwenye masuala ya ajira kuna wafanyakazi Wazanzibari wangapi wamepata ajira na waliokuwa si Wazanzibari wangapi wapo tukapata kujua.

Mhe. Mwenyekiti, kwenye suala la vijana ukiangalia vijana taifa kusema la kweli ni jambo zuri, lakini kwenye shehia na wilaya ndio pa kusaidia wakapewa fedha na ndio kwenye watu wengi, lakini leo tunaangalia vijana taifa moja kwa moja. Mimi ninachoomba kwamba akija hapa atueleze Mhe. Waziri ni sababu zipi walizo-*focus* juu tu hawaja-*focus* chini na huko ndiko kwenye watu, kwenye shehia na wilaya, kwenye vijana wengi, fedha hizi zimeelekezwa wapi waje watujibu, fedha hizi zianzie wapi kwenye taifa, vijana au wilaya.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe subiri kidogo, Waheshimiwa minong'ono inakuwa mikubwa hotuba yake haisikilikani naomba utulivu.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwaeleza kwa sababu huu ndio mtindo unaoendelea kila siku. Mhe. Mwenyekiti, mimi nilichokuwa nakieleza kwamba wizara ije itujibu ni utaratibu gani wanaotumia hivi fedha zinafaidisha taifa wasifikirie kuanzisha kwenye shehia na wilaya kwa upande wa vijana. Kwa kweli vijana wanaachiliwa wanasahauliwa wanakumbukwa sehemu kubwa kubwa, tungeomba sana tu-*focus* huko chini ndio kwenye watu hivi vitu vya juu, *management* za juu hazina watu wengi sio walengwa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitakwenda kwenye udhalilishaji, kwa kweli Zanzibar bado udhalilisaji upo na ndio maana nikasema mimi sitaki kumsifu mtu yeyote kwenye wizara hii, sitaki kumpendelea mtu bora nisisifu. Kwa sababu wizara hii bado haijafanya kazi ya kutosha ni watu wachache sana wa kuwahesabu na mimi siwajui ndio maana sitaki kumsifu mtu. Sasa ninachoomba cha kushangaza ndani ya nchi hii mtu anayeiba ndizi, madafu *Wallahi* watu watamuua lakini leo mtu anayebaka anapelekwa polisi kwa nini wasimmalize huko kwa huko, hili suala ndio maana sisi tunataka ije sheria hapa ya mtu kunyongwa anayedhalilisha watoto Lakini ukiangalia suala hili limewekwa jepesi sana hawachukuliwi hatua, watu wanauwa kwa madafu tu nje mtu kaiba ndizi wamemuuwa, lakini mtu anayebaka analindwa.

Mhe. Mwenyekiti, cha kushangaza zaidi kuna wazee wanasikitishwa wanachukua fedha baada ya mtoto wao keshabakwa anarudishiwa pesa anamuachilia na kesi anabadilisha. Mimi wazee wa namna hii nitawaita sio wazee ni wanyama, kwa sababu haiwezekani leo mzee unakuta anajifungua anakwenda kumtupa mtoto kwenye karo anamuuwa, anamrusha sehemu

ambayo sio nzuri hayo mambo aliyataka vipi mwanzo, mbele huko tutakwenda kujibu nini. Wizara hii mimi naomba sana ije itwambie wanafanya utaratibu gani, utafiti gani wanaofanya kupunguza haya mambo mbona mambo yanazidi kila siku Mhe. Rais anapiga kelele yanamuumiza, lakini wizara bado tunaona vitu vinazidi. Mimi sisemi kama wizara wanayataka yatokezee lakini tuone nguvu gani wanaitumia kusimamisha masuala ya udhalilishaji nchi hii.

Sasa hivi Zanzibar udhalilishaji umekuwa na jina baya, masuala ya ubakaji imekuwa *too much* Zanzibar ina jina baya sana na wizara yake ndio husika na mimi nahisi tusipendekeze sisi hata yeye apendekeze sheria kali za kuwanyonga hawa watu haiwezekani. Tunaona kila siku mimi nazungumza kitu ambacho kiko wazi, tunaona kila siku wezi wa madafu, maringi wanachomwa nje lakini wabakaji kwa nini wanaachiwa wamalizwe huko huko wasipelekwe polisi. Kuna wazee hawana imani wazee wanahadaika na fedha na hawa ndio wazee ambao sio watu kwamba wako tayari kuchukua fedha kuwaumizisha watoto wao, kuwaozesha watoto wao na wabakaji na kuachilia haya mambo. Mimi namuomba Mhe. Waziri asiwe na *pressure* aje atujibu maswali yetu tu.

Kesho tukijaaliwa aje atujibu maswali yetu vizuri tutafahamiana, tena yaje yawe yenye maana. Kwa sababu kuna vitu vinazungumzwa tunavijua haviko sawa.

Tukienda kwenye suala la Mfuko wa Wazee zile fedha shilingi 20, 000 utaratibu gani hasa aje atueleze unaotumika kwenye kugawa zile fedha. Hilo swali langu jengine.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nisiendelee sana kwa sababu maswali yangu nimeshamuuliza, lakini nimpongeze sana Mhe. Rais jambo hili linamuuma na kafika kufungua Mahkama ya Watoto, lakini sasa kama wizara husika haitotaka kufanya kazi ya ziada Mhe. Rais kwa ujumla atavunjika moyo na sisi tutavunjika moyo. Mimi namuomba sana watu wote wanaodhalilishwa na mambo mengine yote yanayohusiana na wizara yake aje atujibu vizuri na haya mambo atwambie ametumia njia gani ili kuweza kuona kwamba yataweza kupungua kwa wingi kuliko hivi sasa yanavyozidi kwenda.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana na ninakupongeza wewe kwa kunipa nafasi. Wizara nimesema sijui wa kumpongeza nani nitaendelea siku nyengine ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante. Waheshimiwa Wajumbe kwa kuwa muda umefikia na hadi hapo naliakhirisha Baraza hili hadi kesho saa tatu asubuhi.

(Saa 1:45 usiku Baraza liliakhirishwa mpaka tarehe 23/05/2017 saa 3:00 asubuhi)